# Njoo Nifuate

## Mwongozo kwa Mshauri

Toleo la Kimataifa, 2019

Tim Green

Kwanza kilichapishwa huko Uingereza mwaka 2014.

Toleo hili la Kiafrika pia hupatikana bure kwa kupakua kutoka katika tovuti come-follow-me.org

© Haki miliki na Tim Green 2019. Haki zote zimehifadhiwa.
Hata hivyo, mwongozo huu kwa Mshauri unaweza kuchapishwa na kurudufishwa bure kwa ajili ya matumizi binafsi.

***Ombi kwa wasomaji***

This is a second edition of Come Follow Me Advisor's Guide, which has improved on the first with the help of many people's comments and recommendations. If you have any suggestions or comments, kindly send your suggestions using the feedback form at the end of this book.

This course depends a lot on case studies, testimonies, real-life stories, poetry and pictures from the Muslim world. Please help us prepare future courses by sending any examples you have like this that are relevant to believers from Muslim background, whether in Muslim majority countries or in the West. Please also suggest web resources, including video clips, to supplement the study book.

*Kwa nyongeza katika kozi hii ya Njoo Nifuate, sasa kuna maelezo mengi yanayopatikana kwa ajili ya uanafunzi wa Waamini wa Mazingira ya Kiislamu (WMK), ikiwemo tovuti ya www.bmbtraining.org. Sehemu B ya mwongozo kwa Mshauri inaweza kupakuliwa bure somo mojamoja kutoka katika tovuti ya come-follow-me.org.*

**Asanteni sana.** **Tim Green** **come-follow-me.org**

Toleo la Kiswahili

Labda ielezwe vinginevyo, Maandiko yote yametolewa katika The Holy Bible in Kiswahili, Unioni Version, Published as BIBLIA. © Bible Society of Tanzania, 1997

Toleo la Kiingereza

Maandiko yote yamenukuliwa kutoka the Holy Bible, New International Version®,
NIV®. Copyright ©1973, 1978, 1984, 2011 by Biblica, Inc.™ Imetumika kwa ruhusa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa ulimwenguni kote www.zondervan.com . Toleo la "NIV" na "New International Version" ni alama za kibiashara ambazo zimesajiriwa huko Marekani katika ofisi ya Biblica, Inc.™

Nukuu za zenye alama ya NLT zimetolewa katika the Holy Bible, New Living Translation, copyright © 1996, 2004, 2007 na Tyndale House Foundation. Zimetumika kwa ruhusa ya Tyndale House Publishers, Inc., Carol Stream, Illinois 60188. Haki zote zimehifadhiwa.

Ikoni zimetumika kwa kibali kutoka tovuti ya http://onelinewebfonts.com/icon kupewa leseni na CC KWA 3.0.
Ikoni za Biblia zilizotengenezwa na Freepik kutoka tovuti ya www.flaticon.com.

Jalada limebuniwa na David Vosburg. www.zagmediaarts.com

# Shukrani

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wote walionisaidia katika mradi huu kwa kunitia moyo, ukosoaji na maombi. Watu wengi sana walisaidia katika kuandaa kitabu hiki cha kujisomea cha Njoo Nifuate na wote wapokee shukrani hizo; baadhi yao (ni kama vile Sue na Rachel) walitoa mchango wao mkubwa wa mawazo kwa ajili ya Mwongozo kwa Mshauri, kama walivyofanya Scott na Malcolm.

Yakobo yeye alichangia mawazo mengi sana ya kibunifu, hasa kuhusu ‘dokezo za kitamaduni’ ili kuelezea mtazamo wa Waislamu na tamaduni na kulipangilia toleo la kwanza. Kwa toleo la pili, Penny alianza mchakato wa kuyapokea masomo ya mwongozo, na Jen alifanya kazi nzuri sana ya kuiendeleza kazi hii kwa hatua nyingine, akichangia mawazo mapya mengi na kupakia kwa ajili ya uchapishaji.

Naishukuru familia yangu hasa Rachel mke wangu. Kwa pamoja kwa muda wa miaka kadhaa tumeshiriki furaha na mioyo yetu kuguswa sana kwa ajili ya wale waliompa Yesu maisha na kutoka kwenye Uislamu; wanachukua njia ndefu na wakati mwingine ni njia ya kipweke katika kumfuata Yesu. Kwa neema tu Rachel amejitahidi kuikamilisha kazi hii kwa tarehe nilizoziweka (kazi ambayo niliianza muda kitambo takribani mwongo mmoja uliopita!) ametoa msaada wa kipekee sana katika kuipitia tena na kuihakiki kwa kuisoma.

‘Asanteni sana’ nyote.

# Tafadhali Soma Hapa Kwanza

Kozi ya *Njoo Nifuate* ni kozi ya watu wenye mazingira ya Kiislamu ambao wameanza kumfuata Yesu Kristo. Inalenga kuwasaidia kukua na kuimarika katika yeye na katika jumuia yake.

Kozi ya *Njoo Nifuate* ina vipengele vitatu:

1. Kitabu cha kozi kwa ajili ya mwanafunzi, kwa ajili ya kujisomea nyumbani akijiandaa na majadiliano;
2. Mwongozo kwa mshauri, ili kukusaidia kuongoza vipindi vya majadiliano;
3. Wewe, mshauri! Vitabu havifanyi wanafunzi. Wanafunzi hufanya wanafunzi.

Chini ya mkono wa Mungu, unaweza kuwa na ushawishi katika maisha ya waamini wapya: kama mshauri wao, kiongozi, mfariji, kielelezo, mwombezi na rafiki. *Njoo Nifuate* ni zana tu ya kutumia katika muktadha wa mahusiano ya kufanya wanafunzi. Mwongozo huu kwa Mshauri utakusaidia kutumia zana hiyo kwa manufaa, iwe kwa muumini binafsi au kwa kikundi.

Mwongozo kwa Mshauri una sehemu mbili. ***Katika Sehemu A, tafadhali wekeza dakika tano za kusoma 'Jinsi ya kusoma kozi hii'***. Hii ni muhimu kwa sababu njia ya kujisomea na muktadha vinaweza kuwa vipya kwako. Baadaye, soma sehemu zingine za Sehemu A kulingana na hitaji lako. Sura ya **'Dokezo za Kitamaduni'** imesheheni mwongozo muhimu kwa wale ambao hawana ufahamu wa kutosha kuhusu tamaduni za Kiislamu. Tunashauri kwamba usome dokezo hizi kila wiki, maana zimegawanyika kulingana na somo.

***Sehemu B hutoa miongozo hatua kwa hatua kwa kila somo***. Zinajumuisha maswali ya kujadiliana na miongozo yenye maelezo ya kina, ili kuwashauri aina mbili za washauri Wakristo: wale ambao hawaujui vizuri Uislamu, na wale ambao si wajuzi wa kutunga maswali ya majadiliano. Kama wewe tayari una uzoefu wa vipengele vyote hivyo viwili, unaweza usiwe na hitaji la miongozo hiyo yenye maelezo ya kina. Lakini bado utayatumia kama mwanzo wa kuandaa maswali yako mwenyewe ya majadiliano.

Katika hali yo yote, tafadhali hakikisha kwamba ukiwa pamoja na wanafunzi mnajadili maswali ya kitabu cha kozi hii ambayo yametiwa alama ya 'kwa ajili ya majadiliano' au 'mwitikio binafsi'.

Maarifa ya kichwa peke yake hayatoshi, na kozi hii itasaidia waamini kutoka katika mazingira ya Kiislamu (WMK) kuweza kubadilika kwa ngazi tatu:

- 'kichwa', kuwa na mtazamo uliobadilishwa kulingana na Neno la Mungu;
- 'moyo', kugusa maeneo yenye mihemuko, motisha na nia;
- 'moyo', kugusa maeneo yenye mihemuko, motisha na nia.

Mwongozo kwa Mshauri huu unaweza kupakuliwa, kuchapisha au kuzalishwa bure kwa ajili ya matumizi binafsi kutoka katika tovuri ya [come-follow-me.org](http://come-follow-me.org).

**Asante!** **Tim Green** **comefollowmecourse@gmail.com**

# Yaliyomo

## Sehemu A: Miongozi ya Kijumla


| Mada | Ukrasa |
|---|---|
| Jinsi ya kutumia kozi hii | 2 |
| Jukumu lako kama Mshauri | 4 |
| Jinsi ya kuongoza kila Somo | 5 |
| Kuongoza Kikundi cha Majadiliano | 9 |
| Kufuasa Waamini wa Mazingira ya Kiislamu | 10 |
| Maneno ya Kiislamu na Mambo ya Kitamaduni | 12 |
| Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara | 12 |
| Kuomba Mrejesho | 13 |
| Dokezo za Kitamaduni | 14-26 |


## Sehemu B: Miongozo ya Somo


| Somo | | Ukrasa |
|---|---|---|
| | Kikao cha Utangulizi | 28 |
| 1 | Kufanyika Mfuasi wa Kristo | 30 |
| 2 | Maisha Mapya Ndani ya Kristo | 32 |
| 3 | Mungu Baba | 34 |
| 4 | Kumtii Kristo kwa Nguvu ya Roho wake | 36 |
| 5 | Kuzungumza na Mungu | 38 |
| 6 | Neno la Mungu Kwetu | 40 |
| 7 | Washirika wa Kanisa la Kristo | 42 |
| 8 | Washirika wa Jumuia Mbili | 44 |
| 9 | Sabatu za Mateso | 46 |
| 10 | Mwitikio kwa Mateso | 48 |
| 11 | Waume na Wake | 50 |
| 12 | Kutatua Mabishano yetu | 52 |
| 13 | Kutoa Ushuhuda | 54 |
| 14 | Ubatizo | 56 |
| 15 | Njia Iliyonyooka | 58 |
| 16 | Sheria ya Pendo | 60 |
| 17 | Kufunga na Utoaji | 62 |
| 18 | Hatima na Uchawi | 64 |
| 19 | Kutumikiana Kila Mmoja na Mwenzake | 66 |
| 20 | Safari Yetu ya Kwenda Mbinguni | 68 |
| Nyongeza: Mistari ya kukariri | | 70 |

# Sehemu A:
# Miongozo ya Kijumla

# Jinsi ya Kutumia Kozi Hii

*Tafadhalli soma kabisa sehemu hii. Itakusaidia kunufaika na kozi hii.*

## Kozi hii ni kwa ajili ya nani?

Ni kwa ajili ya *wafuasi wa Kristo kutoka katika mazingira ya Kiislamu*, au wale waliokaribu kuamua kumfuata Kristo. Huwasaidia kuchukua hatua ya kwanza katika uanafunzi. Waamini waliokomaa watafaidika pia, kwa sababu kozi huwasaidia kutafakuri mambo muhimu kwa tamaduni za Kiislamu na kuzijadili na watu wengine.

## What is the learning method?

Kozi hii haikamiliki kwa kujisomea tu binafsi. Itumike kwa njia ya mahusiano. Kozi hii kila wiki wanafunzi:

1. kwanza, watajisomea wenyewe *kwa njia ya kujisomea binafsi nyumbani*;
2. pili, atazungumza na wewe (na wengine kama inawezekana) katika majadiliano, kwa kawaida ni mara moja kwa wiki;
3. tatu, *wataweka mafundisho haya katika vitendo* katika muktadha wa maisha yao ya kila siku.

Kwa maelezo zaidi:

- Hatua ya *'kujisomea nyumbani'* inahusisha mazingira yaliyo hai ya kujisomea na siyo kusoma tu kilichoandikwa. Inawataka wanafunzi wafanye kitu fulani baada ya kila sehemu fulani ya mafundisho:
    - Baadhi ya maswali huwasaidia wanafunzi *kukumbuka* kile walichokwishakisoma;
    - Baadhi ya maswali huwasaidia *kufahamu* na *kukazia maishani* mafundisho hayo;
    - Baadhi ya maswali huwasaidia *kuakisi* nia zao na kuzungumza na Mungu kuhusu nia hizo;
    - Baadhi ya maswali huwasaidia kuwa tayari *kushirikisha* uzoefu wao katika kipindi cha majadiliano;
    - Pia zile picha na mifano huwasaidia wanafunzi *kuunganisha* Neno la Mungu na uzoefu wa maisha yao.

- Hatua ya *majadiliano* huyafanya maelezo haya yawe hai na yenye kufaa. Wanafunzi hutoa maoni yao wenyewe na kuwasikiliza maoni ya wenzao. Hii huondoa au kukatisha nia za kizamani na kuleta motisha mpya.

- Hatua ya *'Tekeleza Jukumu'* huwapa wanafunzi kitu fulani cha kufanya kabla ya kikao kijacho. Inaondoa hali ya kulifanya somo liwe la kinadharia tu bali hulifanya somo liwe sehemu ya maisha yao.

## Je! Hutumika kwa watu binafsi au na kwa vikundi?

Kozi hii inaweza kutumika kwa njia yo yote ile, na kuna faida na hasara kwa kila moja. Utaongozwa na matukio kulingana na nani aliyepo ili kujisomea kozi hii. Kama inawezekana kuunda kikundi kidogo cha WMK, hii huboresha mahusiano yao na kuwapa fursa ya uzoefu zaidi wa kuongoza majadiliano. Kushauri mtu mmoja ni muhimu pia. Lakini 1:1 majadiliano yanweza kuwa ya mwelekeo mmoja tu, unapouliza maswali wanatoa majibu tu; jaribu kuweka mazingira ya ushirikishaji, ambapo wote mnajifunza kutoka katika Neno la Mungu na kutoka kwa kila mmoja.

Katika Mwongozo kwa Mshauri mara kwa mara neno 'mwanafunzi', tunamaanisha mtu mmoja au zaidi. Pia, badala ya neno 'yake au chake' tunatumia 'yao au vyao' ili kujumuisha wote, mwanamume na mwanamke. Maswali yote ya mjadala yanaweza kutumiwa katika vikundi au mtu binafsi, ingawa baadh iya shughuli za kujifunza zinahitaji kufanyika katika kikundi.

## Lazima masomo yote ishirini yamalizike mara moja?

Siyo lazima. Wiki ishirini bila mapumziko ni kozi ya muda mrefu sana! Hivyo uwe huru kuifanya kozi hii katika nusu mbili kukiwa na kipindi cha mapumziko hapo katikati au chagua masomo yale tu ambayo unaona ni muhimu kwa wanafunzi wako.

## Kipindi cha Majadiliano kina muundo na muda gani?

Hakuna muda wala muundo maalumu. VInaweza kutofautiana kadiri inavyowezekana, lakini kipindi cha majadiliano kinaweza kudumu angalau kwa muda wa saa 1½ (kikiwemo kipindi cha viburudisho) na itajumuisha:

- Viburudisho na mazungumzo (mwanzoni au mwisho)
- Maombi ya kufungua kipindi
- Marudio ya Tekeleza Jukumu la wiki iliyopita
- Marudio ya kujisomea nyumbani
- Majadiliano ya maswali yaliyochaguliwa kutoka katika somo husika
- Majadiliano ya kifungu cha Biblia
- Wakati mwingine, onyesho la video au shughuli ya pamoja
- Mazoezi ya kukariri mstari wa Biblia
- Kuahirisha kwa maombi, ukijumuisha mahitaji binafsi

Katika kipindi cha majadiliano, usipitie tu maelezo yaliyomo kwenye kitabu cha kujisomea. Hii huchosha. Hata hivyo, wanafunzi lazima wawe wamepitia somo hilo kabla ya kuja kwenye kipindi cha majadiliano, kwa hiyo unapaswa upitie yote kwa pamoja. Wala usiongeze mambo mengi mapya katika muundo wa mahubiri. Badala yake, jikite kwenye hoja za kivitendo katika majadiliano ambazo husaidi kuleta mabadiliko maishani mwa mwanafunzi.

## Je! Kozi hii inaendana na Biblia?

Ndiyo, ten asana. Ina mzizi wake kutokana na ushawishi kwamba Biblia ni Neno la Mungu na sisi ambao ni wafuasi wa Kristo (wote, wanafunzi na washauri) tunapaswa kufahamu na kutii. Kozi ya *Njoo Nifuate* imejengwa katika 1 Petro, kitabu ambacho kwa asili kiliandikwa ili kuwaongoza Wakristo katika muktadha wa misukosuko.

Uti wa mgongo wa kozi hii ni kujisomea kwa kuchunguza 1 Petro, imechukuliwa kwa mpangilio kuanza na sura ya kwanza hadi ile ya mwisho (ingawa siyo kupitia aya zote). Kutokana na uti wa mgongo huu, kama mbavu, kuna mada ishirini muhimu zinazoendana na **W**aamini wa **M**azingira ya **K**iislamu (WMK). Mbavu hizi zinatuunganisha na mafundisho muhimu kutoka katika sehemu zingine za Biblia.

Kila somo lina mstari au aya ya kukariri ili kutoa muhtasari wa dhamira yake. Mistari hii hutolewa kutoka katika 1 Petro na vitabu vingine, na zimekusanywa kwa ajili yako katika sehemu ya Nyongeza ya Mwongozo kwa Mshauri. Kusaidia ukaririaji wa aya, aya fupifupi zimechaguliwa, au sehemu fupi ya aya ndefu.

## Kwa nini kitabu cha kujisomea kinaonekana kuwa ni rahisi?

Kwa asili kiliandikwa katika muktadha wa watu wachache ambao hawakubahatika kupata elimu ya juu. Kwa hiyo, hutumia maneno rahisi kusoma, kukiwa na mifano halisi na picha zake. Hii haimaanishi kwamba mawazo yake ni rahisi. Kujisomea binafsi kwa masomo haya hutoa kiunganishi cha kipindi cha majadiliano ikipelekea tafakuri ya kina, mtazamo uliobadilika na uanafunzi wa kivitendo. Mifano halisi huwezesha majadiliano na mikazo kuwa rahisi kuliko kama yangekuwa mafundisho dhahania. Yasiyotekelezeka kivitendo. Pia mtu aliyefuaswa kwa njia ya kozi hii anayo zana rahisi ya kuwafuasa wengine. Hii huwezesha ufuasaji kuwa wenye manufaa zaidi.

### Kwa nini Mwongozo kwa Mshauri una maelezo ya kina?

Umeandikwa kusaidia washauri wengi. Baadhi yao wanahitaji msaada zaidi katika kuandaa maswali ya majadiliano, baadhi yao wanahitaji miongozo ya kitamaduni. Pia tumependekeza maswali ya majadiliano. Washauri wenye uzoefu hawatahitaji hili, lakini yote yamejumuishwa hapa ili kwamba unaweza kuchagua kile kinachokufaa wewe.

Kama kuna maswali mengi sana ya kujibu katika kipindi cha kila wiki cha majadiliano, basi chagua tu yale ambayo yanafaa kwa wanafunzi wako. Tafadhali jaribu kuchagua yale tu yenye alama ya 'kwa ajili ya majadiliano' au 'mwitikio binafsi' katika somo lilimo kwenye kitabu cha kujisomea.

### Je! Kila mwanafunzi anahitaji kuwa na nakala yake mwenyewe ya kitabu cha kujisomea?

Ndiyo, na ndivyo ilivyo kwa mshauri. Unaweza kuzipata kupitia tovuti yetu: come-follow-me.org

# Jukumu Lako Kama Mshauri

### Kitabu ni mwalimu



Kitabu chenyewe kinatoa mafundisho kwa njia rahisi. Huuliza maswali rahisi na pia hutoa majibu mwishoni mwa kila somo. Picha ya 'mwalimu' huwakumbusha wanafunzi juu ya hoja muhimu au mawazo makuu. Hii hulifanya jukumu lako kuwa rahisi, maana huhitaji kuandika somo lako mwenyewe. Usitumie kipindi cha majadiliano kutoa mahubiri, bali wasaidie wanafunzi kuchunguza na kutumia mafundisho ambayo tayari yametolewa kwenye kitabu.

### Wewe ni mshauri na rafiki

Wanafunzi wanakutazama kama mshauri wao. Wewe ni kielelezo chao, mshauri na rafiki. Wat learners look tokuchunguza kwa makini. Kielelezo chako ni muhimu zaidi kuliko maarifa yako. Kama muumini mmoja wa Afuganistani alivyosema, *"nilipoomba kujisomea Biblia ... nilikuwa ninamsoma mtu aliyenifuasa mimi".*

Kumbuka kwamba wanafunzi ni watu wazima, siyo watoto. Wana uzoefu mwingi wa maisha ambao wanaweza kuchangia kwenye kikundi. Kwa hiyo, kipindi cha majadiliano, waulize maswali mengi. Waulize kuhusu maoni na uzoefu wao. Wasaidie wawaze kwa ajili yao. Hakikisha wanaifanya sehemu ya 'Tekeleza Jukumu' kwa kila wiki. Uwe kielelezo chema kwao. Wajali. Waombee. Shiriki katika furaha na huzuni zao. Kunapojitokeza majanga, wasaidie waweze kukabiliana nayo kwa nia njema.

Kutana na rafiki yako kwa muda wa kawaida nje na vikao vya kila wiki. Wakaribishe kwenye chakula, au mtoke nje mkafanye kitu cha burudani kwa pamoja. Fanyeni mambo ya kawaida kwa pamoja. Fanyeni mambo ya kawaida kwa pamoja. Utashangaa kuona namna wanavyofaulu kwa kutazama matendo yao na mwitikio wako, namna unavyoshughulika na misukosuko, unavyowasamehe wengine, mazoea yako, maisha ya familia yako.

### Wanafunzi Hufanya Wanafunzi

Kitabu cha kujisomea hakiwezi kufanya wanafunzi. Ni wanafunzi tu wanaofanya wanafunzi. Mtu Fulani alikusaidia kukua kama mwanafunzi wa Kristo. Sasa ni zamu yako kumsaidia mtu mwingine akue. Siku hizi kuna Waislamu wengi wanamgeukia Kristo kuliko kipindi kingine cho chote katika historia. Lakini uinjilisti bila uanafunzi huleta matunda yenye ukomo. Mungu akutumie kama mtenda kazi mwenza, kuona matunda yakiongozeka katika maisha na familia za watu wapendwa wake kutoka katika Uislamu na kumfuata Yesu Kristo.

# Jinsi ya kuongoza kila Somo

## Kabla ya kila kikao

1. Angalau siku mbili kabla ya kukutana pamoja, andaa somo wewe mwenyewe, kana kwamba wewe ni mwanafunzi. Andika majibu yako mwenyewe kwa maswali yote. Usichukue njia za mkato.

2. Soma 'malengo' ya somo. Malengo yaliyopendekezwa yamo ndani ya kisanduku cha juu upande wa kushoto, mwanzoni mwa somo katika miongozo ya kila wiki. Kwa mfano, haya hapa ni malengo ya somo la 9:

| Somo la 9: Sababu za Kuteswa | |
|---|---|
| **Malengo kwa ajili ya kila mwanafunzi:**<br>a. Hakikisha kwamba hakuna kitakachotutenga na upendo wa Mungu.<br>b. Fahamu kwamba mateso hayana budi kuja lakini Mungu huyatumia kwa ajili ya mema kwetu.<br>c. Jifunze kutenda kwa busara ili kuepuka mateso yasiyo ya lazima.<br>d. Kariri 1 Petro 2:21. | **Dokezo za kitamaduni:**<br>• Kuwashauri WMK walio katika mateso<br><br>**Andaa:** vipange vi karatasi vyenye maneno kutoka Warumi 8:36 (kwa ajili ya swali la 12) |

Malengo haya yana kitu kwa ajili ya washirika wote kufanya wiki hii:

- 'kuwa na hakika' ni *nia*.
- 'kufahamu' ni kipengele cha *maarifa*;
- 'jifunze kutenda kwa busara' ni *stadi* ya kutekeleza kwa vitendo;
- 'kariri' ni njia nzuri ya kuleta Neno la Mungu ndani ya mioyo na maisha yao.

3. Kifuatacho, soma Miongozo ya somo hili. Tumekupa miongozo kwa kina ili kukusaidia hatua kwa hatua. Chagua maswali yale ya majadiliano ambayo yanaendana na wanafunzi wako. Baadaye, kadiri unavyopata uzoefu, jisikie huru kuandika maswali yako mwenyewe ya majadiliano kulingana na mahitaji ya washirika wako na malengo ya somo.

4. Soma 'Dokezo za Kitamaduni' kwa ajili ya somo, hasa kama siyo mzoefu na tamaduni za Kiislamu.

5. Andaa vifaa vilivyotajwa ndani ya kisanduku, kama una mpango wa kuifanya hiyo shughuli ya kujifunzia.

6. Hatimaye, ombea kila mmoja ndani ya kikundi. Mwombe Mungu akusaidie kuwa mshauri mzuri.

## Kila Mkutanikapo

1. Wakaribishe watu kadiri wanavyofika. Wapatie viburudisho kama unapenda.

2. Fuata hatua chini ya kipengele cha 'Ufunguzi' ili kuanza kikao.  Mfano kwa ajili ya somo la 9:

| Ufunguzi |
|---|
| **Omba kwa ajili ya somo. Rudia sehemu ya 'Tekeleza Jukumu' ya wiki iliyopita:** Ulifanya nini ili kuihudumia jumuiya yetu au mtu mhitaji au mtu aliyeko kwenye madaraka? Mtu huyo alionesha mwitikio gani? |
| **Somo la 9: marudio ya kujisomea nyumbani:**<br>**Swali la 1:** kwa ajili yako, kukuachia mfano, kwamba wewe ufuate hatua zake (1 Petro 2:21).<br>**# 2:** 1) ulimwengu, utawachukia; 2) Mungu, mateso; 3) kutenda pasipo busara; 4) hatua za Kristo |
| **Tambulisha mada ya leo:** Mada ya leo ni mateso, ni somo gumu sana. Yawezekana majadiliano yetu yanaweza kuleta machozi kwa sababu ya maumivu tuliyokwisha kuyapitia. Lakini Mungu hutumia mateso kwa ajili ya wema, na anaweza kuponya maumivu yetu kadiri tunavyoyazungumzia mambo haya. |

Ni muhimu 'kurudia sehemu ya Tekeleza Jukumu ya wiki iliyopita'.  Hii humwonesha mwanafunzi kwamba kozi hii siyo tu inahusu kujifunza kweli bali na kuziweka katika vitendo. Pia, hukuonesha namna wanavyoendelea katika uanafunzi na pale wanapokutana na changamoto. Waombe wanafunzi watoe taarifa ya namna wanavyoitekeleza sehemu hii ya Tekela Jukumu, lakini usianzeshe majadiliano kuhusu mada ya wiki iliyopita maana unahitaji kusonga mbele kwa mada ya somo jipya.
Kusudi la 'marudio ya kujisomea nyumbani' ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wamejisomea nyumbani na wanaweza kukumbuka hoja muhimu za mafundisho. Kama unaifanya kozi hii kizamani, waombe wanafunzi wako wafunike vitabu vyao na wajibu maswali kwa mdomo. Kama unaifanya kisasa zaidi na kwa kupata alama, basi andaa nakala za Marudio ya Somo kama majaribio ya kila mwanafunzi kuweza kujibu kwa kuandika huku vitabu vyao vikiwa vimefunikwa. Majaribio yao yanaweza kusahihishwa na kupewa alama (kazi hiyo unaifanya wewe baada ya kipindi), au wakati wa kipindi kikiendelea kila mmoja anasahihisha karatasi ya mtu mwingine).

3. Kisha ongoza majadiliano, ukitumia maswali ya majadiliano uliyochagua hapo awali. Kama muda hautatosha, basi hakikisha unashughulika na maswali yenye alama ya 'kwa ajili ya majadiliano' au 'mwitikio binafsi' yaliyomo ndani ya kitabu cha kujisomea. Katika matoleo ya hapo baadaye ya kitabu cha kujisomea, maswali haya yana alama ya ikoni (kulia). Kama huna uzoefu wa njia za kuongoza kikundi cha majadiliano, soma miongozo 'Kuongoza Kikundi cha Majadiliano' katika ukrasa wa 8. Maswali yanayohitaji uchunguzi wa kibiblia yana alama ya ikoni ya Biblia, k.v.

| Soma 1 Petro 1:3-7 |
|---|
| • Kutokana na mstari wa 4, urithi wetu uko wapi?*Huko mbinguni*<br>• Je! 'Utatoweka, kuharibika au kupotea'? *Hapana – tofauti na urithi wetu wa kidunia!*<br>• Kulingana na aya ya 5, ni nini kinachotukinga kwa wakati huu?*Nguvu ya Mungu* |

4. Wewe kama mshauri usizungumze sana kipindi kikiendelea. Badala yake, wanafunzi ndio wazungumze zaidi. Kwa hiyo, kila inapofikia sehemu ya kusoma paragrafu kutoka katika kitabu cha kujisomea au kifungu cha Biblia, ni vizuri mwanafunzi asome kwa sauti, siyo wewe.

5. Baadhi ya majibu kwa maswali ya majadiliano yametolewa kwa italiki, kama ulivyo mfano hapo juu. Tafadhali jaribu kuwatia moyo wanafunzi wako kuweza kujibu maswali, kwa mfano, kwa kurudia swali au wazo kwa aya sahihi, kabla hujatoa jibu wewe mwenyewe, kama hakuna aliyeweza kujibu. Italiki hizi pia hutoa dokezo za kitamaduni na kumbukumbu kwako kukusaidia wakati wote wa somo kama vile:

| |
|---|
| **Swali la 17:** Soma paragrafu ya pili.<br>• Nini maoni yako kuhusu swali hili? *Jibu 'sahihi' au 'siyo sahihi' hutegemeana na mazingira. Mtu aliye katika hatari ya maisha yake na anataka kuhamia sehemu nyingine kwa kipindi fulani. Hata hivyo, kama hawamo hatarini basi wajitahidi kukaa nyumbani kwa utulivu mpaka hali itakapotulia. Lazima wajaribu kuonesha kwamba bado wana uaminifu kwa familia zao hata kama wanamfuata Yesu Kristo.* |

6. Katika baadhi ya masomo, tumejumuisha mapendekezo kwa ajili ya masomo yenye shughuli za kufanya, au kuonesha video kwa kifupi. Mapendekezo haya yana alama ya ikoni ya mpira (kushoto). Ambapo maandalizi hutakiwa kwa ajili ya shughuli hizi, hii itazingatiwa katika sehemu ya 'jiandae' ya kisanduku chenye kichwa cha somo. Kama utapanda vipande vingine vizuri vya video au shughuli za kujifunzia zinazoendana na masomo, tafadhali tujulishe.

Vipindi vingi vya majadiliano vitatoa nafasi ya kurudia mstari wa kukariri wa wiki. Katika matoleo ya hapo baadaye ya Kitabu cha Kujisomea, mstari wa kukariri una alama ya ikoni (kulia). Kwa kurahisisha marejeo, kuna jedwali la mistari ya kukariri katika ukrasa wa 70 wa kitabu hiki.
Ili kuwasaidia wanafunzi wako kukariri kila mstari wa kukariri kwa kila wiki, unaweza kumrekodi mtu Fulani anausoma na kuutuma kwenye kikundi ili wasikilize kwa wiki hiyo. Hii itawasaidia sana ambao wamezoea kujifunza kwa kupokea kila kitu kwa mdomo.

7. Mwishoni, fuata hatua zilizomo kwenye kisanduku ili kuahirisha kikao. Kwa mfano, hiki hapa ni kisanduku mwishoni mwa somo la 9:

| ***Mwisho*** | |
|---|---|
| **Kutii mafundisho ya leo:**<br>• Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?<br>• **Someni kwa pamoja sehemu ya Tekeleza Jukumu.** Wanafunzi wanaweza kutumia mchakato ule ule kwa tafakuri ya leo ili kutafakari aya moja kila siku. | **Ombeni pamoja:** Waombe watu waombe sala fupi fupi, wakimshukuru Mungu kwa ahadi zake imara wakati wa mateso. Ombeeni waamini walio katika mateso katika nchi zingine, hasa wafuasi wa Kristo wa mazingira ya Kiislamu. |

## Baada ya kikao

1. Kama kikundi chako kina alama za majaribio au mahudhurio, ziandike. Pia ni vizuri kutoa alama kwa ajili ya a) ukamilishaji wa kazi za nyumbani (hasa maswali ya majadiliano yaliyotiwa alama, b) uchangiaji wakati wa majadiliano na c) kuifanya sehemu ya Tekeleza Jukumu. Katika baadhi ya hali, hii huwasaidia wanafunzi kushiriki kwa makini katika kozi, na kunufaika zaidi. Katika hali zingine, ni vizuri kuendelea tu katika hali ya kawaida.

2. Ona kama umeongoza majadiliano vizuri. Jiulize mwenyewe maswali haya manne:

- *"Je! Nilizungumza sana?"*
- *"Je! Washirika wote walihusika katika majadiliano wakiwemo wale wakimya na wenye aibu?"*
- *"Je! Maswali yangu yalikuwa yanaeleweka na mazuri kwa ajili ya majadiliano?"*
- *"Je! Somo limefikia malengo yake na je, linatekelezeka kivitendo katika maisha yetu?"*

Jifunze kutokana na uzoefu na jaribu kuboresha udhaifu wo wote kwa wiki ijayo.

3. Endelea kuwaombea wanafunzi kwa wiki nzima.

# Kuongoza Kikundi cha Majadiliano

*Kama huna uzoefu wa kutosha, basi hii hapa miongozo yake.*

- Usizungumze sana wewe! Unapaswa kuuliza maswali tu, siyo kuhutubia. Watu wazima hujifunza zaidi kwa njia hii na huifurahia zaidi. Maswali mazuri lazima:

  - yawe rahisi kueleweka

  - yaendane na somo

  - yafungue mjadala (na siyo kuufunga kwa jibu la neno moja kama vile 'ndiyo' au 'hapana')

- Toa fursa kwa kila mshirika ashiriki katika majadiliano. Waombe wale wenye uwezo wa kuzungumza sana wasizungumze sana. Wasaidie wale wenye haya kwa kuwauliza maswali rahisi (na usiruhusu mtu ajibu kwa niaba yao.)

- Kama wanakikundi hawatalielewa swali, usitoe jibu wewe, bali uliza swali hilo kwa njia tofauti.

- Usiruhusu mjadala ukahama kwenye wazo kuu.

- Kama mshirika atatoa jibu ambalo 'siyo sahihi' au halisaidii katika majadiliano, usiwaaibishe kwa kusema 'si sawa'. Badala yake, uliza wale wengine wanafikiri nini. Mara nyingi watatoa jibu zuri zaidi. Au unaweza kusema, 'asante kwa mchango wako, tunashukuru, je! Umezingatia kipengele hiki pia?'

- Jikite kwenye sehemu ya Tekeleza Jukumu ya kila somo, ili kwamba kila mshirika wa kikundi anaondoka na kitu cha kutumia katika maisha yake.

- Ruhusu washirika wakuulize maswali. Kama hujui majibu yake, waambie utatafuta majibu kabla ya kikao kijacho. Watakuheshimu zaidi kwa hilo kuliko kujifanya kuwa unajua kila jibu. Hakikisha unatimiza ahadi hii kwa kuleta majibu yako kwenye kikao kijacho.

- Kama ni kipindi cha kusoma aya ya Biblia au sehemu kutoka kwenye kitabu cha kujisomea, mwombe mtu mmoja asome. Hii huwapa nafasi ya ushiriki zaidi. Ni njia nzuri ya kuwapata wale wenye haya kushiriki katika majadiliano.

- Kama unatumia lugha mbalimbali, unaweza kuomba mtu mmoja kutoka katika kila lugha hiyo kusoma kwa lugha yao, au unaweza kusoma mara moja katika Kiswahili na kisha kuwaruhusu wanafunzi kusoma katika lugha zao wenyewe.

# Kufuasa Waamini wa Mazingira ya Kiislamu

***Kama huna uzoefu sana wa kufuasa Wakristo wa mazingira ya Kiislamu, na hasa kama wewe unatoka nchi za magharibi, naomba usome kurasa hizi.***

Yesu Kristo ametuita kufanya wanafunzi kutoka katika tamaduni zote. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa kuwafanya wawe wa Wakristo wa kimagharibi. Kuna mambo mazuri na mabaya katika tamaduni zote. Sisi sote lazima tuliache neon la Mungu ling'are katika vipengele dhaifu vya kitamaduni, tuwe tunatoka Magharibi au Mashariki. Kwa mfano, je! ni Kibiblia zaidi kuvaa nguo za kimashariki au kimagharibi? Kula kwa mikono yetu au kutumia kisu na uma? Kuomba huku tumeshikana mikono kwa pamoja au viganja vyetu vikifunguka kuelekea juu? Kujali ubinafsi au kushirikishana?  Kujali familia zetu tu au pia kujali ndugu wengine katika ukoo? Kwa matendo yote hayo, Mungu hukaribisha utofauti wa kitamaduni, na katika baadhi yake kuna mambo mazuri tunaweza kujifunza  kutoka kwa waamini wa mazingira ya Kiislamu.

Hata hivyo, Neno la Mungu hutoa changamoto kwa vipengele vingine vya kitamaduni, pale vinapokuwa vimeathiriwa na dhambi ya mwanadamu. Uanafunzi hujumuisha kujifunza kuthamini na kuheshimu, kusamene wale wanaokuudhi, kuwa na nia njema kwa wale wa jinsia tofauti na wewe, kumweka Mungu kwanza katika maamuzi yetu yote, n.k. Mambo haya na mengine hujitokeza kutoka katika mazingira na tamaduni zilizochanganyikana. Unawezaje kuyapata mambo sahihi kwa ajili ya rafiki yako? Ni kwa kupata muda wa kukaa nao, kwa kuwasikiliza na kuwaombea. Kuwauliza maswali kuhusu namna walivyolelewa na maisha yao ya familia. Kumbuka kwamba watu wote wako tofauti. Hivyo tafuta kwa kuuliza.

Tamaduni nyingi za Kiislamu zina mambo yanayoendana. Lakini kumbuka kwamba hutofautiana pia. Wapakistani, Wairani na Waarabu hawafanani! Hapa pamoja na tamaduni hizo kuna utofauti kati ya vikundi fulani au madaraja ya kiuchumi. Hivyo mwulize rafiki yako alivyolelewa: wanapenda nini kuhusu utamaduni wao na nini ambacho hawakipendi. Wakati mwingine baada ya kumpokea Kristo huzikataa tamaduni zao za kale. Lakini kwa ustawi wao wa muda mrefu wa kisaikolojia ni vizuri kuunganisha baadhi ya vipengele vya utamaduni wa kale na ule mpya, badala ya kuvigandamiza vyote kwa pamoja.

Pia tafuta nini kinachowakabili 'waumini wa mazingira ya Kiislamu' (**WMK**). Baadhi ya mambo ambayo hukabiliana nayo mara baada ya kumfuata Kristo ni:

- Kuziacha nyumba, familia na tamaduni zao za awali. Hii inaweza kupelekea hali ya *upweke* usio na kifani ambayo ni hisia ya *kupoteza utambulisho wao*.
- *Mateso* makali kutoka kwa wanafamilia. Hii inaweza kupelekea kuwa na hisia za *kukataliwa*.
- *Aibu* wanayopewa na jumuia zao za awali.
- *UKosefu wa muundo* katika imani ya Kikristo, ikilinganishwa na Uislamu ambao huwapa watu waumini wa wazi wa kufuata.
- *Ukosefu wa jumuiya* katikati ya wafuasi wa Kristo ukilinganisha na kile walichokizoea.

**WMK** katika nchi za magharibi wanaweza wakapata matatizo madogo katika baadhi ya maeneo, pamoja na changamoto za nyongeza kutokana na hali zao. Kwa mfano, Mwislamu mhamiaji anapokuwa mfuasi wa Kristo huko Magharibi, lazima waendane na utambulisho wote wa aina mbili kwa wakati mmoja, mmoja unaotokana na uhamiaji na mwingine kutokana na uongofu wake.

Kwa sababu ya mambo haya, kozi ya *Njoo Nifuate* imejengwa katika kitabu cha 1 Petro, kukiwa na lengo maalumu ya maswali kuhusu utambulisho. Hufundisha kwama sisi 'watu wa miliki ya Mungu', wa thamani mbele zake na tumeunganisha kila mmoja na mwenzake katika Kristo.

Kufahamu simulizi za watu ni ufunguo kwa mafanikio ya kozi hii. Itakusaidia wewe kama mshauri kufahamu furaha nyingi na magumu mengi ambayo waliokuwa Waislamu wanayapitia katika kumfuata Yesu. Pia itakusaidia kufanya muunganiko kati ya maelezo ya kozi na maisha ya wanafunzi unaowafunza. Kwa

nyongeza, itakuruhusu kufahamu kwa nini maelezo haya yanajumuisha mada kama zilivyo kukiwa na msisitizo katika mada kama vile mateso, mada ambayo huwa haijitokezi katika kozi zingine za uanafunzi. Kipindi cha chakula/viburudisho kabala au baada ya majadiliano inaweza kujenga urafiki na hali ya kuaminika kwa wanafunzi wako ili kwamba waweze kukushirikisha habari za maisha yao.

Hatimaye, yote hii inahusu kujali. Upendo huwa na mguso mkubwa zaidi. Upendo hustili wingi wa mapugnufu ya kitamaduni! Upendo humaanisha kwamba upo kwa marafiki zako pale wanapokuwa katika hali ya kuchanganyikiwa au kuumizwa. Humaanisha kutoa ukarimu wakati wanapoikosa familia yao. Humaanisha kutunza mawasiliano nao kwa njia ya simu na ujumbe, na siyo katika njia tu ya kawaida ya barua pepe na vikao. **WMK** mmoja alisema, *"Niliacha familia yangu ili kumfuata Yesu, na katika vyote hivyo nilipata vikao tu!"*

Inatarajiwa kwamba maelezo zaidi na mafundisho yataendelea kupatikana ili kukusaidia kuwaimarisha Wakristo kuwajali na kuwafuasa waamini wa mazingira ya Kiislamu. Hii inaweza kufaa pia katika muktadha wan nchi za magharibi. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tuma barua pepe: comefollowmecourse@gmail.com.

# Maneno ya Kiislamu na Mambo ya Kitamaduni

## Ukomo wa Matumizi ya Maneno ya Kiislamu

Kwa mwanafunzi kuelewa mawazo mapya, inaweza kuwa ni msaada kuanza na daraja kutokana na mawazo yao ya zamani. Hii huwasaidia kulinganisha na kutofautisha ya kale na mapya. Pia huwasaidia kueleza ujumbe wa Kikristo kwa marafiki zao wa Kiislamu kwa njia ambayo huleta maana na bila kusikika kuwa ni kitu kigeni sana.

Kwa hiyo, kwa *ukomo* fulani kozi hii hutumia maneno machache ya Kiislamu kama mahali pa kuanzia, na kama daraja la kuwaondoa katika ulimwengu uliozoeleka kwao na kuwaingiza katika ulimwengu mpya wa mafundisho ya Kikristo. Kwa mfano, kama tukizungumzia *shariah* (sheria) za Kristo, huwasaidia wanafunzi kutafakari *shariah* zao za kale kama Waislamu na kutambua kwamba ile njia yao mpya ya kumtii Kristo kuwa ni Bwana ni tofauti.

## Faharasa ya Maneno

Maneno yafuatayo ya Kiarabu yametajwa katika kozi hii. Hapa tunayaandika kwa herufi za Kiswahili, bila kuweka alama maalumu za kitaalamu, na kwa maana zake za kawaida. Herufi na maana zake za ndani sana zinaweza kupatikana katika vitabu vyake husika. Utangulizi mzuri katika Uislamu kwa mtazamo wa Kikristo hujumuisha *Urafiki Kwanza* na Steve Bell, *Msalaba na Nusu Mduara* na Colin Chapman.

| | |
|---|---|
| *Dua* (sura 5) | maombi binafsi |
| *Hija* (sura 20) | kwenda kuhiji katika eneo takatifu, Makka |
| *Halal* (sura 15) | kinachokubalika |
| *Injili* (sura 1) | Injili |
| *Jini* (sura 18) | zina zoaminika ziliumbwa kutoka moto |
| *Kafiri* (sura 2) | mpingaji wa dini ya Kiislamu |
| *Kalima* (sura 1) | ‘neno’ pia hutumika kwenye *shahada* (ona hapo chini) |
| *Murtadi* (sura 2) | ni mkengeufu aliyekengeuka dini ya Kiislamu |
| *Paradiso* (sura 1, 9, 20) | peponi |
| *Kibla* (sura 20) | ni mwelekeo wa kijiografia wakati wa swala – kwa Waislamu, Makka |
| *Salat* (sura 5) | utaratibu wa swala hufanywa na Waislamu mara tano kila siku |
| *Saum* | mfungo unaofanyika kwa kujinyimja kula chakula katika mwezi wa Ramadhani |
| *Shahada* (sura 13, 20) | shuhuda. Hasa tamko la Kiislamu “Hakuna Mungu ila Alla, na Mohammed ni mtume wake” |
| *Sharia* (sura 17) | sheria za kidini na njia ya maisha |
| *Shirki* (sura 3) | sanamu, kukihusisha kitu cho chok na Mungu, ushirikina |
| *Suna* (sura 17) | Kuige mfano au mwenendo wa kuishi (kwa Waislamu, hasa mfano wa Mohammed) |
| *Taurat* (sura 4) | vitabu vya Musa, Pentatuku |
| *Umma* (sura 7,14) | neno la Kiarabu kumaanisha jumuia ya waamini wote ulimwenguni |
| *Zaburi* (sura 6) | Zaburi |
| *Zaka* (sura 17) | matoleo ya hisani ambayo ni lazima kwa Waislamu |

‘Nguzo tano’, zilizotajwa katika sura ya 20, ni misingi mitano katika matendo ya Kiislamu; *shahada, sala, mfungo, zaka* na *hija* (ona maana zake hapo juu).

## Mambo ya Kitamaduni ya Kiislamu

Masomo mengi katika kozi hii huandikwa kwa kuzingatia mambo ya kitamaduni. Haya yameelezwa kwenye maelezo kwa Mshauri katika kila somo. Hata hivyo, kumbuka kwamba siyo WMK wote wanashawishiwa na mambo haya kwa kiwango kile kile, hivyo lazima mikazo yako ya masomo iendane na aina ya wanafunzi ulio nao.

# Maswali Yaulizwayo Mara kwa Mara

## Kitabu cha Kujisomea hupatikana katika lugha gani?

Kozi hii kwa sasa imetafsiriwa katika lugha ya Kiingereza, Kijerumani, Kiarabu, Kidari, Kifarsi, Kibengali na Kirusi, pamoja na lugha zingine ikiwemo Kiamhariki, Kiurdu, Kipashtu na Kiswahili sasa zinaendelea kutafsiriwa. Tafadhali tembelea tovuti ya come-follow-me.org kuona maendeleo yake, na sehemu zingine za kuweza kununua lugha zilizopo.

## Ni kwa namna gani kitabu cha kujisomea kinaweza kupatikana katika nchi zingine?

Kwa kutumia tovuti ya come-follow-me.org, tafsiri nyingi zitapatikana kwa njia ya mtandao ulimwenguni kote. Baadhi ya watoaji wamechapisha katika maeneo yao, kwa mfano, Kijerumani, Kiarabu. Mpaka sasa taarifa za utoaji hupatikana kwenye tovuti.

## Je! Hupatikana kwenye mtandao au kwa kupakua?

Kitabu cha kujisomea hakijaandaliwa kama waraka wa kusomwa kwenye kioo cha kompyuta. Badala yake, ni kitabu cha kazi kwa mwanafunzi kuandika majibu yao, na kisha kuja nacho kwenye kipindi cha majadiliano pamoja na mshauri wanaweza kujadili mikazo maishani kwa vitendo. Mchakato huu ni hai na njia nzuri ya kuweza kujifunza kwa manufaa kuliko kule kukaa tu kusoma kilichoandikwa.

Kutokana na sababu hizo, hakuna mpango wa kuandaa kitabu cha kujisomea ili watu wakisome kwa njia ya mtandao. Labda toleo maalumu la kutumia kwenye tableti linaweza kufikiriwa baadaye. Hata hivyo, Mwongozo kwa Mshauri huu hupatikana bure kwa kupakua kutoka kwenye tovuti yetu.

## Je! Kozi hii inafaa kwa wale wanaojifunza kwa mdomo?

Kwa njia moja, njia ya kozi hii ni kwa mdomo, kwa sababu sehemu yake muhimu ni kipindi cha majadiliano. Pia wanafunzi ambao hawajapita shuleni wanaweza kukariri aya za Biblia, kujadili picha zilizomo ndani ya kitabu cha kujisomea, na kufanya sehemu ya Tekeleza Jukumu.

Hata hivyo, kipengele cha kujisomea nyumbani hakihitaji ustadi ya kujua kusoma na kuandika. Kwa mwanafunzi ye yote ambaye hawezi kusoma kwa urahisi au hawezi kabisa, fuata mwongozo huu:

- Kila mmoja wa watu hawa, tafuta mshirika mwingine katika kikundi ili kuwa msaidizi wake. Watakuwa wanalipitia somo mapema wakiwa pamoja, ili kuwasaidia wale wasiojua kusoma (au wale wanaosoma polepole) kufahamu fundisho kuu. Kisha wakati wa kikao watakaa pamoja, na kuwasaidia kupata mahali au picha sahihi ndani ya kitabu. Msaidizi anaweza kuwa mmoja wa familia, au mtu mwingine kabisa.

- Kumbuka kwamba watu wasiojua kusoma ndani ya kikundi wana uzoefu mwingi wa maisha kuliko wale wanaoweza kusoma. Maoni yao ni ya thamani sana. Hakikisha kwamba wanapata fursa sawa ya kuchangia katika majadiliano ili kwamba washirika wote wanufaike.

## Je! Kozi hii inawahusu Waislamu moja kwa moja?

*Kitabu cha Kujisomea* hakitaji Uislamu moja kwa moja. Kwa sehemu hii ni kwa ajili ya sababu za kiusalama, maana kwa asili kiliandikwa kwa ajili ya nchi zenye misimamo mikali ya Uislamu, ambapo cho chote kilichochapishwa ambacho kinadhaniwa hakiendani na Uislamu kinaweza kuwahatarisha (kwa nchi za Magharibi hili siyo tatizo). Pia kwa sababu lengo siyo Uislamu bali kwa kumfuata Yesu na mafundisho yake.

Hata hivyo, kozi inazungumzia mambo ambayo huibuka kwa wafuasi wa Kristo kutoka katika mazingira ya Kiislamu. Pia kuna ukomo wa matumizi wa maneno ya Kiisalmu kama daraja la kumvusha mwanafunzi kwenda kwenye maana mpya ya Kikristo, kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 'Maneno ya Kiislamu na Mambo ya Kitamaduni'.

*Mwongozo huu kwa Mshauri* unahusu Uislamu moja kwa moja, ili kuwaongoza washauri ambao wanaweza kupungukiwa ufahamu wa mazingira ya kitamaduni, na pia kwa sababu tunadhani kuwa hapatuwa na suala la kiusalama. Hata hivyo, kama inawezekana tungeweza kutoa toleo kwa ajili ya matumizi katika muktadha ambao itakuwa ni msaada bila kutaja Uislamu. Tafadhali wasiliana nami kama unadhani kuwa toleo hili linahitajika.

## Ombi la Mapendekezo

Tunapenda kuwashukuru watu wote ambao tayari wamekwisha kutoa mapendekezo yao ambayo ni muhimu sana wakati wakitumia kozi hii, mengi ya mapendekezo hayo yameingizwa kwenye toleo hili jipya la Mwongozo kwa Mshauri. Tunakaribisha mapendekezo zaidi na mawazo kwa ajili ya kuboresha matoleo yajayo. Tafadhali uwe huru kujibu swali lo lote linalotolewa hapo chini na ututumie kwa barua pepe.

1. Swali gani liboreshwe na ni kwa namna gani?
2. Ni 'dokezo za kitamaduni' zipi zinaweza kuboreshwa au kuongezwa?
3. Je! Kuna miongozo zaidi katika mada yo yote ambayo inaweza kuongezwa katika mwongozo huu?
4. Tafsiri ya Biblia iliyotumika katika kozi hii ni The Holy Bible, Union Version, published as Biblia Maandiko Matakatifu au itumike ile ya Kiswahili cha Kisasa (kwa ajili ya kizazi kipya)?
5. Ni video zipi au shughuli za kujifunzia unaweza kupendekeza kwa ajili ya masomo haya?
6. Ni mifano gani katika utamaduni wa Kiislamu, au visa vya wafuasi wa Kristo kutoka katika mazingira ya Kiislamu, ungependekeza kwa ajili ya kozi zijazo za aina hii?

***Tafadhali tuma mapendekezo kwa come-follow-me.org. Asante kwa msaada wako!***

Tim Green
comefollowmecourse@gmail.com
come-follow-me.org

# Dokezo za Kitamaduni

*Soma dokezo za kitamaduni kwa kila somo kadiri unavyojiandaa kwa wiki hiyo, hizi zimeandikwa hasa kwa wale ambao hawana ufahamu wa kutosha kuhusu utamaduni wa Kiislamu, na ni muhimu katika kutoa mazingira ya kitamaduni kwa kila somo la wiki.*

## *Somo la 1*

### Mahali pa kuanzia na WMK (Waamini wa Mazingira ya Kiislamu)

Mahali pa kuanzia kwa wiki hii ni mazungumzo kati ya Muislamu na mfuasi wa Kristo. Nia ya Muislmu huyu ni ya kienyeji, ingawa siyo kwamba Waislamu wote wako hivyo.

'Njoo Nifuate' imebuniwa kwa wale ambao tayari ni wafuasi wa Kristo, lakini somo la 1 huelezea hatua za kuifikia imani kwa sababu:

- Hii hukusaidia wewe, mshauri, kukagua ufahamu wa kiroho wa mwanafunzi.
- Ye yote ambaye hapo awali hajaomba kumpokea Kristo, ana fursa ya kufanya hivyo.
- Huwapa wanafunzi njia rahisi ya kuelezea hatua hizi kwa Mwislamu anayetafuta kumpa Yesu maisha yake.

Hatua za kiimani zilizoelezwa katika somo hili ni za kawaida kabisa, isipokuwa hatua ile ya mwisho kuhusu 'kujiunga na jumuia ya Kristo' ambayo haisisitizwi sana katika nchi za Magharibi wakati wa kuwasilisha Injili. Ni vigumu sana kwa waamini kutoka katika mazingira ya Kiislamu kuishi bila ushirika na watau wengine. Kwao, 'jumuiya ya Kristo' linaweza kuwa ni kanisa, au kikundi cha **WMK**, au hata kikundi kinachokutana kwa siri na waamini wengine, lakini aina yo yote ya ushirika ni muhimu sana. Tutasoma kwa kina kuhusu jambo hili katika Somo la 7.

### Waamini wapya na kuhesabu gharama

Ni jambo la wazi kutaja gharama kubwa kwa Mwislamu kumfuata Yesu. Hata hivyo, baadhi ya waamini kutoka mazingira ya Kiislamu hudhani kwamba ni jambo lisilofaa kusisitiza sana hili. Ingawa swali la 13 huelezea gharama, swali la 14 huweka wazi kwamba inastahili. Omba mwongozo wa Mungu kuhusu namna ya kuweka uwiano sawa wa kweli hizi kulingana na hali ya wanafunzi.

## *Somo la 2*

### Jihad

Watu wa Magharibi wakisikia neno hili 'Jihad', mara kwa mara huwaza msimamo mkali wa kidini katika vyombo vya habari. Lakini neno la Kiarabu jihadi maana yake ni 'kuhangaika'. Huhusika migogoro ya kijeshi, ambayo katika Uislamu huitwa kitaalamu kuwa ni 'jihad ndogo'. 'Jihad kubwa' ni mahangaiko ya mtu kujinyenyekesha kwa maadili yenye kiwango cha Allahh. Hufanana sana na wazo la 'vita vya kiroho' tunavyopigana dhidi ya dhambi. Inaweza kusaidia kuelezea kwa namna hiyo. Hata hivyo, uwe makini na wanafunzi. Kama neno jihad humaanisha msimamo mkali wa kidini kwao, basi usitumie mfano huo.

### Mwonekano wakati wa sala

Katika picha ya swali la 20, viganja vimegeuzwa kuelekea juu wakati was ala, na siyo kuunganishwa pamoja. Je! umeshawahi kujiuliza kwa nini Wakristo wao kwa kawaida huinamisha vichwa vyao, hufumba macho yao na kuunganisha mikono yao wakati wa maombi? Hakuna kibaya katika hayo yote, lakini Maandiko hayatulazimishi kufanya hivyo wakati was ala, na hutoa picha mbalimbali za mionekano wakati was ala. Mara kwa mara Waislamu huomba kwa Allahh huku viganjwa vyao vikiwa vimegeuzwa kuelekea juu, na wanafunzi wako watakuwa na uzoefu huo. Inaweza kuwa ni njia rahisi kuonesha picha ya namna tunavyokuja mbele za Mungu tukiwa mikono mitupu, tukiomba rehema zake. Kama unataka, mwulize mwanafunzi kama hapo awali alikuwa akiomba kwa namna hii na kama watapenda kuendelea kufanya hivyo huku wakiwa wafuasi wa Kristo.

# Somo la 3

## Kumwita Mungu 'Baba'

Kwa Waislamu, Allahh yuko juu sana na hashirikishi uungu wake na ye yote. Kwao, neno la Kiarabu *shirk* maana yake ni kuhusisha kiumbe cho chote na Mungu mwenyewe. Waislamu huamini kwamba ubaba ni wazo la kibinadamu linalounganishwa na shughuli za tendo la ngono, hivyo kumwita Mungu 'Baba' itakuwa ni *shirk*. Lakini tunapomwita Mungu 'Baba', tunasisitiza ukaribu wake kwetu na mahusiano anayotaka tuwe nayo kupitia kwa huyu Kristo, haimaanishi kwamba yeye ni mwanadamu kama tulivyo sisi. Hii inaelezwa zaidi katika Somo la 3.

## Ukaribu na Mungu

Waislamu humwona Allah kuwa yuko mbali sana na hafikiki. Ingawa wanazungumza habari zake kuwa 'yuko karibu sana kuliko mishipa ya shingo zetu', lakini hii haimaanishi mazungumzo ya pande mbili. Wazo la mahusiano ya karibu na Mungu ni geni kwa Waislamu walio wengi, ingawa Wasufi hulitafuta wazo hilo. Wazo la Kikristo kuhusu Mungu ni tofauti sana – Mungu ametutafuta ili autokoe, na anatukaribisha tumwite 'Baba'.

# Somo la 4

## Uzoefu wa Utatu Mtakatifu

Waislamu wanaweza kumgeukia Yesu Kristo bila kuwa na ufahamu wa asili yake ya kiungu, au namna ambavyo inavyounganisha na Baba na Roho Mtakatifu katika Utatu Mtakatifu. Baadaye huwa wanataka ilete maana, hivyo somo la 4 huelezea kidogo kuhusu utatu wa Mungu, bila kuzama sana katika maelezo ya kina maana hii ni kozi ya utangulizi tu. Msisitizo ukiwa ni namna tunavyopata uzoefu wa Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu katika maisha yetu, hata kama hatumwelewi kikamilifu.

Baadhi ya waamini wa mazingira ya Kiislamu wamegeuka nyuma na kuacha kumfuata Yesu, kwa sehemu inatokana na kutopata maelezo ya kutosha ya Utatu Mtakatifu, hivyo ni mada muhimu. Pia wanahitaji njia rahisi ya kuitetea doktrini hii kwa Waislamu watakaowashambulia kuhushu mada hii. Hata hivyo, hatuwezi kutosheka kikamilifu kiakili kuhusu mada hii, na wakati mwingine ni udhuru kwa kushindwa kimaadili. Wewe kama mshauri utahitaji kugundua ni kwa kiasi gani unatakiwa kuzama ndani ya majadiliano ya mada hii pamoja na wanafunzi wako kwa kipindi hiki.

Roho Mtakatifu humdhihirisha Mungu kwetu, hutufungulia mlango kwa Baba na polepole akitufanya sisi kuwa kama Yesu. Kutokana na msisitizo wa juhudi binafsi katika Uislamu, somo hili hukazia sana kuwa ni kwa nguvu za Roho tunaweza kuishi kama Mungu apendavyo. Hii ni muhimu sana kwa Mwislamu. Kutokana na somo hili tunahitaji kujazwa na Roho wa Mungu kila siku, tukimwomba aongoze maisha yetu zaidi na zaidi. Somo hili linajaribu kuongoa hali ya kutoelewana juu ya doktrini za Kipentekoste.

## Dhabihu na Agano

Ingawa Kurani na Hadithi kimsingi hazifundishi kwamba dhabihu huondoa dhambi, Waislamu maarufu hufundisha kwamba dhabihu kwa njia Fulani huondoa dhambi. Hii inadhihirika kwenye sikuku ya Kiislamu ya *Eid al-Adha*, pale Waislamu hukumbuka dhabihu ya Ibrahimu kuwa tayari kumtoa mwanawe pekee (linganisha Mwanzo 22). Hata hivyo, ingawa baadhi ya Waislamu hufikiri kwamba dhabihu huondoa dhambi, haihusishi na agano ambalo Mungu analifanya na mtu atoaye dhabihu hiyo.

Kinyume chake, katika kitabu cha Kutoka 24, dhabihu ya wanyama haikuwa tu kwa ajili ya kuondoa dhambi, bali pia ni ishara na muhuri kwamba watu wa Mungu wameunganishwa naye kwa dhamana iliyo imara ambayo tunaiita 'agano'. Katika Agano Jipya, Kristo amelitia muhuri agano jipya kwa damu yake. Wanafunzi wako lazima wafahamu kwamba ingawa dhabihu ya Kristo hutuweka huru kutoka katika dhambi za kale, pia haimaanishi kwamba tuko huru kwenda na kutenda dhambi tena! Badala yake, tumefungwa imara ndani yake. Tutasoma kwa kina jambo hili katika somo la 15, maswali ya 17-22.

## Uanafunzi katika fikra ya Kisufi

Vitendo vya Wasufi vimeenea sana katika nchi nyingi (siyo zote) za Kiislamu. Wale wanaofuata kwa nguvu njia za Kisufi, hupata mwongozo au mwalimu wa kiroho ambaye kwa Kiarabu huitwa '*murshid*' au kwa lugha ya Kiurdu ni '*pir*'. Mtu huyu huwa ana mamlaka sana juu ya 'wanafunzi' wake ambao huapa agano la kumtii yeye katika kila kitu.

Kutegemeana na mazingira ya wanafunzi wako, mfano huu unaweza kuwasaidia kufahamu namna tulivyojitoa kwa dhati kumfuata Yesu Kristo (ingawa wanafunzi wako) wanaweza wasipendelee kumwita *'murshid'* wao.

## Waislamu, Roho Mtakatifu & Gabrieli

Kitabu cha Kozi katika swali la 8 hutaja jibu la (a) kwa sababu Waislamu wengi hufikiri Roho Mtakatifu ni jina la malaika Gabrieli (kwa Kiarabu ni *Jibrail*).

# *Somo la 5*

## Theologia ya Swala

Katika sura ya 3 tuliona namna wazo la Kikristo la kumfahamu Mungu kama Baba – kwa namna ya karibu na ya kibinafsi kabisa – ni wazo geni kabisa kwa Waislamu. Hii huathiri maombi pia, maana Wakristo hutazama maombi kuwa ni ya kimahusiano ya kina. Kwa Waislamu, swala hufanyika kuwa ni utaratibu wa lazima kumkumbuka Allah kwa siku nzima na kupata fadhila zake. Ingawa Waislamu wana maombi ya kawaida ambayo huitwa 'dua' na baadhi ya tafakari za kiroho, lakini wale wanaoamua kuwa wafuasi wa Kristo hufurahia kupata mahusiano mapya na Mungu ambaye hawakumfahamu hapo mwanzo. Unaweza kuwauliza wanafunzi wako kuhusu uzoefu wao wa swala kabla na baada ya kumpokea Kristo.

## Tafakuri ya Kisufi

Siri za Kisufi zimekuwa na ushawishi mwingi katika baadhi ya tamaduni za Kiislamu. Mashairi ya Kisufi hutumia upondo wa kibinadamu kama mfano war oho inayomtamani Mungu; mpenzi anayetafuta mwenza ni mwanadamu anayemtafuta Mungu (huku katika Ukristo ni kinyume chake!). Tafakuri ya Kisufi huhusisha matamko kwa njia ya kiwimbo ijulikanayo kwa Kiarabu ni *dhikr* au Kiurdu ni *zikr* kwa lengo la kufikia hali isiyo ya kawaida na kuhisi uwepo wa Mungu.

## Waislamu, maombi na utakaso wa '*wudu'*

Mara kwa mara Waislamu katika ibada zao hutawadha, tendo hilo huitwa *wudu* na hufanyika kabla hawaingia katika swala. Huonekana kuwa ni njia ya kuitakasa nafsi kabla ya kuingia katika swala. Wanafunzi wako wanaweza kuona ni msaada kutubu dhambi zetu ni kama *wudu* ya kiroho, ingawa bila shaka Mungu mwenyewe ndiye atutakasaye, na siyo tendo la toba. Hata hivyo, kama mfano huu hauendani na wanafunzi wako, usilazimishe.

## Kuandaa orodha ya mambo ya kuombea

Orodha ya mambo ya kuombea inayopendekezwa huanza siku ya Ijumaa kwa sababu huwa ni siku ya mapumziko kwa wiki katika baadhi ya nchi za Kiislamu. Mahali pengine, ni Jumapili. Kuandika majina ya marafiki ambao ni Waislamu na wanafamilia linaweza kuwa si jambo la busara sana kama mwanafunzi anaishi nao na kama wanaweza kukigundua kitabu cha kujisomea. Pia unaweza kupendekeza orodha za maombi ambazo hupatikana kwa njia ya mtandao katika simu ikiwemo 'PrayerMate' ambayo huruhusu kuandaa au mada za maombi na kuzirudia kila siku.

# Somo la 6

## Waislamu na uvuvio wa Maandiko

Waislamu wana mtazamo tofauti kuhusu maandiko matakatifu kwa Wakristo. Kwao, Kurani na neno la milele la Allah, liliandikwa mbinguni na kufunuliwa kupitia malaika Gabrieli kwa Mohammed. Mohammed aliandika vile vile kwa Kiarabu kwa imla kutoka kwa Gabrieli. Hata hivyo, Wakristo wanaamini kwamba Mungu alivuvia au kwa tafsiri ya moja kwa moja "alipulizia pumzi' ndani ya watu ili waandike Maandiko. Mungu alitumia mchakato wa wanadamu kuandika kusudi lake la kiungu na kulitunza bila makosa. Waarabu huona Kurani ya Kiarabu ndiyo neno takatifu la Allah; tafsiri zingine zote zinapungukiwa hali hiyo. Wakristo huamini kwamba Biblia inaweza kutafsiriwa katika lugha yo yote nab ado ikabaki kuwa ni Neno la Mungu.

Waislamu walio wengi huamini kwamba Biblia imebadilishwa. Wanafunzi wako wanaweza kushawishika na kuaminika kwake lakini inahitaji msaada namna ya kuelezea hilo kwa marafiki zao wa Kiislamu. Pia, wanaweza kushangaa kuhusu tofauti mbalimbali za maneno katika tafsiri mbalimbali, au kuhusu kwa nini maandiko ya kiungu yanaelezea sana habari za wanadamu.

## Mfululizo wa Habari na ufunuo wa Mungu

Biblia imeundwa kuwa ni habari kuu ikianzia kitabu cha Mwanzo hadi kile cha Ufunuo – kuanzia uumbaji hadi uumbaji mpya. Kiini cha habari hii ni Mungu akijituma mwenyewe kwetu. Kurani ina semu kuhusu  tabia ya Allah, na maelezo ya kuishi kulingana na viwango vya Allah; inajumuisha habari fupifupi, lakini haziko katika wendo au mpangilio kwa kufuata matukio na hakuna simulizi inayounganisha kitabu kizima. Katika Uislamu, Mungu alijifunua mwenyewe kwa kutuma kitabu, lakini katika Ukirsto, Mungu alijifunua mwenyewe kwa kujituma mwenyewe, na kujituma huku mwenyewe ndicho kiini cha habari ya Biblia.

# Somo la 7

## Mawe maalumu mawili

Mamilioni ya Waislamu wamekwenda hija huko Makka, ambako jiwe jeusi la Kaba ni alama ya kiini cha ibada yao. Lakini kwetu sisi, Kristo mwenyewe ndiye jiwe lililo la thamani zaidi katika kiini cha ibada yetu, na ni jiwe kuu la pembeni la 'nyumba yetu ya kiroho'!

## Kuponya utambulisho uliogawanyika

Binti mmoja wa Kipakistani huko Uingereza alikuwa akiwa amechanganyikiwa kuhusu utambulisho wake, alikuwa amegawanyika kwa sehemu alikuwa Mwingereza na kwa sehemu nyingine alikuwa Mwislamu wa Pakistani, ndivyo alivyohisi ndani yake. Alipomgeukia Kristo alitamka kwamba amepata utambulisho mpya,  na hiyo 'ilishangaza sana'. Kifungu cha Biblia kilichosema naye kwa nguvu sana kuhusu hili kilikuwa ni kile ambacho tumekisoma, 1 Petro 2:9-10.

## Umma

Waislamu wana hisia za ndani sana kuwa wao ni sehemu ya jumuia ya kiulimwengu ambayo wao huita ni umma. Kwao, umma ni jumuia ambayo hufuata sheria za Allah (*sharia*)  na kwa nadharia lazima isimamiwe na viongozi wa Kiislamu (Kalifu). Jumuia hii ya kiulimwengu hudhihirishwa wazi katika hija ya kila mwaka, ambapo Waislamu wa nchi mbalimbali hukusanyika huko Makka, wote wamevaa kwa kufanana. Hata hivyo, kivitendo, mgawanyiko na ubaguzi (ikiwemo ubaguzi wa rangi), hii humaanisha kwamba umma wa Kiislamu una mapungufu makubwa katika malengo yake.

Kwa njia Fulani, hii hufanana sana na lengo la Kanisa la jumuia ya kiulimwengu, ambapo Wakristo ulimwenguni kote huwa hawaishi kwa kutimiza hilo. Baadhi ya tafsiri za Kiarabu katika 1 Petro 2:9 hutumia neno '*ummah*' kumaanisha watu wa Mungu, na inaweza sana kusaidia kujadili na wanafunzi  mfanano huu au tofauti hizo.

## Kupima uhatarishi uliopo

Katika baadhi ya nchi za Kiislamu, kuna hali hatarishi pale waamini wanapokutanika pamoja. Wakati mwingine watoa taarifa hujipenyeza kwenye makundi hayo, wakijifanya kuwa wao ni waamini. Huchukua majina, mawasiliano na picha za waamini ili kuwaweka wazi, na hii inaweza kuleta maangamizi makubwa. Katika hali kama hizo waamini wawe wenye busara siyo kujiweka wazi kwa kila mtu moja kwa moja, bali wapate muda wa kuwafahamu polepole na kwa makini. Roho Mtakatifu atawaonesha ni nani wa kumwamini moja kwa moja na ni nani wasimwamini haraka. Wawe na tahadhari sana kuchukuliwa picha za kikundi chao. Hata hivyo, kuna hali hatarishi hata kwa upande mwingine.

Kama kila mmoja atakuwa kama Majidi na kukataa kumwamini ye yote, jumuia ya waamini haitaweza kukua. Pia, waamini waliojitenga hukua wakiwa na baridi katika imani yao. Hawatakuwa na mtu wa kuwasaidia kwa kipindi cha kuhitaji msaada. Na kama watoto wao hawatajiunga na jumuia ya Wakristo, watarudi katika dini yao ya zamani. Kama waamini wanawatakia mema watoto wao hapo baadaye lazima watafute mahali pa jumuia ya Kristo. Kwa hiyo, kuna hali hatarishi kama tunakutana na wafuasi wengine wa Yesu, lakini kuna hali hatarishi zaidi kama tutaacha.

Huko Magharibu, waamini wa mazingira ya Kiislamu wanaojiunga na kanisa mara nyingi hawawi katika hatari ya kimwili. Lakini katika hali fulani fulani, wanaweza kutaka iwe siri (kwa mfano, kutoleta hali ya aibu kwa familia zao). Ni uamuzi wao wa lini na nani wamwambie. Wakristo wasiwasengenye hao kwa Waislamu.

# *Somo la 8*

## WMK na Jumuia ya Kiislamu

Waislamu wanaomgeukia Kristo mara nyingi hujisikia wamegawanyika kati ya jumuia yao ya Kiislamu ya hapo awali na jumuia mpya katika Kristo. Familia na jumuia huwa imara sana katika Uislamu, na wale wanaomfuata Kristo mara nyingi hukabiliwa na hali ya kukataliwa na wale wawapendao sana. Ni kwa namna gani wanaweza kurekebisha mahusiano hayo kwa kipindi fulani? Je! watapata ‘familia’ mpya katika jumuia ya Kristo iliyo karibu nao kama familia ya hapo awali? Haya ni maswali yenye msukumo na maumivu kwa **WMK** walio wengi. Somo la 8 hufundisha kwamba wafuasi wa Kristo huwa wana jumuia mbili, ile ya kale na ile mpya, na wanapaswa kuwa sehemu ya zote mbili kadiri wanavyoweza. (Hii ni kweli kwa kizazi cha kwanza cha waamini, lakini mara nyingi migogoro huwa ni mikubwa sana kwa wale wanaotoka katika mazingira ya Kiislamu).

# *Somo la 9*

## Kuwashauri WMK katika mateso

Wakristo wa nchi za Magharibi wanaweza kuwa na mtazamo usio sahihi kuhusu mateso. Tunaweza kupuuza au kuyakumbatia matokeo yake. Kwa **WMK** wanaopitia katika mateso ni muhimu kuwapa ushauri wa busara, katika ngazi zote mbili, ile ya kivitendo na kisaikolojia. Kivitendo, mara zote ni vizuri kwa WMK kubaki katika familia na jumuia zao, huku wakiitikia kwa uvumilivu upinzani wo wote mpaka pale utakapotulia. Katika mazingira ambapo kuna hatari kubwa, **WMK** wanaweza kukimbia kwa ajili ya usalama, lakini baadaye wajaribu kurejesha mahusiano na familia zao. Hatari za kimaisha siyo kitu cha kawaida kwa **WMK** waishio katika nchi za Magharibi.

Kisaikolojia, ni muhimu kutambua namna **WMK** wanavyoumia kwa ndani pale wanapokataliwa na familia zao, na ni kwa kiasi gani wanawakosa ndugu zao. Kipengele kikuu cha kurejesha mateso katika hali njema, ni kupata mtazamo wa Kimungu kuhusu mates ohayo, ambalo ndiyo lengo la somo hili.

# Somo la 10

## Kisasi na msamaha

Somo hili liliandaliwa kwa ajili ya nchi ambako ‘mzunguko wa kisasi’ umesababisha matokeo hatarishi sana kwa kizazi kizima. Ingawa siyo Waislamu wote hutetea ulipizaji kisasi, bado ni jambo lililo na nguvu sana katika tamaduni za Kiislamu. Asili ya mwanadamu mwenye dhambi hupatikana katika tamaduni zote, ikiunganishwa na shauku ya kuonekana ‘mwenye nguvu’ na ‘kurejesha heshima’ katika jamii za kienyeji, humaanisha kwamba Waislamu wengi hudhani kwamba ni kawaida kulipiza kisasi. Kwa hiyo, Waislamu wanaokutana na amri ya Kristo ya kuwapenda adui zao (aya ya kuriri kwa wiki hii) huona kuwa ni mafundisho mapya na matokeo yake wengi wamevutwa kwa Kristo.

**WMK** walio wengi hushikilia maumivu na uchungu ndani ya mioyo yao kwa wale walio watesa au kuwakataa kwa ajili ya imani yao (kwa mfano, swali la 15). Kuachana na hali hiyo hi muhimu sana ili kuwasaidia kusonga mbele katika Kristo. Ni kwa sababu hii mada hii imesisitizwa katika somo hili, na imeelezwa mara kwa mara. Majadiliano ya mada hii inaweza kuondoa mihemuko yenye nguvu, lakini inaweza kupelekea uponyaji!

Swali la 5 huweka utofauti kati ya Yesu aliyekufa akisamehe watesi wake, na viongozi waliokufa katika uwanja wa vita wakiwalaani maadui zao. Dokezo ni kumkumbuka kiongozi Huseini, aliyeuawa katika vita ya Karbala mnamo mwaka wa 680 BK, hukumbukwa sana na Waislamu wa Kishia, na husimama ikitofautiana na kifo cha Kristo. Inaweza kufaa au isifae kutaja hili kwa wanafunzi wako, inategemeana na nia zao kwa Uislamu wenye mtindo wa Kishia.

# Somo la 11

## Ndoa katika Uislamu

Kwa Waislamu kama ilivyo katika tamaduni zote, baadhi ya ndoa zina utulivu na baadhi yake zina migogoro, hivyo ni vigumu kusema kwa ujumla. Maisha ya kifamilia ya Kiislamu mara nyingi huvutia kwa namna nyingi, ingawa kunaweza kuwepo na ukatiri na hali ya kuvunja moyo iliyofichika.

Wanazuoni wa Kiislamu hutofautiana katika ufafanuzi wa mafundisho ya Kurani kuhusu ndoa, na baadhi baadhi ya jamii ambazo zina msimamo wa kiume huwatesa wanawake zaidi kuliko ilivyo Kurani. Hata hivyo, kozi hii huzungumzia mawazo ambayo yanapokelewa na jamii nyingi za Kiislamu, kama vile, mwanaume anaruhusiwa kumpiga mkewe au kutalakiana naye kirahisi, anaweza kuoa hadi wake wanne, na sababu moja inayokubalika ya kuchukua mke mwingine ni kama mke mwingine hawezi kuzaa watoto. Na mke pia ana haki katika Uislamu, ingawa haki hizo siyo kama zile za mume. Kikanuni, ndoa ni mkatabu siyo agano.

Somo hili lina lengo la kuwasaidia wanafunzi wako kutathimini mawazo waliorithishwa kuhusu ndoa na kujenga msingi wa Kibiblia zaidi. Mawazo ya kawaida ya Kiislamu yamezungumzwa katika sura hii, yale yanayotofautiana na mafundisho ya Kibiblia, na swali la 10 linalileta wazo hili kwa kutumia aya ya Kurani inayojulikana sana ‘wanawake wenu ni mashamba yenu’ (Sura 2:223). Mafundisho ya Biblia kwamba mwanamume ataoa mwanamke mmoja maisha yake yote, na mwanamume aoneshe pendo la kidhabihu kwa mke wake, ni muhimu sana. Somo la 11 linaanzisha tu mada hii pana, na kama mwanafunzi wako tayari ameoa au anajiandaa na ndoa, inaweza kuwa ni vizuri kumpa mafundisho zaidi. Hii pia hutumika kama watapenda kujadiliana kuhusu malezi ya watoto.

## Umama katika Uislamu

Katika Uislamu, mama huwa anaheshimika sana. Vijana wa Kiislamu wanaamriwa kutoa heshima kubwa na uaminifu kwa mama zao na mara zote kuna mahusiano makubwa sana kihisia na mama zao kuliko baba zao. Pia, kitamaduni, katika tamaduni nyingi za Kiislamu bibi arusi huwaacha wazazi wake siku ya ndoa na kujiunga na familia ya mumewe, lakini hakuna ‘kuacha na kuambatana’ kwa ajili yake. Maana uaminifu wake wa kihisia unaweza kuendelea kuwa imara kwa mama yake kuliko kwa mke wake, na mama anaweza kuwalaghai kwa manufaa yake na siyo kwa faida ya bibi arusi. Somo hili linashughulikia mambo haya. Lakini ni kwa ujumla wake tu, na kwa mazingira ya Kimagharibi ambapo familia kwa kuwahusisha ndugu haina nguvu sana.

# Somo la 12

## Mabishano na namna ya kuyatatua

Binadamu wote katika jamii zote huwa na mabishano kwa nyakati tofauti tofauti, na jamii za Kiislamu hazijakwepa hili. Njia tatu mbaya za kutatua 'mabishano' ambazo zimeelezwa katika swali la 7-10 hupatikana mara nyingi katika jamii za Kiislamu, husisitizwa kwa maadili ya kitamaduni ya ulipizaji kisasi, kuacha au mtiririko wa kiutawala. Usengenyaji pia huchanganya mambo. Bila shaka, matatizo haya hupatikana katika jamii zingine pia.

Waislamu wengi hutoka katika miktadha yenye heshima/aibu. Yaani, wazo lao la mema na mabaya huhusiana kwa ukaribu sana ha hali zai katika jumuia zao. Kama familia haina heshima katika jumuia, wanaweza kuhesabiwa haki kurejesha heshima yao kwa kulipiza kisasi. Utamaduni wa Mashariki ya Karibu kipindi cha Yesu inaweza kuwa ulikuwa na mazoea hayo. Kwa wale wa Magharibi, mafundisho ya Yesu kuhusu msamaha mara nyingi hushughulika na ngazi ya mtu binafsi. Lakini kwa wale wanaotoka katika tamaduni zenye heshima/aibu, amri ya Yesu inaweza kuwahusu jumuia nzima, ambapo ulipizaji kisasi unaweza kurithishwa kizazi hadi kizazi kingine.

Baada ya furaha yao ya awali ya kujiunga na jumuia ya wafuasi wa Kristo, **WMK** mara nyingi hukutana na migogoro na kukua bila kuwa na taswira sahihi. Kujifunza kushughulikia hili na kuhamia upande wa pili ni hatua muhimu sana katika uanafunzi wao. Hii hujumuisha namna ya kushughulika na mabishano kwa njia inayojenga na siyo ile inayobomoa. Somo la 12 linaweka hatua za kivitendo ili kuwasaidia kuliweka hili katika vitendo.

## Je! Mungu ana mihemuko?

Kaatika Uislamu, Muumbaji ametengana na viumbe vyake na vivyo hivyo kwa viumbe. Waislamu hupinga kwamba matendo ya mwanadamu yanaweza kumfanya Mungu afurahi au asikitike, au kwamba anahisi maumivu yetu, kwa sababu hii inasikika kana kwamba tunamlazimisha kumshusha chini mpaka afikie ngazi yetu au kumfanya yeye kuwa katika sura yetu wenyewe. Kwa Wakristo, tendo la Mungu kufanyika mtu humfunua Mungu aliyetayari kushuka chini hadi kwenye ngazi yetu na kushiriki maumivu yetu. Yesu Kristo alihisi kwa nguvu mihemuko (huruma, hasira, furaha, huzuni) na anatupatia picha ya Mungu yukoje. **WMK** wakitambua hili, hubadilisha mtazamo wao kuhusu Mungu, maana anahisi maumivu yao (ona Somo la 11, 18) na husikitika pale wanapotenda dhambi (kama ilivyo katika Somo la 12).

# Somo la 13

## Waislamu na ushuhuda (*Shahada)*

Kwa Waislamu, kutoa ushuhuda kimsingi humaanisha kurudia kutamka tamko la Kiislamu (*shahada*): "Hakuna Mungu ila Allah, na Mohammed ndiye mtume wake." *Shahada* ni kiini cha utambulisho wa Kiislamu na ni moja ya 'nguzo' za kuwa Mwislamu. Hunong;onezwa masikioni kwa mtoto mchanga aliyezaliwa na  kuimbwa katika wito wa zile swala tano za kila siku.

Kwa Wakristo, ushuhuda wa mapema ulikuwa kwamba Yesu Kristo amefufuka kutoka katika wafu, na hakika ni Bwana (Rum. 10:9). Ushuhuda huu ni kiini cha utambulisho wa Kikristo, hivyo inaweza kuwa ni msaada kuelezea neno *shahada* kwa WMK kuwa ni tendo la kutoa ushahidi kuhusu ufufuo na Ubwana wa Kristo. Hata hivyo, wanafunzi wako wanaweza wasipendelee kutumia neno hilo la Kiislamu kwa njia hii, hivyo uwe makini kwa mapendekezo yao.

Katika Agano Jipya, neno la Kiyunani lenye maana ya 'ushuhuda' pia humaanisha 'kufia dini', na ulinganifu huo hupatikana katika Kiarabu. Shahidi ambaye anatoa ushuhuda (*shahada*) anaweza kuwa mfia dini (*shaheed*).  Hii iko wazi sana kwa **WMK** wanaokufa kwa ajili ya imani yao, kama vile Mehdi Dibaj katika somo hili. Wakristo wengi wa huko Irani hutiwa moyo na mfano wake na wafia dini wengine katika nchi ya Irani waliokufa kwa ajili ya Kristo. Somo la 13 huleta muunganiko huu na wanafunzi wanaweza kuona kuwa inaleta maana sana.

Kwa **WMK**, ni mahangaiko hasa kufahamu namna, lini na kwa nani wamwambie habari za Kristo katika wanafamilia wao. Wanaweza kuwa na hofu kushuhudia au kuhisi hatia kutoshuhudia. Wanafunzi wanaweza kuwa ni mihemuko kiasi kadiri wanavyozungumzia mahangaiko waliyonayo katika eneo hili, na hamu yao ya kuona ndugu zao wanampata Kristo. Ruhusu mihemuko hiyo idhihirike.

## Ujasiri au tahadhari?

Kwa baadhi ya **WMK**, ushuhuda na ukuaji wao wa kiroho huharibika kwa sababu ya kuhofu kuwaambia wengine kuhusu Kristo. Kinyume chake, wengine husema kwa ujasiri sana na kwa haraka, na hii inaweza kuharibu zaidi hasa itachochea mgogoro kipindi ambacho siyo sahihi. Kwa hiyo, wafuasi wengi wenye uzoefu huwa wanahisi kwamba njia nzuri kwa **WMK** kuandaa mazingira polepole kwa kuelezea uaminifu wao mpya, na siyo kubaki kuwa ni siri wakati wote. Ni haraka kiasi gani 'kujitokeza' kama mfuasi wa Kristo hii hutegemeana na hali ya mazingira, ikiwemo nia ya familia, na kama uhuru katika nchi ile umeminywa sana au uko wazi (kama ilivyo katika nchi za Magharibi).

Pia, weka akilini kwamba kuna sehemu ya katikati kati ya kuwa 'msiri' au 'mwazi'. **WMK** walio wengi huwa wako wazi kuhusu imani yao kwa baadhi ya watu fulani ambao wanawaamini, na siri kwa wengine. Kufunguka ni mchakato wa polepole. Hata hivyo, wakati mwingine **WMK** hujikuta kwamba imani yao imewekwa wazi kwa ndugu zao wa Kiislamu kwa bahati mbaya au mapema mno, na wanapaswa kuwa tayari kwa hili pia, wakiwa na majibu sahihi.

Mada hii ya namna ya kutoa ushuhuda ni muhimu sana kwa **WMK**. Somo la 13 linataka kufungua mambo kwa uwiano ulio sahihi, lakini namna ambavyo mambo hayo yanatumika yatatofautiana kutoka kwa mwanafunzi mmoja hadi mwingine. Kwa hiyo, hekima na maombi sana huhitajika katika kuwashauri waamini binafsi.

## Mchoro wa 'Daraja'

Mchoro katika sehemu ya nyongeza ya 2 inafanana na 'mchoro unaojulikana wa daraja' lakini umetumika kwa ajili ya utamaduni wa Kiislamu kwa njia zifuatazo:

- Hauoneshi picha yo yote ya Mungu.
- Humwonesha Mungu yuko juu yetu, na siyo katika ngazi yetu.
- Huzungumzia Njia Iliyonyooka na siyo Daraja.

Hata hivyo, inawezekana kuionesha picha kwa mlalo kama ulivyo mchoro wa daraja la kawaida, na kujenga katika wazo la Kiislamu kwamba tunapaswa kuvuka daraja jembamba ili kufika Peponi. Waislamu walio wengi hufundishwa kwamba daraja hili ni 'jembamba sana kuliko unywele wa mwanadamu' na wengi wana mashaka kwamba wanaweza kudondoka wasifike Peponi.

Tunaweza kueleza kwamba Yesu Kristo ni ndiye pekee anayetuvusha daraja hilo. Hadithi moja husimuliwa kuhusu mtu mmoja aitwaye Blondini aliyevuka maporomoko ya maji ya Niagara kwa kutumia kamba nyembamba na aliwaomba wenzake kwamba awabebe mgongoni mwake ili awavushe. Wengi walikataa, lakini mtu mmoja alimwamini na kupanda mgongoni mwake. Blondini alimbeba mtu huyo nadi ng'ambo ya pili. Yesu Kristo anajitoa kwamba atatufikisha salama huko Peponi, lakini lazima tuyawekeze kwake maisha yetu. Kama sehemu ya somo hili unaweza kuonesha video fupi kuhusu Blondini kama inavyoshauriwa katika mpangilio wa somo hili.

Ombi la mrejesho: tafadhali waoneshe wanafunzi wako katika matoleo yote mawili: wima (kama ilivyo kwenye kitabu cha kujisomea) na malalo (kama daraja la kwenda Peponi). Waulize ni toleo lipi litakaloendana zaidi na Mwislamu. Tafadhali toa maoni yako kwa comefollowmecourse@gmail.com ili tuweze kubadilisha kitabu cha kujisomea hapo baadaye kama itahitajika.

# *Somo la 14*

## WMK na ubatizo

Ubatizo ni hatua muhimu kwa **WMK**. Huwa ni alama ya uaminifu wao kwa Kristo na jumuia yake. Hata hivyo, familia na jumuia zao za Kiislamu huiona hatua hii kuwa ni alama ya usaliti. Kwa mtazamo wao, mtu anayebatizwa huikataa familia yake ya kale na kuleta aibu kubwa kwao. Hii huifanya familia na jumuia kwa ujumla kuwa na hasira sana, na katika baadhi ya nchi za Kiislamu wanaweza hata kumwua muumini huyo. Huko Magharibu hakuna hatari kubwa, lakini yawezekana kukawa na hali ya maumivu na kukataliwa. Ni vizuri kuwa na tahadhari ya mambo haya na kujaribu kupunguza mshtuko na aibu kwa familia kadiri inavyowezekana.

Kwa hiyo, katika maandalizi ya ubatizo wa **WMK** usiwaze tu kipimo cha kiroho bali pia maana ya kijamii. Jadili pamoja na mtu huyo:

- Ni upi muda mzuri kwao kwa ajili ya kubatizwa? (Mara zote Mungu atawaonesha kwa Roho wake; lakini muda ukiwa sahihi, usiahirishe).
- Ni akina nani wanapaswa kuhudhuria kwenye ubatizo? (angalau marafiki wa karibu kabisa; lakini vipi kuhusu kanisa kwa upana wake, au vipi kuhusu ndugu wa Kiislamu? Jadili maswali haya na muumini, maana hali hutofautiana).
- Je! Muumini huyu atawajulisha ndugu zake Waislamu kabla ya tukio? Hii inategemeana sana na hali ya familia)
- Je! picha zitapigwa wakati wa ubatizo na je! kutakuwa na udhibiti wo wote katika kusambaa kwake? Kwa picha za mfumo wa kidijitali na mtandaoni hii ni swala la muhimu sana! Usambazaji wa picha za ubatizo unaweza kuleta hali ya hatari kwa waamini na hakika kuleta aibu katika familia yao. Jambo lililo la makini sana ni pale **WMK** wanaingia ndani ya maji, HASA kama ni ubatizo wa wanaume na wanawake. Picha kama hizo lazima zizibitiwe kabisa. Lakini picha za makundi baada ya hapo, za watu waliobatizwa wakiwa pamoja na marafiki zao Wakristo, hazina umakini sana).
- Kwa **WMK** wanawake, ni hatua gani zitachukuliwa kulinda unyenyekevu wao wakati wakitoka kwenye maji? (nguo nyembamba hung'ang'ania mwili zinapolowana. Vaa nguo nzito na uwe na taulo ya kujifunga kiunoni mara watokapo ndani ya maji).
- Je! cheti cha ubatizo kinaweza kutolewa? (Hili halina tatizo katika nchi za Magharibi, lakini inaweza kuwa ni hatari kwa nchi zenye msimamo mkali wa Kiislamu, kwa wote wawili, mbatizaji na mbatizwa. Lakini uthibitisho wa ubatizo ni muhimu. Jadilini hili.)

## Utaratibu wa kutawadha katika Uislamu

Katika Uislamu, ni lazima kutekeleza wudu (utaratibu wa kuosha kichwa, mikono na miguu) kabla ya swala tano za kila siku. Kuoga mwili wote ni mara chache sana au *ghusl* ambayo inaaminika hutakasa dhambi kubwa. Waislamu wapya hufundishwa kwamba dhambi zao za kale huondolewa pale wanapoongoka kuingia katika Uislamu, na wengi wao hufanya *ghusl* kamili kama ishara ya hilo. Hata hivyo, wale wanaoondoka kwenye Uislamu na kumgeukia Kristo mara zote hulenga ubatizo kuwa ni ishara ya kufufuka katika maisha mapya kuliko kule kuondoa dhambi.

# *Somo la 15*

## *Sheria* na utunzaji wake katika Uislamu

Somo la 15-17 huzungumzia mada muhimu sana kwaw wale wanaomgeukia Kristo kutoka kwenye Uislamu. Hii ni kwa sababu 'sheria' ni ya muhimu sana katika Uislamu. Hakika, neno la Kiarabu '*shariah*' siyo sheria tu na maana yake ndogo, bali ni mtindo wa maisha yote. Kama mwanazuoni wa Kiislamu aitwaye Badru Kateregga aliandika, *shariah* ni "maadili ya kina ya mwenendo kwa Waislamu kuweza kufuata, katika maisha yao binafsi ya yale ya hadharani". Humwambia mtu "namna atakavyokula, kupokea wageni, kununua na kuuza, kuchinja wanyama, kujisafisha mwenyewe, kulala, kwenda chooni, kuongoza serikali, kutenda haki, maombi" (Kateregga & Shenk: Uislamu na Ukristo, Uzima Press, Kenya (1980), ukr.67). Hivyo, Waislamu waaminifu hutaka *shariah* siyo tu kwa kujenga maisha yao wenyewe, bali pia jamii nzima na utamaduni wote. Utii huu unaaminika kuleta baraka za Allah katika maisha haya na thawabu katika maisha yajayo.

Watu wanaouacha Uislamu huwa wanajisikia huru kutoka kwenye maadili haya ya kina lakini huwaacha wakiwa na maswali ya kujiuliza na kuyafanyia kazi. 'Sheria' ina nafasi gani katika maisha ya Mkristo? Kama haina nafasi, tuko huru kufanya lo lote tutakalo? Kama ina nafasi, basi asili yake ni nini? Kwa nini tunaitii 'shria hii ya upendo': kutafuta thawabu au ni kutokana na furaha? Tunawezaji kushughulikia mambo maalumu, kwa mfano, ni wakati gani wa kufunga na tutoe kiasi gani? Ni kanuni zipi zinazotuongoza katika kumtii Kristo kuwa ni Bwana kama kuna maelezo kidogo hivyo ya miongozo ukilinganisha na *shariah* ya Kiislamu?

Hivyo, mazingira ya kitheologia kwa somo la 15-17 ni tofauti sana na yale ya Kimagharibi. Kwa namna fulani, inakaribia sana na mazingira ya kitheologia ya Biblia (ingawa kuna tofauti pia kati ya

sheria ya Musa na *Shariah* ya Kiislamu). Kusudi la sheria ya Mungu katika Agano la Kale, na ukatiri wa Mafarisayo na sheria mpya ya upendo' iliyofundishwa na Yesu, yote huwa ni ya muhimu kwa WMK.

Kama maelezo ndani ya sura hizi ni mageni kwako, waombe marafiki zako wa **WMK** kutoa maoni yao kutokana na mitazamo yao. Baadhi ya Waislamu wa zamani wanaweza kusaidiwa na ufahamu kwamba katika Kristo tunaishi chini ya aina mpya ya *shariah*. Baadhi yao wana mwitikio wa kimhemuko dhidi ya neno *shariah* kutokana na kile ilichobeba kwa uzoefu wao wa zamani, lakini bado wanapaswa kufahamu wazo kwamba tunamtumika Bwana mpya na hatuko huru kufanya kile tunachokitaka.

## Waislamu na njia Iliyonyooka

Kila siku Waislamu huswali, "tuongoze katika Njia Iliyonyooka". Wamefundishwa kwamba maelfu ya manabii walikuwa kufundisha njia ya Mungu iliyonyooka. Baadhi tu ya hao wametajwa katika Kurani na inavutia kuona kwamba wengi wao wanatoka katika Biblia: Adamu, Nuhu, Ibrahimu, Musa, Daudi, Yesu na wengine wachache. (Waislamu huwaita Adamu, Nuhu, Ibrahimu, Musa, Daudi na Isa).

Waislamu huamini kwamba manabii wote hawa walikuja kuwaonesha wanadamu 'njia iliyonyooka' ya *shariah* za Mungu, hivyo kwa kuzifuata hizo wanaweza kupata thawabu na baraka zake. Hata hivyo, hata kama tungeijua hiyo njia iliyonyooka na kutaka kuifuata, je! tunaweza kufanya hivyo? Kama siyo, kwa nini siyo? Hiki ni chanzo cha kitheologia cha Somo la 15.

## Dhambi 'kubwa' na 'ndogo'

Waislamu hufundishwa kwamba baadhi ya dhambi zina umakini zaidi kuliko zingine. Mungu anaweza kupuuza dhambi 'ndogo' kama vile kusema uongo, lakini zile 'kubwa' lazima zipate hukumu. Pia kama mtu fulani ana 'nia' (*ne-ah*) ndani ya moyo wake kufanya kitu fulani na asikifanye, siyo dhambi. Hii inakinzana na mafundisho ya Kristo kwamba kutazama kwa kutamani ndani ya moyo ni dhambi, kama uzinzi (ona swali la 13).

Sehemu hii hufundisha kwamba sheria takatifu za Kristo huweka kiwango cha juu sana. Kimaadili, ni ngumu kuzishika na kuzitunza kuliko *shariah* ya Uislamu, hata kama inaonekana rahisi kwa mtazamo wa kiutaratibu.

# *Somo la 16*

## Motisha wa Waislamu kuhusu utii

Somo la 16 huendeleza majadiliano ya sheria ya Mungu, ambayo yalianza katika Somo la 15 (ona hapo kwa maelezo ya kijumla). Pa kuanzia katika somo hili ni tofauti kati ya utii wa sheria za Mungu kutokana na tumaini la thawabu au hofu ya hukumu, na utii unaotokana na furaha na yote aliyotufanyia sisi. Hii ni hatua ya msingi ya mwonekano pale Mwislamu anapomgeukia Kristo.

Tunapenda kwa sababu Mungu alitupenda sisi kwanza, kama inavyooneshwa kwa kifo cha Kristo pale msalabani. Kwa hiyo, kwa kujibu, tunataka kutii 'sheria ya upendo' ambayo ni kumpenda Mungu kwa moyo wote na majirani zetu kama nafsi zetu.

## Waislamu, WMK na ukarimu

WMK hutoka katika tamaduni ambazo huthamini sana ukarimu. Kinyume chake, Wakristo wa huko Magharibi wana kitu cha kujifunza katika eneo hili la kukaribisha watu katika nyumba zao. Kama WMK akija nyumbani kwako bila taarifa, je! atakaribishwa hata kama hajatoa taarifa mapema? Kama watu kanisani mwako watamwambia **WMK** kuwa ni 'familia' yake, je! watakuwa tayari kumchukua pale familia yake itakapomtupa nje nay eye anahitaji mahali pa kuishi?

# *Somo la 17*

## WMK na miongozo ya kina kuhusu *Shariah*

Baada ya kutoa muhtasari wa mafundisho ya sheria ya Mungu katika Somo la 15 na 16, somo hili huuliza namna wafuasi wa Kristo wanaweza kulitekeleza hilo kwa vitendo, wakati hatuna aina ile ile ya miongozo ya kina ambayo hupatikana katika Uislamu.

Hapa tunatazama hasa 'nguzo' mbili za Uislamu ambapo Waislamu huambiwa kile cha kufanya. Lazima wafunge kuanzia jua kuchomoza hadi machweo ya jua kwa mwezi wa Ramadhani na lazima watoe sehemu fulani ya mali zao kama zaka (kodi ya hisani). Je! wafuasi wa Kristo wafanya nini katika mambo haya? Somo hili hufundisha kanuni za Kibiblia, huku tukitambua kwamba makanisa mbalimbali huzitumia kwa namna tofauti tofauti. Hivyo, kama mshauri, uwe huru kufundisha vile vile kama kanisa lako lifanyavyo, lakini kumbuka kwamba jambo la muhimu sana ni kwa muumini kuzifahamu kanuni. Weka uwiano ulio sawa kati ya kumpatia mtu miongozo maalumu kama wanaitaka, lakini siyo kutawala maisha yao. Wasaidie wamtii Yesu Kristo kuwa ni Bwana na kufuata maongozi yake juu ya vitu vyote.

## WMK na Ramadhani

Katika nchi nyingi za Kiislamu, Ramadhani ni kipindi maalumu kwa umoja wa kifamilia. Uwe makini kwamba hiki ni kipindi cha mwaka ambapo **WMK** wanazikosa familia zao. (Kipindi kingine cha upweke ni wakati wa Krismasi, ambapo Wakristo huwa wanashughulika na familia zao na kusahau kwamba waliokuwa Waislamu hapo awali huachwa wapweke bila mtu wa kusherehekea pamoja nao).

Kwa **WMK** ambao bado wanaishi na familia zao, njia panda ya Paveni ni dhahiri, ajiunge au asijiunge na mfungo wa Ramadhani. Baaadhi ya Wakristo huamini kwamba hii inaweza kuwa ni njia sahihi ya kuonesha uaminifu kwa familia; muumini anaweza kufunga kwa ajili ya Yesu na siyo kwa wajibu wa Kiislamu, na huzuia mateso yasiyo ya lazima kwa jambo lisilo na maslahi. Wakristo wengine huamini kwamba hiyo ni muhimu kuonesha msimamo na kutengana na familia katika jambo hili, kuonesha ushuhuda wa wazi na kuzuia udanganyifu. Lakini, kufunga siyo ushuhuda mzuri, kama huwafanya Waislamu wawaze kwamba Wakristo ni wazembe katika jambo hili?

Jadilini mitazamo hii ya tofauti na wanafunzi, ukizingatia kwamba mengi hutegemeana na hali za familia zao. Kama wataamua kutofunga wakati wa Ramadhani, je! watafunga kwa kipindi kingine, kama Bwana aelekezavyo?

## Waislamu na utoaji

Katika zaka au kodi ya hisani, kiasi kimezingatiwa ni 2.5% ya mtaji wa Mwislamu kila mwaka (siyo mapato yao), kukiwa na miongozo ya kina namna ya kukokotoa hiyo kila mwaka. Watu wako huru kuchagua kumpatia nani, ilihali inakidhi vigezo fulani kama vile kusaidia masikini au kuenea kwa Uislamu. Pia, Waislamu wengi hutoa kwa hiari yao ndani ya mwaka na kwa kusudi hili, au kwa ajili ya gharama za msikiti, n.k.

# *Somo la 18*

## Waislamu na uchawi

Watu wa Magharibi wanaweza kushangaa kuona kwamba 'bahati' na 'uchawi' ni mawazo muhimu kwa Waislamu wengi ulimwenguni. Kihistoria, imani hizi zilikuwepo katika tamaduni nyingi kabla watu hawaja Waislamu, na mchanganyiko huo hujulikana kama 'Uislamu wa kawaida'. Pia, katika Uislamu wenyewe, Allah huonekana yuko mbali sana. Kama anaamua kila kitu na mwanadamu hawezi kufanya cho chote cha kubadilisha, hii husisitiza bahati ndiyo inayotawala maisha yao. Zaidi ya yote, kwa kuwa Allah anadhaniwa kuwa yuko juu sana, Waislamu hawana hakika kama anajali kwa karibu matatizo yao au kusikiliza maombi yao, hivyo hutafuta msaada kwa wapatanishi wengine wa kiroho ambao huonekana kirahisi. Vipengele vyote hivi vinawashawishi Waislamu wa leo.

Utafutaji wa majibu kwa maombi au nguvu ya kiroho au maarifa yaliyofichika, hupelekea baadhi ya Waislamu kujishughulisha na shughuli za kiuganga na ushirikina. Baada ya kumgeukia Kristo, watahitaji kufunguliwa kutoka katika utumwa. Kwa wengine, huonekana kuwa ni ushawishi wa kitamaduni, kwa mfano, kuweka kago mikononi au kwenye magari kwa ajili ya 'ulinzi'. Wengine wanaweza kuwa na uzoefu kidogo kuhusiana na jambo hili.

Somo la 18 hutoa mafundisho ya kibiblia juu ya mada hii. Lakini kutaja tu shughuli mbaya haina tija sana kuliko kutathimini mtazamo unaoshikilia mambo hayo. Kama WMK wataweza kumtegemea Kristo aliyeshuka hadi akatufikia (hivyo akahisi maumivu yetu) na kisha akafufuka akapaa mbinguni juu kuliko mamlaka yote ya kiroho (hivyo kuwashinda), hivyo wakati wa hitaji watakuwa tayari kumkaribia Kristo mwenyewe kwa ajili ya msaada. Pia kifo kilishinda nguvu zote za giza na kutuweka huru tusiishi katika hofu ya nguvu hizi za uovu.

## Waislamu na nguvu za kiroho

Waislamu wengi huamini katika nguvu za kiroho kama vile:

- **Malaika**, wakiwemo baadhi yao wametajwa katika Biblia kama vile Gabrieli (Jibrail), pia malaika binafsi ambao hutunza kumbukumbu za matendo mema na mabaya ya kila mtu;
- **'Jicho ovu'**, ushawishi wa ambao unaweza kusababisha madhara kwa watu, kama vile mtoto anayesifiwa kwa kuwa mrembo;
- **Bahati**, kulingana na hatima ya watu ambayo tayari imekwisha kuandikwa na hawawezi kuibadilisha kwa cho chote;
- **Majini**, viumbe vya kiroho ambao wanaweza kuwa wema au waovu zaidi, kwa mfano kusababisha magonjwa au upungufu wa akili;
- **Roho wabaya**, kulingana na wazo la kibiblia.

Wanakikundi wanaweza kuelezea vitengo tofauti ambavyo hutumiwa na Waislamu katika ushawishi wa uovu ikiwemo: kago kwa ajili ya watu na magari, hirizi, picha za jicho n.k.

Kwa kawaida Waislamu huamini katika *baraka*, 'baraka' zisizoonekana huunganishwa na watu watakatifu au mahali patakatifu (yakiwemo makaburi ya watakatifu), ambayo hutekeleza shughuli zao kwa kuyafikia kwa karibu. Wakati mwingine watu hufunga nguo juu ya miti karibu na madhabahu kama kumbukumbu ya maombi au viapo waliyofanya hapo. Au wanaweza kutoa kiapo cha uaminifu kwa viongozi wa kiroho (huitwa *pir,murshid* au *marabout* katika sehemu tofauti tofauti za ulimwengu wa Kiislamu), kwa kuwatii bila kujua na kutafuta upatanisho wao na Mungu.

Baadhi ya Waislamu hutoa matoleo yao kama *sadaka* (k.m. kutoa fedha au dhabihu ya mbuzi mweusi) ili kutafuta kusudi maalumu kama vile uponyaji. Hii ni tofauti na dhabihu ya *kurbani* ya mwaka itolewao kwa kumkumbuka Ibrahimu.

## Kutoa faraja

Katika tamaduni nyingi za Kiislamu ni kawaida kutembelea mara moja watu waliofiwa, kukaa pamoja nao na kushiriki katika majonzi yao. Ni njia muhimu ya kuonesha umoja, na inakaribiana na utamaduni wa kipindi cha Biblia (mfano Yohana 11) kuliko ilivyo katika nchi za Magharibi leo.

Hata hivyo, njia ya kawaida ya Waislamu kujaribu kutoa faraja ni kusema 'yalikuwa mapenzi ya Allah', tunapaswa kuikubali hatima yetu. Katika swali la 6 tunapendekeza kwamba **WMK** anaweza kutoa faraja ya kina, kwa njia tofauti kwa mtazamo wa Mungu: Mungu ajaye karibu na kushiriki mateso yetu.

# *Somo la 19*

## Kutawadha miguu katika tamaduni za Kiislamu

Waislamu wengi huishi katika tamaduni ambapo miguu hudhaniwa kuwa michafu sana, inafanana na kipindi cha Yesu. 'Kuinua goti' dhidi ya mwingine au kumtupia mtu kiatu, huonekana kuwa ni hatia kubwa. Kisha kutawadha miguu ya mtu mwingine, ni njia nzuri sana ya kuonesha mfano wa unyenyekevu wa Yesu.

## Mambo ya kiuongozi katika vikundi vya WMK

Kukosa umoja ni jambo la kawaida kabisa katika vikundi vya **WMK**, katika nchi za Waislamu na hata zile za Magharibi. Kwa Mwislamu mmoja kuwa mfuasi wa Kristo huwa ni vigumu sana; kwa wafuasi hao kukutana pamoja kama kikundi ni vigumu sana; ili kikundi kiendelee kukaa pamoja chini ya viongozi waliokomaa bado ni vigumu. Uongozi mzuri wa vikundi vya **WMK** ni mada muhimu sana!

Kozi ya 'Njoo Nifuate' ni kwa ajili ya waamini wapya, hivyo haigusi sana mambo ya uongozi. Hata imedokezwa tu katika sehemu hii, lakini unaweza kufuatilia jambo hilo hapo baadaye, wanafunzi watakapokuwa tayari kwa ajili hiyo.

# *Somo la 20*

## Waislamu, hija na peponi

Kwa Waislamu ni jukumu la kidini kwenda kuhiji Makka angalau mara moja katika maisha yao kama wanaweza, hii huwezekana tu kwa sehemu ndogo ya Waislamu wote ulimwenguni na huonekana kama manufaa. Kozi hii imetoa dokezo kuhusu 'nguzo' za Kiislamu kwa njia tofauti, ingawa siyo kwa kuzikazia sana maana **WMK** hupendelea kuweka ukomo wa wazi kuhusu mawazo ya Kiislamu.

Katika somo hili, ulinganifu uliofanywa na maisha ya Kikristo kama hija ya kwenda mbinguni (kitabu maarufu sana cha Safari ya Msafiri kinafanya hivyo pia). Katika Uislamu, mbingu imeelezwa kuwa ni peponi iliyo na starehe nyingi. Katika Somo la 20, furaha pekee ya mbinguni hufundishwa kwamba tutakuwa pamoja na Mungu mwenyewe na kufurahia uwepo wake milele. Waislamu wanaamini watapita juu ya daraja jembamba sana kwenda peponi. Ni jembamba sana kama unywele na wanaweza kuanguka kirahisi sana.

## Yerusalemu na Usayuni

Hii ni mada moto sana katika majadiliano na Waislamu, na **WMK** mara nyingi hushikwa kwenye njia panda. Malezi yao ya Kiislamu yamewafundisha kuwachukia Wayahudi na kupinga kwa nguvu kuhusu Usayuni. Lakini, kuwa mfuasi wa Kristo, wanapaswa kuhangaika na ufahamu wa agano la Mungu na Wayahudi katika Agano la Kale na vifungu vinavyosherehekea 'Sayuni'. Zaidi ya yotetana na fafanuzi mbalimbali za Kikristo za unabii kuhusu Wayahudi, wakiwemo baadhi ya Wakristo wanaoonekana kuunga mkono matendo yote ya taifa la sasa la Israeli na hata kuwaona Waarabu kama maadui wao. Lakini bado, **WMK** huwa na msimamo wa Israeli ya baadaye, hali hii huleta hisia ndani ya ndugu zao Waislamu kwamba wao ni wasaliti. Yote haya yanaweza kuwachanganya na kuleta hisia za maumivu kwa WMK. Hivyo, wanawezaje kuyapokea yota hayo kwa pamoja ndani ya vichwa vyao na mioyo yao? Somo hili ndilo pekee ambalo hugusa jambo hili kwa kifupi na huhitaji kuingia kwa kina sana, bali uwe makini na unyeti wake.

Katika somo la 20 kuhusu hija, majadiliano yanaweza kugeukia katika suala la Yerusalemu. Siku hizi Waarabu na Wayahudi arabu, wote wanataka kuitawala Yerusalemu. Wafuasi wa Kristo wafuate upande gani? Wakristo mbalimbali wana mtazamo tofauti kuhusu jambo hili. Baadhi ya hoja muhimu ni:

- Wafuasi wa Kristo mara zote wawe katika upande wa haki, na kutathimini sawasawa matendo ya wote, Wayahudi na Waarabu.
- Yesu alibadilisha mwelekeo wa kijiografia wakati wa swala ('*qibla*') hivyo Yerusalemu siyo kiini cha imani yetu.
- Baadhi ya Waarabu humfuata Kristo, na baadhi ya Wayahudi pia humfuata Kristo. Watu wa Kristo kutoka katika mataifa yao ni ndugu zetu wa kiroho.

# Sehemu B:

# Miongozo ya Somo

# Kikao cha Ufunguzi

| **Malengo ya kila mwanafunzi:**<br>a. Furahia kozi na ujitoe kikamilifu ili kuzifanya kazi zote za nyumbani kwa wiki hii.<br>b. Fahamu namna ya kuzifanya kazi za nyumbani kwa kila somo.<br>c. Lipia gharama za vitabu vyao au ahidi kuleta fedha wiki ijayo. | **Andaa:**<br>Pata mwongozo wa kujisomea kwa kila mwanafunzi. |
|---|---|

## *Kufungua*

**Utangulizi:** Kama hili ni kundi jipya, mwombe kila mmoja ajitambulishe. Wanaweza kusema kitu kuhusu maisha yao, kazi au familia kama inafaa. Hata hivyo, kama baadhi ya washirika hawataki kusema sana mpaka waliamini kundi, ni SAWA.

**Fungua kwa maombi:** Mwombe Mungu atusaidie sote kunufaika na kozi hii kwa pamoja.

## *Toa Maelezo kuhusu kozi hii ya Njoo Nifuate*

### "Nini?" – maudhui ya kozi

**Vitabu vya Kujisomea:** Mgawie kila mwanafunzi kitabu cha kujisomea.
*Inapendekezwa walipe kitu kidogo kwa ajili ya vitabu, maana watakithamini zaidi. Lakini ni uamuzi wako wa kuomba fedha. Kwa wale wasiojua kusoma au wanaosoma polepole, ona sehemu ya wanafunzi wa mdomo katika sehemu ya 'Maswali yaulizwayo mara kwa mara' katika Sehemu A ya Mwongozo kwa Mshauri.*

**Fungua kitabu cha kujisomea katika ukrasa wa v:** Yaliyomo.
- Mwombe mshirika mmoja asome orodha ya mada hizo.
- Waombe washirika wakae wawili wawili na washirikishane ni masomo yapi wangependelea zaidi, na ni kwa nini? Kisha wawashirikishe kundi lote.

### "Kwa nini?" – kusudi la kozi

**Kusudi la Kozi:**
- Kusudi la kozi hii ni kutusaidia kukua kama wafuasi wa Kristo.
- Sisi sote ni wanafunzi kwa pamoja, mimi na wewe pia. Kwa pamoja tunataka kumkaribia Mungu, kuweza kumjua zaidi, kumtegemea yeye, kumtii yeye na kutimiza wajibu wetu katika jumuia ya Kristo.
- Eleza: "Kundi moja la Waafugani waliosoma kozi hii pamoja walisema, 'nguvu ya kitabu hiki ni kwama kila ndugu, mkubwa au mdogo, ana fursa ya kushirikisha mawazo, maswali, matatizo na maumivu yake kwa uhuru – kadiri ya uzoefu wa maisha yao. Hiki ndicho kinachowavutia wanafunzi na kuweza kufunguka kusema wazi, na wanaweza kuomba, siyo tu kwa ajili yao wenyewe bali pia kwa ajili ya wengine".
- Uliza: "Je! Mnatarajia kujifunza kwa pamoja kama kundi hili la Waafugani?"

### "Kwa vipi?" – njia ya kozi

**Fungua kitabu cha kujisomea katika ukrasa wa iv** na mtazame pamoja kwenye mchoro.
- Eleza: Kozi hii hutumia njia tatu kwa ujumla kwa kila wiki:
  1. **Kujisomea nyumbani** hutusaidia kukumbuka na kuyaelewa mafundisho;
  2. **Majadiliano** hutusaidia kueleza maoni yetu na kujifunza kutoka kwa wengine;
  3. **Jukumu la kutekeleza** hutusaidia kulitii somo katika maisha yetu ya kila siku.
- Nini kusudi la kila sehemu: kujisomea nyumbani, majadiliano na jukumu la kutekeleza?
  *Swali hili ni la kuwasaidia wanafunzi kuzielewa njia hizi za kujisomea.*

**Fungua kitabu cha kujisomea katika ukrasa wa vi:** Miongozi kwa ajili ya mwanafunzi.

- Kila mwanafunzi asome kwa sauti sentensi moja.
- Uliza kama kuna kitu ambacho mtu ye yote hajakielewa.

## Kulitazama somo la 1

**Fungueni pamoja somo la 1:** Kufanyika mfuasi wa Kristo (ukrasa wa 1).

- Soma paragrafu mbili za mwanzo zenye kichwa cha habari 'Kusudi la maisha yetu'. Pia soma povu lenye maneno cha maneno kinachofuata.
- Uliza kwa maneno yako mwenyewe, nini kusudi la maisha yako? *Jadili. Wanafunzi watoe maoni yao wenyewe. Wewe kama mshauri lazima uwashirikishe maoni yako.*
- Mtu mmoja asome swali la 2 kisha useme jibu. Waoneshe namna ya kupata majibu katika ukrasa wa mwisho wa kila somo.

**Kulinganisha majibu yako:**

- Kitabu ni mwalimu wako. Ndiyo maana kinakupa majibu mwishoni mwa kila somo, ili uweze kulinganisha na majibu yako mwenyewe. Hii haimaanishi kwamba basi unakili tu majibu kutoka kitabuni! Kwanza andika majibu yako mwenyewe, kasha linganisha kama umeyapata vizuri.
- Kama jibu litasema 'jibu binafsi' au 'kwa ajili ya majadiliano', hakuna jibu 'lililo sahihi' maana kila mmoja atatoa maoni yake mwenyewe au uzoefu wake.

**Maswali kwa ajili ya majadiliano:**

- Katika majibu ya Somo la 1, ni jibu gani limetolewa kwa ajili ya swali la 5 au 13? *'jibu binafsi'.*
- Je! Humaanisha kwamba maswali haya uyaache wazi bila kuandika cho chote? *Hapana haimaanishi hivyo! Kila mshirika lazima aandike majibu yake mwenyewe na awe tayari kuzungumzia katika kipindi cha majadiliano. Mara kwa mara wanafunzi huwa wanaacha kuandika majibu yao binafsi, ndiyo maana tunasisitiza sana.*
- Kwa nini ni muhimu kuandika majibu binafsi kwa maswali kama hayo, na siyo kuyaacha wazi?" *Tunapoandika kitu fulani, hutufanya tufikiri kwa kina kuhusu kitu hicho. Na tutakikumbuka vizuri zaidi. Pia, tunakuwa na kitu kilicho tayari kwa kuwashirikisha wengine wakati wa majadiliano*

## Kujisomea nyumbani

**Kukamilisha somo la katibu cha kujisomea kila wiki:**

- Kabla ya kikao chetu kijacho, tafadhali kamilisha Somo lote la 1 kwa muda wako.
- Mwishoni, tafadhali fanya Marudio ya Somo. Maswali ya kwenye Marudio ya Somo ni muhtasari wa yale uliyokwisha kuyajibu katika somo husika. Kwa hiyo, hatujakupa majibu. Kama hujui majibu yake, rudia tena somo.

<table>
<tr><th colspan="2">Mwisho</th></tr>
<tr><td>Kumaliza kikao cha ufunguzi:<br>• Uliza kama kuna mtu ana maswali zaidi.<br>• Eleza muda na mahali kwa ajili ya kikao kijacho.<br>• Wakumbushe wanafunzi kupitia somo la 1 la mwongozo wa kujisomea kabla ya kikao kijacho.</td><td>O)mbeni pamoja:<br>Mwombe Mungu aseme na kila mmoja wetu wiki hii kadiri tunavyoianza kozi hii mpya.</td></tr>
</table>

# Somo la 1: Kufanyika Mfuasi wa Kristo

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. Kuzingatia kama ni mfuasi wa Kristo au la.
b. Kama bado kuwa mfuasi wa Kristo, kujua namna ya kufanya hivyo.
c. Kariri Mathayo 11:28.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Mahali pa kuanzia na WMK
- Waamini wapya na kuhesabu gharama

**Andaa:** video ya hiari kwa ajili la 15-18.

## Kufungua

**Omba kwa ajili ya somo la leo.**
**Somo la 1 marudio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** Fanyeni mazoezi ya kusema kwa pamoja mstari au aya ya kukariri (Mat. 11:28). Kwa kuisoma ayah ii, unajisikiaje?
**Swali la 2:** Waulize wanafunzi wameandika nini kwenye vitabu vyao.
*Wanaweza kujibu kwa zamu. Au wanaweza kubadilishana vitabu na kusahihisha majibu ya wengine.*

**Tambulisha mada ya leo:** Leo tunajifunza namna Yesu Kristo alivyomwita Simoni Petro kufanyika mfuasi wake, na namna ambavyo hata sisi tunaweza kufanyika wafuasiwa Kristo.

*Eleza kwamba hakuna muda wa kutosha kujadili kila swali. Lakini watie moyo watu kuuliza kuhusu swali lo lote unaloliacha kama hawakuelewa, na pia ruhusu waulize maswali mengine kadiri mnavyoendelea.*

## Majadiliano

### Utangulizi (na Swali la 1-2)

**Utangulizi:**
Omba watu wawili wasome mitazamo ya watu hao wawili kuhusu kusudi la maisha. Uliza swali la mwalimu lililomo kwenye povu lenye maneno.
- Nini kusudi la maisha yako?

  *Washirikishe kusudi la maisha yako mwishoni kabisa.*



### Kufanyika mfuasi wa Yesu (Swali la 3-4)

**Swali la 3:** Someni pamoja kifungu kilichomo ndani ya kisanduku. Uliza:
- Mtu mmoja asimulie tukio hilo kwa maneno yake mwenyewe.
- Waza kwamba wewe ni Simoni. Unapata hisia gani tofauti ulipomwona Yesu akifanya muujiza huu?
- Ni hatua nne zipi ambazo Simoni Petro alizipitia ili kufanyika mfuasi wa Yesu?

*Wengine wanaweza kujaza nafasi yo yote iliyo wazi. Yawezekana: alistaajabu nguvu yake. Mwenye dhambi mbele zake. Alipata fursa ya kuitwa.*
*1. Kugeuka kuiacha dhambi. 2. Kuifahamu gharama. 3. Kujitoa mwenyewe kwa ajili ya Kristo. 4. Kujiunga na jumuia ya Kristo.*

### Hatua ya kwanza: Kugeuka kuiacha dhambi (swali la 5-11)

**Swali la 8-10:** Soma paragrafu ya kwanza ya swali la 8 na tazama nyongeza ya 2.
Omba watu wawili wasome maneno ya Imrani na Shafiki. Ni yupi ambaye Yesu atamsafisha? Kwa nini?
- Hebu kila mmoja wetu ajifikirie mwenyewe. Je! Tuko kama Imrani au Shafiki?
- Nini tofauti kati ya kusikitika tu na toba ya kweli?
- Kama Shafiki ameonesha toba ya kweli, tutajuaje?

*Kama kuna muda, unaweza kuwaomba wanafunzi kuelezea nyongeza ya 2 kila mmoja na mwenzake.*
*Shafiki, kwa sababu anajua anamhitaji Yesu*

*Majibu binafsi.*

*Ona swali la 9. Toba ni kuelekea mwelekeo mpya kabisa, mabadiliko ya mtindo wa maisha. Mtindo wa maisha yake utabadilika.*

## Hatua ya pili: Kuifahamu gharama (Swali la 12-14)

**Swali la 12:**

- Unadhani Simoni alihisi nini alipozingatia gharama za kumfuata Yesu?
- Je! Umeshakabiliana na uamuzi kama huo katika maisha yako? Je! Bado hujafanya uamuzi?

*Kama wanafunzi wanaaminiana kila mmoja na mwenzake, wanaweza kusema kama tayari wamekwisha kumpokea Kristo au bado wanafikiria gharama.*

**Swali la 13-14:** Soma maneno ya Yesu katika kisanduku.

- Kwa maoni yako, nini maana ya habari hii?
- Umeandika majibu gani kwa swali la 13?
- Je! Gharama yote hii inafaa kumfuata Yesu?
- Uliandika jibu gani katika swali la 14?

*Kumfuata Kristo inaweza kuwa ni gharama kweli, lakini inafaa. Yeye ni wa thamani mno kuliko lulu! Inafaa kumfuata yeye.*
*Yeye alilipa gharama kubwa zaidi.*

## Hatua ya tatu: Kujitoa mwenyewe kwa ajili ya Kristo (Swali la 15-18)

**Cheza mchezo wa kuaminiana:** *shughuli hii inaweza ikafaa kwa umri Fulani na aina fulani ya watu, lakini siyo wote. Amua kama utafaa kwa wanafunzi wako. Au tazama video yake kwenye youtube kuhusu Charles Blondin,na chukua maswali hayo.*

- Wagawe wanakikundi katika vikundi vya watu wawili wawili kwa kufanana urefu na uzito, na jinsia sawa. Mtu mmoja mwangukaji na mwingine ni mkamataji. Mwangukaji asimama wima huku miguu yake ikiwa pamoja, akigeukia upande tofauti na Mkamataji. Mkamataji lazima asimame mguu mmoja mbele ya mwingine, mikono ikiwa imefunguliwa, tayari kumkamata mwangukaji.
- Mwangukaji lazima aulize kama mkamataji yuko tayari kabisa, na kisha aanze kuanguka kwa kurudi nyuma, mwili wake ukiwa imara. Mkamataji lazima awakamate salama kabla hawajaanguka sana!
- Badilisha wakamataji na waangukaji.

**Kumtegemea mkamataji:**

- Ulihisi nini ulipojitoa kwa dhati kabisa kwa huyo mkamataji?
- Kujitegemeza wenyewe kwa Yesu Kristo ni kama kujitegemeza wenyewe kwa Mkamataji. Inaweza kuogofya kwa mara ya kwanza, lakini tukigundua kwamba anatukamata kila wakati, tunajifunza kumtegemea zaidi.

**Swali la 16:** Soma mifano mitatu uliyopewa. *Mtoto aliyechoka, mgonjwa na msafiri.*

- Kwa nini watu hawa watatu wanamtegemea mwingine? *Kwa sababu wanadhani yule mtu mwingine anastahili.*
- Je! Tunaweza kumtegemea Yesu kwa njia ile ile? *Ndiyo, anaaminika zaidi kuliko binadamu ye yote.*
- Tunamtegemea atufanyie nini sisi? *K.m. kusamehe dhambi zetu, kuingia maishani mwetu, kutupatia nguvu za kutenda mema, kutulinda na kutuongoza, kutufikisha salama mbinguni.*
- Kumbuka jinsi ulivyohisi wakati wa zoezi la 'kuanguka'. Je! Unaweza kumtegemea Yesu kwa njia ile ile katika kila eneo la maisha yako? *Majibu binafsi.*

## Hatua ya nne: Kujiunga na jumuia ya Kristo (Swali la 19-20)

**Swali la 20:** Soma maelezo ya mwalimu kwenye povu lenye maneno.

- Mwalimu anaelezea aina tatu zipi za watu?
- Wewe ni nani katika watu hawa?



*Ni wale ambao tayari ni wafuasi wa Kristo, wale walio tayari kuwa wafuasi, wale wanaohitaji muda zaidi wa kufikiria.*
*Amua kama ni sawa kwa wanafunzi kuzungumza sasa au ni kufikiria tu kimyakimya.*

## *Mwisho*

**Kutii mafundisho ya leo:** Somo la leo litaleta tofauti gani kwako? **Someni kwa pamoja sehemu ya jukumu la kutekeleza.**

- Je! Una rafiki ambaye unaweza kushirikiana naye kutekeleza jukumu hili?
- Kamilisha kujisomea Somo la 2 kabla ya wiki ijayo.

**Ombeni pamoja:**
Mshukuruni Mungu kwamba tunaweza kumfahamu binafsi katika Yesu Kristo.

# Somo la 2: Maisha Mapya katika Kristo

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. Kufurahia maisha yao mapya katika Kristo.
b. Kukariri 2 Wakorintho 5:17.
c. Kufahamu kwamba tunapokea utambulisho mpya, uzao mpya na asili mpya.
d. Kujitoa kwa dhati kupigana vita vya kiroho dhidi ya asili ya kale.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Jihadi
- Mwonekano wakati wa sala

**Andaa:**
video fupi (hiari) kwa ajili ya swali la 19.

## *Kufungua*

**Ombea somo la leo. Rudia jukumu la kutekeleza la wiki iliyopita:**
- Tafadhali mtu mmoja asome Jukumu la Kutekeleza kutoka katika Somo la 1.
- Je! Ulifikiria kwa makini jambo hili? Tutalizungumzia zaidi siku ya leo katika kipindi cha majadiliano.

**Somo la 2 marudio ya kujisomea nyumbani:**

**Swali la 1:** a) mpya; b) wateule
**Swali la 2:** kale, mpya
**Swali la 3:** majibu binafsi *chunguza uone kwamba wanafunzi wote waliandika kitu kwenye vitabu vyao*
**Swali la 4:** Kristo, mpya, kale, mpya

**Tambulisha mada ya leo:** Leo tutajifunza kuhusu maisha mapya tupewayo na Bwana Yesu Kristo. Hii hujumuisha utambulisho mpya, uzao mpya na asili mpya. Hii inafurahisha!

## *Majadiliano*

### Utangulizi na Maswali (Swali la 1-4)

**Swali la 1-4:** Someni pamoja 1 Petro 1:1-2. *Kama wanafunzi bado hawajapata Biblia, andaa nakala za kifungu hicho.*

- Ni nani aliyeandika waraka huu chini ya uongozi wa Mungu? *Mtume Petro. Huyu ni Simoni Petro yule yule tuliyejifunza habari zake katika Somo la 1.*
- Ni kwa maneno gani Petro anawaelezea watu waliopokea waraka huu? *'wateule' (waliochaguliwa) bali pia 'wautawanyiko', 'watumwa na wageni', ambao hawako nyumbani hasa katika ulimwengu huu.*
- Unahisi nini kuwa mbali na nyumbani, kuwa mgeni? *Majibu binafsi. Ona swali la 3.*

### Utambulisho wetu mpya (Swali la 5-7)


**Swali la 5:** Soma swali lote.
- Je! Umewahi kuitwa mpinga dini (*kafir*) au mkengeufu (*murtadd*)? Ulihisi nini?
- Lakini utambulisho wetu mpya ni upi katika jicho la Mungu?
- Unajisikiaje kuwa "mteule wa Mungu"?

*These are common attacks on believers from this background.*

*This is wonderful, especially if our community reject us.*

### Uzao wetu mpya (Swali la 8-13)

**Swali la 8:** Tazama picha ya kiwavi na kipepeo
- Kiwavi anapokuwa kipepeo, je! Huwa ni kiumbe yule yule kama hapo awali au hubadilika ?
- Ni kwa namna gani mfano huu unafanana na uzao wetu mpya katika Yesu Kristo?



*Kwa njia moja ni ile ile, lakini imepitia aina fulani ya 'uzao mpya' hivyo sasa anaonekana wa tofauti kabisa na anaweza kupaa juu.*

*Kwa njia moja ni watu wale wale kama hapo awali, lakini mabadiliko ya kiroho ndani yetu ni makubwa mno kama kiwavi anavyofanyika kipepeo. Tofauti zitaonekana katika maisha yetu na tutaishi katika kiwango kipya cha Roho wa Mungu.*

**Swali la 11:** Soma mstari uliomo kwenye kisanduku (1 Pe 1:3)

- Ni nani awapaye uzao mpya wale wanaomfuata Kristo?
- Kwa nini anafanya hivyo?
- Uzao huu mpya hutupatia nini sisi?



*Mungu mwenyewe, Baba wa Bwaba wetu Yesu.*

*Kwa sababu ya rehema zake kuu.*

*Tumaini hai. Tunaweza kuwa na ujasiri wa maisha yetu mapya katika Kristo. Yataendelea hata baada ya kufa*

**Swali la 12:** Soma kile daktari anakisema na uombe watu watatu wasome majibu hayo matatu.

- Mfikirie daktari kuwa ni Yesu, akitoa uzao mpya kwa watu ambao ni wagonjwa kiroho.
- Mgonjwa A ni mtu wa aina gani?
- Mgonjwa B ni mtu wa aina gani?
- Mgonjwa C ni mtu wa aina gani?
- Hivyo, ni kwa namna gani tunaupokea uzao mpya wa kirho?

*A: Mtu anayemwamini Kristo lakini ana hofu ya kumfuata.*

*B: Mtu asiyemwamini Kristo hata kidogo.*

*C: Mtu anayeukubali wito wa Kristo na kumtegemea ndani ya maisha yake. Kwa kuupokea wito wa Kristo, kama mgonjwa C. Tunamwambia 'karibu maishani mwangu'. Ona swali la13*

**Swali la 13:** Soma kitufe chenye maneno. *Mkaribishe mtu ye yote ambaye hajachukua hatua hii uzungumze naye binafsi.*

## Asili yetu mpya (Swali la 14-16)

**Swali la 14-15:** Wanafunzi mbalimbali wanweza kusoma maoni yaliyomo kwenye visanduku vya maneno.

- Je! Sisi, ni kwa namna gani hisia au tabia zetu zimebadilika tangu tulipofanyika wafuasi wa Kristo? Uliandika nini katika swali la 15? *Wakumbushe wanafunzi kuandika majibu yao binafsi wakati wa kujisomea ili wawe na kitu tayari cha kushirikisha wengine. Wanafunzi wengine ambao bado hawajamfuata Kristo hawawezi kujibu swali hili lakini wanaweza kutoa maoni ya mabadiliko waliyoyaona katika maisha ya muumini.*
- Baada ya kushirikishana, au mwishoni mwa kipindi, mshukuru Mungu kwa pamoja kwa mabadiliko haya maishani mwako.

## Vita vyetu vya kiroho (Swali la 17-20)

**Swali la 17-18:** Tazama picha katika swali la 18.

- Ni watu gani wanaonesha asili yao ya kale? Ni wapi wanaoonesha asili mpya?
- Ni mambo gani ya 'asili ya kale' unayohangaika nayo?
- Soma mstari katika kisanduku katika swali la 17. Tufanye nini ili tuweze kushinda vita dhidi ya asili yetu ya kale?



*Kuvua utu wa kale, na kuvaa utu mpya – kama kubadilisha mavazi.*

**Fanyieni mazoezi kwa pamoja aya ya kukariri:** *Swali la 20 hutumia Kiswahili cha zamani*
Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya! (2 Kor. 5:17)

| ***Mwisho*** | |
|---|---|
| **Kutii mafundisho ya leo: Someni pamoja Jukumu la Kutekeleza.**<br>• Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?<br>• Endelea na kujisomea nyumbani! Ni muhimu sana kwamba uje hapa ukiwa umejiandaa kwa kila wiki kuwashirikisha wengine kile ulichojifunza. | **Ombeni pamoja:**<br>Mshukuruni Mungu kwa mabadiliko aliyoyafanya ndani yetu, na tumwombe atusaidie kupigana vita vya kiroho kila siku. |

# Somo la 3: Mungu Baba

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. Kufurahia kuzungumza na Mungu kama Baba.
b. Kuelezea kimsingi kwa nini wafuasi wa Krito humwita Yesu ni Mwana wa Mungu.
c. Kukariri 1 Yohana 3:1.
d. Kulifahamu pendo lisilo na masharti la Mungu Baba na kujaribu kuwa kielelezo cha pendo hilo kwa watoto.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Kumwita Mungu 'Baba'.
- Ukaribu na Mungu

**Andaa:**
'Barua ya baba ya upendo' video au wimbo wakati wa hitimisho.

## *Kufungua*

**Ombea somo la leo. Rudia jukumu la kutekeleza la wiki iliyopita:** Je! Ulipigana dhidi ya tabia mbaya tatu za asili ya kale? Ilikuwaje? Je! Ulihangaika? Je! Uliendelea vizuri?

**Somo la 3 marudio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** a) Baba; b) Baba **Swali la 2:** a) Kweli; b) Kweli; c) Kweli
**Swali la 3:** Tazama ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo.

**Tambulisha mada ya leo:** Waislamu hufikiri kwamba kuomba kwa Baba kama Baba ni kufuru au *shirk*! (ona 'dokezo za kitamaduni'). Lakini kwa njia ya kiroho hili linawezekana. Kama wafuasi wa Kristo, ni fursa yetu kubwa.

## *Majadiliano*

### Yesu alimwita Mungu 'Baba' (Swali la 3-9)

**Swali la 4:** Soma kifungu kilichomo kwenye kisanduku.
- Ni mara ngapi umeweka mduara kwenye neno 'Mwana' na 'Baba'?
- Kwa nini marafiki zetu wa Kiislamu hupinga majina haya Mwana na Baba?

- *Inatakiwa kuwa Mwana ni mara 4, Baba mara 3.*
- *Hufikiri kwamba Wakristo hufundisha kwamba Mungu alikuwa na mahusiano ya kimwili na mwanamke ili kuzaa motto. Lakini wazo hili ni ovu kwa Wakristo pia.*

**Swali la 6:** Tuliona jinsi Agano la Kale lilivyotumia neon 'mwana' kwa baadhi ya watu maalumu walioishi karibu na Mungu, walioonesha baadhi ya sifa zake, au kutawala kwa mamlaka yake.
- Katika kifungu hiki ni sehemu zipi zinazozungumzia Yesu Kristo kuwa karibu na Mungu Baba yake?
- Ni sehemu zipi zinazozungumzia Yesu Kristo kushiriki sifa za Mungu Baba yake?
- Ni sehemu zipi zinazungumzia Yesu Kristo kuwa na mamlaka ya Mungu Baba yake?

- *'Kwa kuwa Baba ampenda Mwana, naye humwonyesha yote ayatendayo'.*
- *'Maana yote ayatendayo yeye; ndiyo ayatendayo Mwana vile vile'. 'Maana kama vile Baba alivyo na uzima na uzima nafsini mwake, vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake'.*
- *'Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka'. 'Naye akampa amri ya kufanya hukumu'.*

**Swali la 7:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Je! Unaweza kufikiria mifano yo yote kutoka katika utamaduni wako unapomwita mtu fulani 'mwana' lakini haimaanishi hasa kuwa ni mwana wa kimwili?

**Swali la 8:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Ni madai gani Yesu aliyatoa kuonesha kwamba anashiriki asili ya Mungu kabisa?

*'Aliyeniona mimi, amemwona Baba'.*

Soma sehemu iliyobaki ya swali la 8. *Gawanyikeni watu wawili wawili. Mtu mmoja ashike uhusika wa mfuasi wa Kristo. Pata dakika tatu za kumwelezea huyo ndugu mwingine kana kwamba unamwelezea asiye Mkristo, kwa nini tunatumia jina la 'Mwana wa Mungu' kwa ajili ya Yesu Kristo. Sasa badilishaneni, hivyo wa pili sasa aelezee*

*vile vile kwa mtu yule wa kwanza.*

## Na sisi pia tunaweza kumwita Mungu Baba (Swali la 10-18)

**Swali la 11:** Soma 1 Yohana 3:1 na kisha paragrafu ya kwanza ya swali la 11.

- Tunaweza kumwita Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Jadili hatua kubwa tunayoichukua pale tunapomwita Mungu Baba yetu, kupitia kwa Kristo.
- Kwa nini tunaweza kuzungumza na Mungu kama Baba yetu kwa njia ya kiroho?

*Kwa sababu Mungu ametuasili kuwa watoto wake wa kiroho, kupitia kwa Yesu 'kaka yetu mkuu'.*

**Igundue aya ya kukariri 1 Yohana 3:1 kwa njia ya kivitendo.**

- Andika kila neon kwenye kipande tofauti cha karatasi na uvichanganye.
- Waombe wanafunzi wavipange kwa mfululizo ulio sawa na kuirudia aya hiyo kutoka kichwani.
- Kisha ondoa vipande 2 au 3 vya karatasi na rudia kuusema tena.
- Endelea hivyo mpaka mwanafunzi aweze kuisema aya yote bila kutumia karatasi yo yote.

**Swali la 12:** Soma swali lote.

- Nini tofauti ya upendo wa baba zetu wa kimwili na upendo wa Baba yetu wa mbinguni?
- Je! Mungu anatupenda wakati wote, au pale tu tunapokuwa wema?
- Je! Tuwapende watoto wetu wakati wote, au pale tu wanapokuwa wema?

*Baba zetu wa kimwili wanaweza kutupenda kulingana na mafanikio yetu, bali Baba yetu wa mbinguni hutupenda kama tulivyo.*
*Mara zote.*
*Mara zote.*

**Swali la 13a:** Hakuna aliye na mahusiano kamili na baba zao wa kidunia.

- Je! Unataka kusema namna baba yako wa kimwili alivyokuwa wakati unakua?

*Watie moyo watu waweze kusema, lakini uwe makini maana wengine wana kumbukumbu mbaya na wasingependa kushirikisha, au kutowaheshimu baba zao.*

**Swali la 13b:** Soma paragrafu ya pili nay a tatu ya swali la 13.

- Je! Tuna hofu kwamba Mungu anaweza kuwa kama yule baba aliyemwacha kijana wake akaanguka chini?

*Ruhusu wanafunzi waelezee wazi hofu zao. Kasha wahakikishie kwamba Mungu kamwe hatawaacha! Ameahidi 'Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa' (Waebrania 13:5).*

**Swali la 14-15**: Soma kisanduku katika swali la 15 (Luka 15:20-24)

- Nini kilicho cha ajabu kuhusu baba katika habari ya Yesu?
- Unadhani Mungu anatufundisha nini kuhusu Mungu katika habari hii?

*Alimkaribisha kijana wake ambaye alikuwa amemletea aibu kubwa.*

*Mungu ni kama baba mkarimu. Hutukaribisha na kutusamehe hata kama tumemletea aibu kubwa sana!*

**Swali la 16:** Soma habari ya Naziri ndani ya kisanduku.

- Je! Kuna mmoja wetu aliyepata uzoefu kama wa Naziri?
- Nini tofauti kati ya baba yake Naziri na Baba yetu wa mbinguni?

*Yawezekana hawajawahi kukataliwa, lakini yawezekana itatokea baadaye baada ya familia kugundua kuhusu imani yao katika Kristo. Baba yetu wa mbinguni hatatukaa kamwe!*

**Swali la 18:** Soma swali lote. Rudia kwa pamoja ayah ii kutoka katika *Zabur* (Zaburi). **'Baba yangu na mama yangu wameniacha, Bali BWANA atanikaribisha kwake.'**

## *Mwisho*

**Kutii mafundisho ya leo:** Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako? **Someni pamoja jukumu la kutekeleza.**

- Je! Una rafiki ambaye mnaweza kushirikiana kutekeleza hilo?
- Endelea na kujisomea nyumbani!

**Tazama:** 'Barua ya upendo wa Baba' ambayo inaweza kupatikana kwenye youtube kwa lugha mbalimbali.
**Au Imba:** WImbo kuhusu upendo wa Baba.
**Ombeni pamoja:** Mshukuruni Mungu kwamba tunaweza kumtegemea zaidi kuliko baba wa kimwili na kwamba mara zote anatukaribisha hata kama wazazi wetu wa kimwili wanatukataa.

# Somo la 4: Kumtii Kristo kwa nguvu za Roho

**Malengo ya kila mwanafunzi:**
a. Kuamua kikamilifu kumtii Bwana, katika mawazo, neno na matendo.
b. Kariri 1 Petro 1:15.
c. Toa mfano unaosaidia kidogo kumwelezea Mungu kuwa utatukatikaumoja.
d. Kutamani kujazwa zaidi na zaidi Roho Mtakatifu.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Utatu Mtakatifu, Dhabihu na agano
- Uanafnzi katika fikra ya Kisufi
- Waislamu, Roho Mtakatifu & Gabrieli

**Maandalizi:** Kwa maonesho: Bilauli, sahani au bakuri, vijiwe vidogovidogo vichafu, jagi la maji.

## *Kufungua*

Anza kwa onesho: *Weka maji kwenye bilauli iliyojaa vijiwe vichafu.*
- Nani anataka kunywa maji yaliyomo kwenye bilauli hii? Kwa nini siyo? Tutajalidili hili baadaye. *Iweke bilauli hiyo chafu pembeni kwa ajili ya baadaye. Weka maji kwenye bilauli safi kwa ajili ya wote.*

**Ombea somo la wiki hii. Rudia jukumu la kutekeleza la wiki iliyopita:** Ni njia zipi ulifikiria kuzitumia kuonesha pendo lisilo na masharti kwa watoto? Ulitekelezaje kwa vitendo?

**Somo la 4 marudio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** a), b), c) na d) yote ni sawa Swali la **2:** b) **Swali la 3:** bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote. (1 Petro 1:15) **Swali la 4:** b)

**Tambulisha mada ya leo:**
Tutajifunza namna Bwana Yesu na Roho wake wanavyofanya kazi katika maisha yetu. Pia tutajaribu kujifunza kitu fulani kuhusu namna Baba, Mwana na Roho Mtakatifu walivyo pamoja kuwa ni Mungu mmoja wa kweli.

## *Majadiliano*

### Kazi ya Kristo katika maisha yetu (Swali la 2-6)

**Swali la 4:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Neno 'agano' lina maana gani?
- Ni kwa namna gani Mungu alitengeneza dhamana hii kwetu?
- Kama tuna dhamana na Mungu kuwa ni watu wake hii humaanisha nini kwetu?

*Agano ni kujitoa kwa dhati au dhamana ambayo haipaswi kuvunjwa. (ona swali la 3)*
*Kupitia dhamana ya Kristo kumwaga damu yake msalabani kwa ajili yetu.*
*Haivunja dhamana hiyo upande wake, hata sisi hatupaswi kuivunja upande wetu. Sisi ni wateule wake.*

- Soma paragrafu ya pili ukianza naa 'dhamana hii…'
  - Sentensi hii ina maana gani kwetu?

*Kujitoa kwetu kwa dhati kwa Yesu lazima kuwe imara kuliko mwanafunzi wa mtu ye yote mtakatifu, maana Kristo amefanya zaidi kwa ajili yetu kuliko mtu ye yote mtakatifu!*

**Swali la 5:** Tazama picha hizo tatu.
- Unadhani ipi ni muhimu zaidi: kumtii Bwana Yesu kwa matendo yetu, au maneno yetu au mawazo yetu? *Yote matatu ni muhimu sana na lazima tusipuuze hata moja wapo!*
- Ni kwa namna gani Kristo amekusaidi kumtii yeye katika mawazo, maneno na matendo?

### Kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha yetu (Swali la 7-12)

**Swali la 8:** Soma paragrafu ya pili.
- Kulingana na mafundisho ya Biblia, Roho Mtakatifu ni nani?
- Tangu umekuwa mfuasi wa Kristo, je! Uwepo wa Mungu ni dhahiri maishani mwako kuliko hapo awali? Tafadhari shirikisha uzoefu wako.

*Uwepo binafsi wa Mungu, uko hai ulimwenguni na hasa kwa wafuasi wa Kristo.*

**Swali la 11:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Umetoa jibu gani katika sehemu a) na kwa nini?
- Umetoa jibu gani katika sehemu b) na kwa nini?
- Ni kwa namna gani mifano ya somo hili ni msaada kwako?

*a) Kisayansi, bila miare au joto tusingeweza kuliona au kulihisi jua kabisa.*
*b) Kama Mungu asingemtuma Mwanawe, tusingejua yukoje. Kama asingemtuma Roho wake, tusingepata uzoefu wake binafsi katika maisha yetu.*

**Kupata uzoefu wa Utatu Mtakatifu:** Soma 1 Petro 1:2-9. *Aya hizi zinaonesha namna tunavyoweza kupata uzoefu wa Mungu kama Utatu Mtakatifu hata kama hatumfahamu kikamilifu.*

- **Katika aya ya** 2 & 3, Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho wametutendea sisi?
- Katika aya ya 5, ni nini kinachotukinga sisi wakati wa maisha yetu hapa duniani?
- Katika aya ya 6, tuitikieje wakati wa majaribu?
- Ingawa hatuwezi kumwona Mungu au kufahamu kikamilifu kama Utatu Mtakatifu, tunajisikiaje kwake? (aya ya 8-9)

*Baba: alitujua tangu zamani, alituchagua, alitupa uzao mpya. Damu ya Yesu inatunyunyiza. Roho wake hutufanya watakatifu (hututakasa), kwa ajili ya kumtii Mwana.*
*Nguvu ya Mungu.*
*Tunapaswa kufurahi.*

*Tunampenda, tunamwamini, tunajazwa na furaha yake isiyoelezeka ya utukufu, tunapokea wokovu wa roho zetu.*

**Swali la 12:** Soma paragrafu ya kwanza ukijumuisha hoja zenye buleti.

- Mpaka sasa, ni mambo gani katika orodha hii Roho Mtakatifu amekuwezesha kuyafanya?
- Je! Ni muhimu au hiari kwa Roho wa Mungu kuwa hai katika maisha yetu?

## Roho Mtakatifu hutufanya watakatifu (Swali la 13-16)

**Endelea na onesho:** *Chukua bilauli yenye mawe, sema:*

- Hakuna mtu anayetaka kunywa maji haya machafu! Kama bilauli hii, kama maisha yetu yamejaa dhambi na aibu kama mawe haya machafu, tunahitaji kusafishwa.
- Tunaweza kufanya nini ili bilauli hii iwe safi? *Kuyaondoa mawe, kuisafisha bilauli kwa maji safi- onesha kwa kuyaondoa mawe na kumimina maji safi ndani ya kikombe mpaka kijae.*

**Swali la 14:** Soma swali lote.

- Unadhani kuwa mtakatifu ina maana gani? Toa mifano.

*Kuwa mtakatifu ni kuwa kama Mungu! Mawazo yetu ni masafi, tunawajenga wengine, hatufanye maovu, n.k.*

**Swali la 15:**

- Tunatarajia kiwango ganir?
- Inawezekana wanadamu kuwa watakatifu kama Mungu
- Kutokana na kile tulichokisoma hapo awali, ni nani anayetufanya tuwe watakatifu?

*Kiwango cha Mungu– Tunapaswa kuwa watakatifu maana yeye ni Mtakatifu.*
*Hapana, haiwezekani kwa juhudi zetu wenyewe. Katika dini nyingi, watu hao wanaojitahidi sana kuwa watakatifu huwa ndio watu wanaokata tamaa sana wanapoanguka.*
*Roho wa Mungu ambaye ni mtakatifu hutufanya sisi kuwa watakatifu, (aya ya 2). Kama maji masafi ambavyo yanaweza kusafisha kibaluli iliyochafuka, tunasafishwa kwa Roho wake.*

**Swali la 16:** Kariri aya iliyomo kwenye kisanduku (1 Petro 1:15) na omba pamoja huku ukiwa umeinua juu mikono, ukimwobma Mungu akujaze Roho Mtakatifu.

## Roho Mtakatifu huyajaza maisha yetu (Swali la 17-20)

**Swali la 20:** Soma swali lote la 20. *Toa kielelezo cha paragrafu hii kwa kutumia bilauli na maji. Tumia jagi la maji na bilauli, pamoja na bakuli au sahani chini yake ili maji yasimwagike chini.*

Mungu hutujaza Roho wake kadiri tuombavyo na kuishi karibu naye kila siku. Wakati mwingine huwa tunajazwa kwa ghafla, wakati mwingine huwa ni polepole. Amri yake ni kuendelea kujazwa. Tuendelee kujazwa zaidi na zaidi kila siku!

## *Mwisho*

**Kutii mafundisho ya leo:**

- Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?
- **Someni pamoja sehemu ya Tekeleza Jukumu.**
- Kama una Biblia au Agano Jipya, njoo nayo wiki ijayo.

*Kama inawezekana, wasaidie wanafunzi wasio na Biblia au Agano Jipya kupata moja. Biblia ya kawaida au kwa lugha yao wenyewe.*

**Ombeni pamoja:** Sasa ni muda wa kuungama mbele za Mungu "uchafu" wo wote ambao unatuchafua sisi. *Ruhusu muda wa ukimya kwa watu kufanya hivyo wao wenyewe. Unaweza kutumia mawe kama kielelezo.* Tumwombe Mungu atupe Roho Mtakatifu atusafishe, atufanye watakatifu na kutujaza kila siku hadi kumwagikia.

# Somo la 5: Kuzungumza na Mungu

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. Kuweza kuzungumza na Mungu wakati wote kila siku.
b. Kufahamu kwamba maombi ni kuzungumza na Mungu, na siyo utamaduni tu.
c. Kujifunza kwamba maombi huhusisha toba, shukrani na kuomba mahitaji.
d. Kukariri sala ya Bwana.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Theoloia ya maombi / Tafakuri ya Kisufi
- Waislamu, maombi na usafi wa '*wudu*'
- Kuandaa orodha ya maombi

**Andaa:** Vichwa vya habari kwa ajili ya shughuli (# 14), karatasi au kadi, kalamu, mikasi, na gundi.

## *Kufungua*

**Omba pamoja. Rudia sehemu ya Tekeleza Jukumu ya wiki iliyopita:** Je! Ulimwomba Mungu kila siku ili akujaze Roho Mtakatifu? Ulimwonaje Roho Mtakatifu akitenda kazi maishani mwako kila siku?

**Rudia aya ya kukariri ya wiki iliyopita (1 Petro 1:15):** Mwombe kila mmoja airudie aya hiyo.

**Somo la 5 marudio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1**: a) **Swali la 2:** kuomba msamaha, kushukuru, kusihi. *Kwa mpangilio wo wote.*
**Swali la 3:** omba bila kukoma **Swali la 4:** Sala ya Bwana kama ilivyo katika Swali la 14.

**Tambulisha mada ya leo:** Tazama picha katika swali la 1. Mungu ni kama Mfalme mkuu. Kwa nini anatusikiliza? *Kwa sababu yeye ni Baba yetu wa mbinguni anayependa kusikiliza watoto wake!*

## *Majadiliano*

### Kuzungumza na Mungu kama Baba (Swali la 2-5)

**Swali la 3:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Kwa nini hatuhitaji maombezi ya watu watakatifu ili kutuleta karibu na Mungu?

*Sisi ni watoto wa kiroho wa Mungu, hivyo sisi wenyewe tuna haki ya kumkaribi yeye!*

**Swali la 4:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Umeweka alama ya vema kwenye moja ya majibu gani haya? *Tunaweza kuzungumza na Mungu kwa kila kitu!*
- Unaona ni mambo gani ni vigumu kuzungumza na Mungu? Kwa nini?

### Maombi ya kitamaduni na yale ya binafsi (Swali la 6-10)

**Swali la 9:**
- Ni kwa sababu gani watu hufanya maombi ya kitamaduni? Kwa nini wanafanya maombi ya kawaida?
- Motisha wetu uwe ni nini katika maombi?

- *k.v. mara kwa mara watu hufanya 'salah' (maombi ya kitamaduni) ili kupata thawabu, au hufanya 'dua' (maombi ya kawaida) kukidhi hitaji.*
- *Kumkaribia Mungu na kuishi katika ukaribu wake.*

**Swali la 10:** Soma paragrafu ya kwanza na kisanduku (1 Petro 1:8).
- Je! Umeshawahi kupata uzoefu huu wa 'furaha isiyoelezeka na yenye utukufu'? Eleza ulijisikiaje.
- Baadhi ya watu hujaribu kupata uzoefu huu wa ukaribu na Mungu kwa njia ya kiwimbo (*dhikr* au *zikr*) lakini tunaufikiaje moyo wa Mungu? *Kwa njia ya Yesu Kristo mwenyewe. Yeye ndiye njia ya kuufikia moyo wa Baba yetu!*

### Omba bila kukoma (Swali la 11-13)

**Swali la 12-13:**
- 1 Wathesalonike 5:17 inatuamuru tufanye nini? *Lazima tuombe kila kukoma.*
- Hii inawezekanaje kwa vitendo? *k.v. Kwa Roho wake tunaweza kumkaribia*

- Kutokana na orodha ya swali la 13, umechagua uamuzi gani?
- Uchaguzi wa mwisho ulioorodheshwa ni 'kabla ya chakula'. Kama hali yako inaruhusu, je! Umeifanya hiyo kuwa tabia yako?
- Soma povu lenye maneno mwishoni mwa swali la 13.

*Mungu wakati wote, ona nukuu katika swali la 13. Au mfano kutoka katika maisha ya wanafunzi.*
*Ni tabia njema kuianzisha. Wanafunzi waishio na Waislamu wanaweza wasipate fursa, lakini baadhi yao wanaweza kufanya hivyo kama ushuhuda.*

## Sala ya Bwana (Swali la 14-15)

**Kujifunza Sala ya Bwana:** kuna wakati wanafunzi walimwuliza Yesu: "Tufundishe namna ya kusali". Aliwafundisha Sala ya Bwana. *Mwombe mmoja asome kwa sauti Mathayo 6:9-13 kwa lugha ya kila mwanafunzi. Kisha wanafunzi waiandike kila sentensi ya sala hii katika karatasi kwa kila lugha ya mwanafunzi. Changanya karatasi hizo mezani (siyo chini!) na waombe wanafunzi wazipangilie katika mpangilio sahihi.*
Kama washiriki wako ni watafutaji wa hifadhi, mamlaka zinaweza kuwaomba waiseme sala ya Bwana wakati mchakato wa hifadhi yao unafanyika, hivyo ni muhimu wajifunze na waifahamu kutoka moyoni.

- Je! Tunapata thawabu yo yote ya kidini tunaposema sala ya Bwana? Kama tukiirudia kuisema mara kumi badala ya mara moja, hiyo itatuongezea thawabu?

*Hapana! Bwaba Yesu alisema,'Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi' (Mat. 6:7).*

- Unadhani ni lugha gani iliyo nzuri zaidi kutumia wakati wa maombi, Kiingereza, Kiarabu au lugha yako mwenyewe?

*Baadhi husema Kiarabu ni kizuri zaidi. Lakini tunaweza kutoa shukrani zetu na mahitaji yetu kwa baba yetu kwa uhuru kabisa kwa kutumia lugha ya mama.*

## Kuomba msamaha, kushukuru na kuomba mahitaji (Swali la 16-22)

**Swali la 15:** Sala ya Bwana inahusisha aina 3 za maombi: kuomba msamaha, kushukuru na kuomba mahitaji. *Waombe wanafunzi kuchambua kila sentensi ya sala ya Bwana kwa kufuata makundi hayo 3. Unaweza kuzibandika ukutani au kuzitandaza mezani.*

**Swali la 17:** Soma swali lote.

- Tunawezaje kuwa na uhakika wa kwamba Mungu anaweza kutusamehe na kutusafisha tunapomwomba msamaha?

*Kwa sababu anaahidi hivyo. 1 Yohana 1:9 inasema 'Kama tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.'*

**Swali la 20:** Kwa pamoja, soma Mathayo 7:7-11 kutoka katika Biblia.

- Katika aya ya 7, Yesu Kristo anatoa amri gani?
- Katika aya ya 7, Yesu Kristo anatoa ahadi gani?
- Yesu anatoa hoja gani katika aya ya 9-11?
- Toa mfano wa namna Mungu alivyojibu maombi yako.
- Hivyo, kwa nini hatupokei kile tunachokitaka pale tunapoomba?

*Wanafunzi wanaweza kuhitaji msaada wa namna wa kukipata kifungu hiki. Somo la 6 huelezea namna ya kutafuta aya za Biblia. Omba, tafuta, na bisha. Utapewa, utapata, mlango utafunguliw. Ahadi hizi zimerudiwa katika aya ya 8. - Baba yetu wa mbinguni ni mwema, na anapenda kuwapa watoto wake vitu vizuri. Wakati mwingine kile tunachokiomba siyo kizuri kwetu. Hivyo mtoto akiomba nyoka baba mwenye upendo atampa? Hapana, haiwezekani. Tusipopokea kile tulichoomba, bado tunaweza kuendelea kumtegemea Mungu akiwa Baba yetu anayetupenda. Hatuadhibu. Anajua mahitaji yetu.*

**Swali la 22:** Tunaweza kuombea mahitaji ya nani? Ni maoni gani uliyowekea vema katika swali la 22?

## *Mwisho*

**Mkazo:** Somo la leo litaleta tofauti gani maishani mwako? Utabadilishaje namna ya kuomba?
**Marudio**: **Pitia sehemu ya Tekeleza Jukumu.** Jadilini namna ya kuandaa orodha ya maombi. Watie moy waandike majina ndani ya kisanduku, kama ni salama kufanya hivyo. Unaweza kuwaambia wapakue Apu ya maombi mtandaoni kama vile 'rafiki wa maombi' ili kujaribu.

**Watie moyo**: Kuendelea kujisomea nyumbani! Kuleta Biblia zao au Agano Jipya wiki ijayo.
**Omba**: Tumia sala ya Bwana kuchochea maombi yako. Mwombe Mungu akusaidie kuishi karibu naye na 'omba bila kukoma'.

# Somo la 6: Neno la Mungu Kwetu

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. Kuanza mazoea ya kutenga muda na Mungu kila siku.
b. Kujifunza hatua tatu za kutumia katika kipindi hicho na Mungu.
c. Kuweza kupata marejeo kutoka katika Biblia.
d. Kuwa na hamu ya kusoma Biblia.

**Dokezo za Kitamaduni:**
- Waislamu na uvuvio wa Maandiko
- Hadithi
- Ufunuo wa Mungu mwenyewe

**Jiandae:** Madaftari ya kugawa kwa ajili ya kuandikia kumbukumbu (kama inawezekana, njoo na mfano wa kumbukumbu hizo). Kama wanafunzi bado hawajapata Biblia katika lugha zao wenyewe, ona uwezekano wa kuweza kupata nakala kwa njia ya kawaida au ya kidigitali.

## *Kufungua*

**Rudia shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** Je, uliisema Sala ya Bwana wiki iliyopita? *Salini Sala ya Bwana pamoja sasa. Unaweza kutumia vipande vya karatasi mlivyotumia wiki iliyopita na kusali sentensi moja kila mmoja.*

**Marudio ya kazi ya nyumbani kwa Somo la 6:** **Swali la 1:** a) Adnan; b) hudhoofika na kufa.
**Swali la 2:** 'b' ndilo jibu sahihi. Sentensi ya 'a' siyo sahihi kwa sababu inasema 'tu'
**Swali la 3:** Kale, Mpya **Swali la 4:** Jiandae; Soma; Omba

**Tambulisha mada ya leo:** Unapompenda mtu fulani, ni kwa namna gani unalionesha pendo hilo? *Mfano: unapata muda wa kutosha kukaa nao, kuzungumza nao, kuwasikiliza.* Wiki iliyopita tulijifunza namna ya kuzungumza na Mungu, leo tutajifunza namna Mungu anavyozungumza nasi kupitia neno lake, Biblia. *Mwombe mtu mmoja asome Zaburi 19:9-10.*

## *Majadiliano*

### Kiu ya Neno la Mungu (Swali la 1-5)

**Swali la 1 & 2:** Tazama picha katika swali la 1. Kisha soma mstari uliomo kwenye kisanduku.
- Je, ni kweli tuna kiu ya Neno la Mungu kama mtoto mchanga alivyo na kiu ya maziwa?

### Biblia Takatifu ni Neno la Mungu (Swali la 6-10)

**Swali la 8:** Soma swali lote. Baadhi ya watu wasio Wakristo hudhani kwamba Biblia ni kitabu cha kibinadamu. Iliandikwa na wanadamu na inazungumzia historia ya mwanadamu.
- Ni kwa namna gani tunaweza kueleza kwamba bado ni Neno la Mungu? *waandishi "waliandika maneno yake kwa njia ya Roho wake"*
- Ni kwa namna gani tunajua kwamba haijapotoshwa? *Maelfu ya miswaada ya kale inapatikana kwa watafsiri katika makumbusho – hutupatia ujasiri kwamba tunayo maandishi ya asili.*

**Swali la 10:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Kwa asili, Biblia ilitolewa kwa lugha gani?
- Je, unamfahamu aliyetafsiri Biblia katika lugha yako ya nyumbani? Je, una nakala?

Kutafsiri Biblia haimaanishi kwamba tunabadilisha maandishi ya asili. Hutusaidia kumsikia Mungu akisema nasi kwa lugha yetu wenyewe!

*Unaweza kuona ni akina nani waliotafsiri katika lugha mbalimbali kutoka katika tovuti ya Wikipedia, tafuta 'bible translations by language'.*
*Tafsiri mbalimbali za Biblia zinaweza kupatikana nchini mwako kutola katika Chama cha Biblia. Toleo la Kidigitali au sauti linaweza kupatikana katika tovuti ya www.biblegateway.com. Baadhi ya Appu (apps) za Biblia kwa ajili ya simu janja huwa na tafsiri za lugha mbalimbali/sauti. mfano 'mybible', 'Andbible', na 'bible.is'.*

### Sehemu mbalimbali za Biblia (Swali la 11-15)

**Swali la 12-14:** *Waoneshe wanafunzi kila sehemu ya Biblia kwa kutumia Biblia yako.*
- Ni sehemu ipi ya Biblia huonesha *Tawrat* (Torati – vitabu vya Musa) na *Zabur* (Zaburi)?
- Ni sehemu ipi hufahamika kuwa ni *Injil* (Injili)?
- Je, Agano Jipya lililiondoa Agano la Kale? Kwa nini siyo?

*Tawrat & Zabur = Agano la Kale.*
*Injil=Agano Jipya. Mara zote Agano Jipya huitwa Injil. Kwa maana zaidi kila kitabu cha injili ni 'Injil'.*
*Hapana, tunayahitaji yote mawili. Yote kwa pamoja ni Neno la Mungu la thamani – habari ya Mungu akiwasiliana na watu kwa njia ya historia.*

**Swali la 15:** Fungueni Biblia katila 'Orodha ya Yaliyomo'. *Kila mwanafunzi atafute kwenye Biblia yake au Agano Jipya.*

Wasaidie wanafunzi kuipata 1 Petro 1:3 & mwombe mtu mmoja asome.

- Kama tutatenga muda maalumu wa kuwa na Mungu kila siku, hutusaidia kuimarika na kuwa na afya, kama mtoto mchanga B mwanzoni mwa somo hili
- Ni kwa namna gani tunaweza kufanya hivyo kwa vitendo?

*Kama wanafunzi wana tafsiri tofauti, eleza namna maneno yanavyotofautina kidogo lakini inatusaidia kuona vipengele tofauti tofauti vya maana ya asili katika lugha ya Kiyunani.*

## Muda wa kila siku na Mungu (Swali la 16-22)

**Swali la 18:** Soma swali lote.

- Uliandika nini kwa sehemu ya a) na b)?
- Kwa muda wetu wa kila siku na Mungu, ni lazima tuchague muda na mahali ambapo patatufaa zaidi. Ni nini kitakachokusaidia kuzoea kila siku?

*Mwamobe kila mwanafunzi ajibu. Kama kuna baadhi yao hawakujibu swali hili katika vitabu vayo, wakumbushe kujaza majibu yote. Tunapofanya hivi, lazima tufikirie kuhusu maoni yetu na hivyo tunajifunza zaidi.*

**Swali la 22:** Soma paragrafu ya pili. *Mwombe kila mwanafunzi ashirikishe maoni yake.*

## Nyongeza 1: Muda wangu wa kila siku na Mungu

**Hatua ya 1: Jiandae:** Kama ulikuwa unatarajia kukutana na mfalme, ungejiandaaje? *Kuoga, kuvaa vizuri.*

- Tunajiandaaje kuja mbele za Mungu? *Waombe wanafunzi waelezee hatua ya kwanza.*

**Andaeni pamoja**: mfano. Someni sala pamoja lakini mwombe kila mmoja ataje dhambi zake binafsi mbele za Mungu.

**Hatua ya 2: Soma:** hatua ya 2 ni ipi katika muda wetu wa kila siku na Mungu? Tufanye nini katika hatua hii?

**Fanyia mazoezi Hatua ya 2 kwa kujisomea 1 Petro 1:13-15 kwa pamoja.**

- Soma kwka sauti 1 Petro 1:13-15, *kisha waombe wanafunzi wasomeane wao kwa wao.*

*Kama lugha mbalimbali zinakubalika, unaweza kuomba mtu mmoja mmoja kusoma kwa sauti kila lugha.*

- Ni mstari gani unaokugusa zaidi?
- Utafanya nini ili kuikumbuka hoja hii muhimu? *Mfano, andika kwenye daftari, kariri, n.k.* ***Gawa madaftari, onesha mfano wa kumbukumbu.***
- Utafanya nini kutii kitu hiki ambacho Mungu amesema na wewe siku ya leo?
- Hakuna mtoto mchanga atakayenyonya maziwa na kisha kuyatema! Lakini hicho ndicho tunachokifanya pale tunapolisoma Neno la Mungu na kutolitii!

*Watie moyo wanafunzi waanze kutunza kumbukumbu kwa kuandika mistari, maombi, na namna wanavyotaka kutii, n.k. Unaweza kuwagawia madaftari ili kuwasaidia watekeleze hili. Kama inawezekana waoneshe mfano wa kumbukumbu zako.*

**Hatua ya 3: Omba** hatua ya 3 ni ipi katika muda wetu wa kila siku na Mungu?

- Maombi ni kuzungumza na Baba yetu wa mbinguni. Ni mambo gani tunayoweza kuzungumza na Mungu wetu?*Ona vifungu mbalimbali vya maneno katika Hatua ya 3 ambavyo vimekolezwa wino.* ***Omba sasa kwa kutumia hatua hizi****.*
- Wiki iliyopita tulizungumzia kuhusu kuandaa orodha ya mambo ya kuombea kwa ajili ya watu wengine. Je, kuna mtu ameandaa au kutumia kwa wiki hii? Ilikwendaje? *Watie moyo wote waandike orodha, mfano; nyuma ya daftari.*
- Je, una mawazo mengine zaidi au maswali kuhusu namna ya kuwa na muda wa kila siku na Mungu?

## *Mwisho*

**Kutii fundisho la leo:** Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako? *Kila mmoja ashirikishe (hata wewe).*

- **Someni pamoja sehemu ya shughuli ya kivitendo.** Shughuli ya wiki hii ni muhimu sana. Wiki ijayo tutakuomba utushirikishe kile ulichojifunza.
- Je, una mtu ambaye unaweza kukutana naye kila mara (mfano, kwa kila wiki)?

**Ombeni kwa pamoja:** Uliza kama kuna mtu ana mahitaji maalumu wiki hii na ombeni kwa ajili ya mahitaji hayo. Mshukuru Mungu kwamba anatupenda na anataka tutumie muda wetu kuwa pamoja naye kila siku.
Omba kwamba atusaidie kupata muda mzuri wa kuwa pamoja naye.

# Somo la 7: Washiriki wa Kanisa la Kristo

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. Ujidhatiti kujiunga na jumuiya ya waumini.
b. Jifunze maelezo matatu ya Kanisa la Kristo kutoka katika 1 Petro 2.
c. Kariri 1 Petro 2:9.
d. Uwe na uwezo wa kutafuta vifungu mbalimbali katika 1 Petro.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Mawe mawili maalumu
- Kuponya utambulisho uliogawanyika
- Ummah
- Kuipima hali hatari

**Andaa:** jengo bandia, matofali ya ujenzi, tofali moja kubwa au mchanganyiko wa zege kwa ajili ya 'jiwe la msingi'. Ona utangulizi.

## *Kufungua*

**Ombea kipindi. Rudia shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** Je, ulifanikiwa kutenga muda maalumu wa kuwa pamoja na Mungu kila siku? Je, ilikusaidia kukaa karibu na Baba yako wa mbinguni? Kwa wale walioshindwa, ni vikwazo gani vilijitokeza? Ni kwa namna gani utaviepuka vikwazo hivyo kwa wiki hii?

**Somo la 7 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:**a) nyumba; b) waliochaguliwa; c) familia **Swali la 2:** Yesu Kristo
**Swawli la 3:** ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru ya ajabudarkness into his wonderful light (1 Petro 2:9).

**Tambulisha mada ya leo:** *onesha matofali ya kujengea yenye ukubwa tofauti tofauti na rangi mbalimbali.*

- Kuna mtu anayeweza kuishi katika rundo hili? Hapama – kunahitajika matofali haya yaunganishwe pamoja ili kujenga nyumba!

*Weka chini tofali kubwa au mchanganyiko wa kokoto na kwa pamoja mwanze kujenga nyumba kwa kutumia matofali mbalimbali.*

Leo tutajifunza kuhusu jumuia ya Kristo - kanisa, au jumuia ya waumini.

## *Majadiliano*

### Utangulizi (Swali la 1-2)

**Swali la 1:** Soma habari ya Majid, povu la maneno na swali la 1.

- Umefikiria nini kuhusu Majid? Uliandika nini kuhusu swali la 1? *Kuna baadhi ya nchi ambapo wafuasi wa Kristo kutoka katikaUislamu wana uhuru wa kukutana, lakini sehemu zingine inaweza kuwa ni hatari sana.*
- Soma povu la maneno la mwalimu baada ya swali la 2.

### Nyumba ya kiroho (Swali la 3-10)

**Swali la 3:** Fungua 1 Petro 2:4-8 *Omba mtu mmoja asome.*

- Katika m.5 sisi ni akina nani, mawe yaliyo hai, yaliyojengwa katika?
- Mstari wa 6 na 7 unaeleza 'jiwe kuu la pembeni'. Jiwe kuu huwekwa sehemu gani ya jengo?
- Unadhani ni nani anayeelezwa hapa kuwa ni jiwe kuu la pembeni?*Yesu Kristo, aliyechaguliwa na Mungu (m.6) na teule kwa wafuasi wake (m.7) bali hukataliwa nawaso amini (m.7) ambao watahukumiwa na yeye (m.8).*

Hakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata mahlai.
*'nyumba ya kiroho'.*
*Huwekwa chini kwenye kona na ndilo huonesha mwelekeo wa kuta zote.*
*Onesha sehemu ya kona kwenye msingi wa jengo bandia.*
*Kama inafaa kwa kikundi chako, onesha tofauti ya Jiwe letu la pembeni na lile jiwe jeusi ambalo ni nguzo ya sala la Kiislamu.*

**Swali la 6:** Soma paragrafu ya mwisho.

- Nini jibu sahihi? *b)*
- Katika mji wetu, ni mahali gani salama kwa wafuasi wa Kristo kukutana? *Jadilini mapendekezo*

*Katika baadhi ya nchi, hakuna kanisa la kitaasisi, kuna baadhi ya nchi ambako kuna sehemu nyingi za waumini kukutana. Hata hivyo, kikundi cha jumuia ya wafuasi wa Kristo kutokana na mazingira ya Kiislamu wanaweza kuchagua kukutana ndani ya nyumba, na siyo jengo la kanisa.*

**Swali la 7:** Soma paragrafu ya pili, anza na 'Bwana Yesu akawaambia wanafunzi wake…'

- Hapa leo, je, tuko angalau wawili au watatu tuliokusanyika kwa ajili ya jina la Yesu?
- Je, Kristo yuko katikati yetu kwa namna ya kipekee? *Hatuwezi kumwona, bali yuko pamoja nasi kwa Roho wake.*
- Je, umeuhisi uwepo wake pale unapokutana na waumini wengine kwa ajili ya ibada? (# 9)

## Mzao mteule (Swali la 11-18)

**Soma 1 Petro 2:9-10:** ni kifungu kipi cha maneno katika mstari wa 9 unakipenda zaidi, na kwa nini?

- Mstari wa 10 unakufanya ujisikieje? *Una maana sana kwa waumini wanaotoka katika mazingira ya Kiislamu maana huwahakikishia kwa uhakika utambulisho wao mpya katika Kristo na jumuia yake.*

**Sisi ni akina nani?** Mchezo kwa vitendo kwa ajili ya mstari wa kukariri, **1 Petro 2:9.** Mwulize mtu mmoja, *'sisi ni akina nani?' Wajibu 'mzao mteule'. Mtu huyo amwulize mtu anayefuata 'sisi ni akina nani?' na jibu lake ni 'ukuhani wa kifamle' na kuendelea. Rudia kwa kulizungukia darasa lote, mpaka kila mmoja awe na ujasiri na vifungu hivyo vya maneno.*

**Swali la 14:** Soma swali lote.

- Ni kutoka katika utaifa upi au makundi ya kijamii yapi umekutana na wafuasi wa Kristo?
- Ni nini unachokiona kuwa unafanana nao?
- Katika hali yako, je, ni vizuri kukutana na waumini wa jamii yako tu au kuwa kwenye kikundi chenye watu mchanganyiko?

*Kama yalivyo matofali haya, sisi sote ni wa tofauti, lakini sisi sote tunahitajika ili kutengeneza jumuiya ya waumini ya kiulimwengu.*
*Kuna faida za kivitendo katika yote mawili, na njia mbalimbali za kuunganisha yote mawili. Jadilini hoja hii.*

**Swali la 15:** Soma sehemu ya kwanza ya swali.

- Kulingana na mstari huu, Mungu ametuitia nini?
- Mungu ametuchagua kwa lengo gani?
- Kwa hiyo, tufanye nini?

*Kutoka gizani, kuingia nuruni.*
*'Kutangaza sifa zake', ona mstari wa 9. Tuwaambie wengine matendo makuu ya Mungu na wema wake.*

**Swali la 16:** Tazama picha hii. Wanawake hawa wenye busara wanafahamu kwamba Kristo aliwaita wawe nuru kwa niaba yake. Ni fursa gani uliyonayo ya kumwambia kila mtu kuhusu matendo makuu ya Mungu?

## Familia (Maswali 19-22)

**Swali la 22:** Soma swali. Jadilini maswali hayo kwa ujasiri.

- **Soma maneno yaliyomo kwenye kitufe cha mwalimu.** Ni kwa namana gani unaweza kujieleza na kuielezea imani yako kwa familia yako ya Kiislamu?
- Utapendelea kuwaambia 'Nimekuwa Mkristo' au 'Mimi ni mfuasi wa Yesu Masihi' au kitu kingine tu?
- Maneno haya tofauti yanaweza kumaanisha nini kwao na kwa Waislamu wenigine?

*Kama tutalitii Neno la Mungu tutakubaliana kila mmoja kuwa ni kaka na dada katika Kristo. Hatupotezi asili yetu au utambulisho wetu wa kijamii bali utambulisho wetu ndani ya Kristo unakuwa na nguvu zaidi.*
*Katika baadhi ya miktadha, neno 'Mkristo' limeambatanishwa na kileo, nguruwe, uovu wa kingono na kuwa kinyume cha Waislamu. Katika miktadha mingine, kuna ufahamu sahihi kuhusu 'Mkristo'. Biblia hutumia maneno mbalimbali kumaanisha waumini. Uchaguzi wa nembo ni jambo binafsi na hutegemea na hali yetu.*

## Je, unahitaji kanisa la Kristo? (Swali la 23-25)

**Swali la 24:** Soma swali lote. Uliandika nini hapa?

- Vipi kuhusu Majid, unadhani anaweza kupata joto kama mfuasi wa Kristo bila wengine?
- Tazama tena kile ulichoandika katika swali la 1. Baada ya siku ya leo, utampa ushauri gani huyu Majid?

**Swali la 25:** Kama tujengavyo nyumba, tunahitaji miunganiko imara ili kuwa jumuia imara ya Kristo.

- Ni kwa namna gani tunaweza kuendelea kuijenga jumuia yetu hapa?
- Ni fursa zipi zilizopo au unazoweza kuzitengeneza ili kukutana na wafuasi wengine wa Kristo?

## *Mwisho*

**Kutii mafundisho ya leo:** Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?

- **Someni pamoja shughuli ya kivitendo.**
- Je, kuna muumini mwingine yeyote unayepanga kukutana naye kwa wiki hii? *Kama mtu hana, basi anaweza kukutana na yeyote ndani ya kikundi, au kukutana na wewe.*

**Ombemo kwa pamoja:** Mshukuruni Mungu kwa ajili ya kaka na dada wengine katika Kristo na kumwomba awasaidie kuaminiana kila mmoja na mwenzake. Mwombe Mungu kwamba atujengee jumuia imara ya kiroho.

# Somo la 8: Washirika wa jumuia mbili

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. Watamani kuzitumikia jumuia zao zote mbili, ya kuzaliwa na ile jumuia ya Kristo.
b. Kuwa tayari kuwatii walio katika mamlaka, kwa ajili ya Bwana.
c. Kariri 1 Petro 2:17.

**Dokezo la kitamaduni:**
- WMK na jumuiya ya Kiislamu

**Andaa:** Karatasi, makapeni.

## *Kufungua*

**Ombeni pamoja. Rudia shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** Je, ulifanikiwa kukutana angalau na mfuasi mmoja wa Kristo? Hii ilikusaidiaje? Je, ilikupatia nguvu za kiroho?

**Somo la 8 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** a) kiroho; b) kidunia **Swali la 2:** tii
**Swali la 3:** onesha heshima sahihi kwa kila mmoja, ipende familia ya waumini (1 Petro 2:17)

**Tambulisha mada ya leo:** Sisi ni wa jumuia tofauti zipi? *(kwa mfano. familia, mahali pa kazi, mtaa, kanisa). Mwombe kila mmoja ashirikishe kuhusu jumuia yao, ziandike kwa kutumia makapeni ili uweze kuzirejea hapo mwishoni.*
Hebu leo tujadili namna sisi tulivyo wa jumuia mbili kwa wakati mmoja, na namna tunavyoweza kuzitumika zote mbili.

## *Majadiliano*

### Washirika wa jumuia mbili (Swali la 1-5)

**Soma 1 Petro 2: 11-12:** *Kila mmoja akitafute kifungu hiki.*
- Kwa nini mstari wa 11 unatuita sisi 'wapitaji na wasafiri' au kwenye tafsiri zingine ni 'wakazi wa muda'?
- Wasio-Wakristo huchunguza kwa karibu sana tabia zetu. Kulingana na mstari wa 12, tunapaswa kuishije katikati yao?

*Maana makazi yetu ya kudumu yako kwa Kristo milele, ona swali la 1.*

*Ishi maisha yenye mwenendo mzuri ili wautazamapo wautambue hata kama wanatushutumu kuwa tunatenda mabaya.*

**Swali la 2:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Ni katika jumuia mbili zipi ambazo Mungu ametuita tumtumikie?
- Kama mtu akisema, 'hatupaswi kuitumikia jumuia yetu ya hapa duniani, kilicho cha muhimu ni jumuia yetu ya kiroho', utampa jibu gani?

*Jumuia ya Kristo, & jumuia ya kidunia (au 'jumuia ya kuzaliwa') ambamo tunaishi.*

*Jadili. Kulingana na 1 Petro sura ya 2, Mungu ametuita tutumika katika jumuia zote mbili.*

**Swali la 4-5:** Soma swali la 4 b).
- Uliandika nini hapa? Shirikisha uzoefu wako.
- Kulingana na kile ulichoandika katika Swali la 5, ni njia gani nzuri ya 'kunyamazisha mazungumzo ya kupuuzi ya watu wajinga'?

*Ruhusu muda kwa kila mmoja aseme kama wako tayari.*

*Kutenda mema.*

### Kutenda mema (Swali la 6-9)

**Swali la 7:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Uliweka vema kwenye jibu gani?
- Je, unaweza kufikiria njia zingine za 'kutenda mema' kwa ajili ya jumuia yetu na taifa letu?

**Somo la 8:** Soma paragrafu ya pili.
- Uliandika wazo gani hapa?
- Kutokana na mawazo yote katika swali la 7 na 8, ni yapi unayoweza kuyaweka katika vitendo?

*Kila mwanafunzi lazima achague angalau tendo moja ambalo linaendana na hali yao.*

## Kutii serikali yetu (Swali la 10-13)

**Soma 1 Petro 2:13-17:** *Mwombe mwanafunzi asome kifungu hiki, mara moja kwa kila lugha kama kundi ni la mchanganyiko.*

- Katika mstari wa 13, Mungu anatuamuru tufanye nini? *'Tiini kila kiamriwacho na watu'.*
- Tutii kwa ajili ya nani? *'Kwa ajili ya Bwana'.*
- Kulingana na mstari wa 16, kuwa huru katika Kristo inamaanisha kwamba tunaweza kufanya cho chote tunachotaka? *Hapana, hatuko huru kufanya maovu. Badala yake sisi ni 'watumwa wa Mungu'. Tutajifunza zaidi kuhusu hili katika Somo la 15.*

**Swali la 13:** Soma swali lote.

- Uliandika nini kwa jili ya swali hili?
  *Jadili. Katika hali hiyo waumini lazima waamue ni wapi wanaweza kukubaliana kuhusu mambo yasiyo ya msingi na ni mambo yapi yaliyo ya msingi ambapo 'lazima wamtii Mungu na siyo mwanadamu' (Matendo ya Mitume 5:29).*
- Kama unafanya kazi dukani na mwajiri wako akakuambia kuwalaghai wateja, utafanya nini? Jibu kulingana na kile tulichokwisha kujifunza kutokana na mfano wa mtume Petro.
  *Jadili. Hii ni ngumu! Hatutaki tusimtii Mungu lakini hatutaki tupoteze kazi yetu pia.*

## Kuwatii waajiri wetu (Swali la 14-20)

**Soma 1 Petro 2:18**

- Mstari huu wameandikiwa akina nani? *Watumishi.*
- Kwa maoni yako, ni nini kinachoweza kuwa kigumu kutumika kama mtumwa? *Mfano. Unafanya kazi kwa bidii sana lakini hupokei kipato wala hupewi uhuru.*
- Je, watumishi katika mstari wa 18 wawatii bwana zao walio 'wema na wenye upole tu' bali nao 'walio wakali'? *Vyote viwili.*
- Kama tuna bwana ambaye siyo mwema, au watu wasiothamini kazi tunazozifanya, ni faraja gani tunayoipata kutoka katika 1 Petro 2? *Tunatii kwa ajili ya Bwana, (ms.13 & 18), ms.20: kama tutateswa kwa kutenda mema huo ni wema hasa mbele za Mungu.*
- Je, kuna mmoja wetu ambaye anapata hali hii ya kuona ugumu kumtii mtu aliye katika mamlaka? Tafadhali shirikisha. *Mwishoni tutaombea hali hizi.*

**Swali la 19:** Tazama watu hao wawili.



- Je, utapendelea kipi, kijana wako awe mkusanyaji wa uchafu mwaminifu au mhadhiri asiye mwaminifu?
- Unafiki Mungu angetaka nini?

**Fanyia mazoezi mstari wa kukariri, 1 Petro 2:17a:** *Waheshimu watu wote. Wapendeni ndugu.*

- Nani anaweza kusema kichwani 1 Petro 2:17a? *Watie moyo kila mmoja aseme.*
- Ni maneno yapi yanayotuambia kufanya sehemu yetu katika jumuia yetu ya kidunia?
- Ni maneno yapi yanayotuambia kufanya sehemu yetu katika jumuia yetu ya kiroho?

## *Mwisho*

**Kutii mafundisho ya leo:** Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako? Je, wapo walioanza kulifanyia kazi somo hili katika maisha yao?
**Soma shughuli ya kivitendo.**
**Watie moyo**: Tazama orodha ya jumuia ulizoziandika hapo mwanzo. Unaweza kuzitumikiaje? Rudi kwenye swali la 7 na 8 na chagua shughuli ya kufanya kwa ajili ya jumuia moja kwa wiki ijayo, au fanya shughuli ya kivitendo kama ilivyopendekezwa kwenye kitabu cha kujisomea.
Endelea kujisomea nyumbani!

**Omba pamoja:** *Ombeni wawili wawili au kwa vikundi kama inakubalika.*
Mwombee mwanakikundi aliye katika hali ambayo ni vigumu kutii serikali isiyotenda haki au bwana aliye mkali.
Tumwombe Mungu atusaidie kuona njia za kuweza kuzitumikia jumuia zetu za kidunia na kiroho kwa wiki hii, na kutii wale walio katika mamlaka, kwa ajili ya Kristo.

# Somo la 9: Sababu za kuteswa

| **Malengo kwa kila mwanafunzi:** | **Dokezo za kitamaduni:** |
| --- | --- |
| a. Kuhakikisha kwamba hakuna kitakachotutenga na upendo wa Mungu.<br>b. Kufahamu kwamba mateso yatatokea, bali Mungu huyatumia kwa wema wetu.<br>c. Kujifunza kutenda kwa busara ili kuepuka mateso yasiyo ya lazima.<br>d. Kariri 1 Petro 2:21. | • Kuwashauri WMK walio katika mateso<br><br>**Andaa:** vipande vya karatasi vikiwa na maneno ya Warumi 8:35 (kwa ajili ya swali la 12) |

## *Kufungua*

**Omba kwa ajili ya somo. Rudia shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** Ulifanya nini katika kuitumikia jumuia yetu au mtu mhitaji au mtu aliyeko madarakani? Huyo mtu aliitikiaje?

**Somola 9 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** kwa ajili  yenu, akawaachia kielelezo mfuate nyayo zake (1 Petro 2:21).
**Swali la 2:** 1) ulimwengu, huchukia; 2) Mungu, mateso; 3) tenda kwa ujinga; 4) nyayo za Kristo

**Tambulisha mada ya leo:** mada ya leo ni mateso, ni moja ya somo gumu sana. Yawezekana somo letu litasababisha machozi kutokana na maumivu tuliyokwisha kuyapitia. Lakini Mungu hutumia mateso kwa wema, na anaweza kuponya maumivu yetu kadiri tutakavyokuwa tukizungumzia mambo haya.

## *Majadiliano*

### Sababu ya kwanza – Ulimwengu unatuchukia (Swali la 1-6)

**Swali la 1-2:** Soma swali lote la 1 na sehemu ya kwanza ya swali la 2.

- Uliweka jibu gani katika swali la 2?  Au umeshawahi kupata uzoefu wa mateso kwa njia zingine? Je, bado unakabiliwa na mataeso?
  *Sitisha kidogo na uombe kwa ajili ya mtu ye yote ndani ya kundi anayekabiliwa na mateso sasa au bado anahisi maumivu kutokana na upinzani wa awali.*

*Hebu kila mtu azungumzie uzoefu wake. Hiki ni kipindi muhimu sana cha kushirikishana na kinaweza kuleta machozi, wahakikishie wote kwamba hiyo ni sawa.*

**Swali la 5:** Ndani ya kisanduku, soma habari ya kweli kuhusu Haim. Ni mihemuko gani unayohisi?

### Sababu ya pili – Mungu huruhusu mateso (Swali la 7-13)

**Soma 1 Petro 1:3-7**

- Kulingana na mstari wa 4, urithi wetu uko wapi?*Uko mbinguni*
- Je, 'utaangamia, utaharibika au kwisha'? *Hapana – siyo kama urithi wetu wa hapa duniani!*
- Kulingana na mstari wa 5, ni nini kinachotukinga kwa wakati huu? *Nguvu ya Mungu*
- Kulingana na mstari wa 6, pale 'tunapokabiliana na aina zote za majaribu' tuoneshe mwitikio gani? *Furaha kuu.*
- Mstari wa 7 unasema imani yetu ni kama nini*? Kama dhahabu, ambayo 'ina thamani kubwa kuliko dhahabu'.*
- Kwa nini mfua dhahabu huipitisha dhahabu kwenye moto? *kuisafisha, mfano kuibadilisha karati 9 ya dhahabu kuwa karati 24.*
- Hivyo, kwa nini Mungu huturuhusu kupita katika mateso? *Kuithibitisha imani yetu, na kutusafisha, kutufanya tuwe wavumilivu na imara. Moto wake wa kusafisha hubadilisha karati 9 za imani yetu kuwa karati za thamani 24 za imani!*

**Swali la 10:** Soma swali lote. Uliweka vema kweney jibu gani? Unajisikiaje kuhusu hili?
*Ni a) tu ndiyo jibu 'sahihi'. Hata hivyo, lengo la majadiliano haya ni kwa wanafunzi kuweza kuwa waaminifu kuhusu mashaka yao binafsi na mahangaiko yao. Kisha wanaweza kujiachilia kwa Neno la Mungu kwa uaminifu, ili Mungu aweze kubadilisha fikra zao na kuwapa nguvu za kumtumaini kwamba ni mwema hata nyakati za mateso.*

**Swali la 11:** Soma swali lote. Uliandika nini kwenye sehemu ya b)? *Shirikisha kutokana na maisha yako mwenyewe pia!*

**Swali la 12:** *Wakati wa kupita katika magumu, waumini wakati mwingine huhisi kwamba Mungu amewaacha au anawaadhibu. Zoezi lifuatalo litawapa ujasiri zaidi kwamba Mungu anawapenda na kamwe hatawaacha. Kabla ya yote, andika kwenye karatasi tofauti maneno haya 'dhiki', 'shida', 'adha', 'njaa', 'uchi', 'hatari', 'upanga'.  Pia andika kwenye karatasi zingine mbili 'nani atakayetutenga' & 'hakuna cha*

*kututenganisha' na ziweke juu ya meza au chini sakafuni. Hatimaye, andika neno 'kifo' kwenye karatasi.*

- Soma **Warumi 8:35**. Ni mambo gani yanaweza kututenga na upendo wa Kristo? Kila mtu achukue karatasi moja na aiweke chini ya kiswa kisemacho 'nani atakayetutenga' au 'hakuna cha kututenga'.
- Soma **Warumi 8:36**. Je, mstari huu unaelezea familia ya Haim kadiri walivyokabiliwa kifo kwa pamoja?
- Someni wote kwa pamoja kwa sauti moja **Warumi 8:37-39**. Je, kifo kinaweza kuitenga familia ya Haim na upendo wa Kristo? *Hapana! Walikwenda moja kwa moja kuwa na Mungu.*

Weka karatasi isemayo 'kifo' pamoja na karatasi zingine chini ya kichwa kisemacho 'hakuna cha kututenga'.

- Je, kuna kitu cha kututenga na upendo wa Kristo, cho chote kile? *Hakuna, hata kama ni kifo!*

## Sababu ya tatu – kuna wakati tunatenda kijinga (Swali la 14-17)

**Swali la 14:** Soma swali baada ya habari ya Shakeel:

- Nini maoni yako katika hili?
- Je, Shakeel alikabiliwa na mateso kwa lazima au haikuwa lazima?
- Ni kwa namna gani tunaweza kuzuia mateso yasiyo ya lazima?
- Je, tunaweza kuzuia mateso ya lazima?

***Wakumbushe wanafunzi kwamba kujisome nyumbani kunawasaidia kushiriki katika majadiliano vizuri zaidi.***
*Mfano: alitenda kijinga kwa kuleta fedheha katika familia yao, kwa kukimbia nyumbani, kumdhihaki baba yake.*

*Yasiyo ya lazima.*
*Mfano: kwa kuwaheshimu wazee wetu, kusaidia familia zetu, kujaribu kutoleta aibu kwao, kadiri inavyowezekana. Hatupaswa kulikana jina la Kristo. Lakini tunaweza kubadilisha makazi, ona swali la 17.*

**Swali la 17:** Soma paragrafu ya pili.

- Nini maoni yako kuhusu swali hili? *Jibu 'sahihi' au 'siyo sahihi' hutegemeana na mazingira. Mtu aliye katika hatari ya uhai wake anaweza kubadilisha makazi kwa muda. Hata hivyo, kama hakuna hatari wajaribu kuishi kwa utulivu nyumbani mpaka pale hali itakapokuwa imetengamaa. Wanapaswa kuthibitisha kwamba bado ni waaminifu kwa familia yao ingawa wanamfuata Yesu Kristo.*

## Sababu ya nne – tunafuata nyayo za Kristo (Swali la 18-22)

**Soma 1 Petro 2:19-21:**

- Ni kwa namna gani mstari wa 20 hueleza mateso yasiyo ya lazima?
  *'Kwa maana ni sifa gani kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makofi?'*
- Ni kwa namna gani mstari huu unaeleza kuhusu mateso yasiyo ya lazima?
  *'Lakini kustahimili mtendapo mema na kupata mateso, huu ndio wema hasa mbele za Mungu.'*
- Kama tunapaswa kustahimili mateso, ni nyayo za nani tunapaswa kuzifuata kulingana na mstari wa 21?
  *Bwana wetu Yesu alitembea katika 'njia ya miiba' na ni heshima kwetu kukanyaga kwenye nyayo zake!*

**Rudia na tafakari mstari wa kukariri 1 Petro 2:21:** *Pamoja na kujifunza mistari ya Biblia ni vizuri kuitafakari. Hii hutusaidia kusikia kile anachotuambia kupita mstari huo na namna anavyotaka tuitikie. Unaweza kuonesha wakati wa somo kwa kutumia hatua zifuatazo:*

1) Mwombe kila mmoja akabidhi moyo wake mbele za Mungu. Mwombe Mungu azungumze na sisi sote kupita neno lake.
2) Omba kila mmoja aanze kuusema mstari wa kukariri kwa sauti.
3) Kila mtu aurudie mstari kimyakimya nafsini mwake mara nyingi tu, asikilize kile Mungu anasema na kutafakari kila sehemu ya mstari huo. *Ruhusu angalau dakika 5 kwa ajili ya hili.*
4) Mwombe Mungu amwoneshe kila mmoja wenu anavyotaka mwitikie. *Ruhusu dakika chache kwa ajili ya hili.*
5) Shirikisha kwenye kikundi au mkiwa wawili kuhusu kile Mungu alisema na wewe kupitia mstari huu na namna utakavyoitikia.

# *Mwisho*

**Kutii mafundisho ya leo:**

- Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?
- **Someni kwa pamoja shughuli ya kivitendo.** Wanafunzi wanaweza kutumia mchakato uleule wa tafakari ya leo na kutafakari mstari mmoja kila siku. *Zingatia: maswali sahihi ni swali la 1,3,7,9,11,15,18,20,22 – na siyo kama ilivyo kwenye kitabu cha kujisomea cha toleo za mwaka 2013.*

**Ombeni kwa pamoja:** waombe watu wasali sala fupi, wakimshukuru Mungu kwa ahadi zake za imara wakati wa mateso. Ombea waumini walio katika adha katika nchi zingine, hasa wafuasi wa Kristo wa mazingira ya Kiislamu.

# Somo la 10: Kuitikia mateso

| | |
|---|---|
| **Malengo kwa kila mwanafunzi:**<br>a. kuamini kwa dhati kwamba msamaha ni bora kuliko kulipiza kisasi.<br>b. kuchukua hatua ya kumsamehe mtu aliyemwumiza.<br>c. Kariri Mathayo 5:44. | **Dokezo za kitamaduni:**<br>• Kulipiza kisasi na msamaha<br>**Andaa:** kwa swali la 4, andika na ukate nakala za Mathayo 5:44. |

## *Kufungua*

**Shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** Je, ulifaulu kutafakari mistari ya Biblia kila siku? Ilikuwaje kwako? Ni mstari gani uliokugusa zaidi?

**Somo la 10 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** msamaha
**Swali la 2:** mpende adui yako na ombea wale wanaowaudhi.

**Tambulisha mada ya leo:** Tazama utangulizi, watu wawili wasome maneno ya hao watu wawili: Je, umeshawahi kuhisi kama kila mmoja wa wanaume hawa? *Ruhusu wanafunzi washirikishane namna walivyohisi bila kukosoa maoni yao.* Leo tunajifunza kuhusu namna Mungu anavyotutaka tuitikie mateso, na hasa namna tunavyoweza kusamehe maadui zetu.



## *Majadiliano*

### Mduara wa kulipiza kisasi (Swali la 1-3)

**Swali la 2:** tazameni picha kwa pamoja.
- Ulizingatia mifano gani pale ulipoona mduara wa kulipiza kisasi unajitokeza?
- Kusamehe ni vigumu na kulipiza kisasi ni rahisi. Lakini ni kipi kinachoharibu zaidi?

### Msamaha badala ya kulipiza kisasi (Swali la 4-16)

**Swali la 4:**
- Yesu alitufundishaje namna ya kuuvunja mduara wa kulipiza kisasi? *Alitufundisha kupenda na kusamehe maadui zetu.*

*Andika na kata vipande vya mstari wa kukariri, Mathayo 5:44. Mwombe kila mwanafunzi avipangilie vipande hivyo kwa mpangilio sahihi.*

**Swali la 5:** Soma swali lote.
- Yesu alisali maneno gani wakati misumari ikipigiliwa viganjani mwake? *'Baba wasamehe'.*
- Je, Yesu alikuwa kiongozi dhaifu au imara? Nguvu yake ilimruhusu kufanya nini? *kusamehe*
- Tunaweza kujifunza nini kutokana na mfano wake? *Kusamehe siyo ishara ya udhaifu, bali nguvu/ujasiri.*
- Ni nani atakayetupatia nguvu ya kusamehe maadui zetu? *Yesu, kwa nguvu za Roho wake anayeishi ndani yetu.*

**Soma 1 Petro 2:21-25:**
- Kulingana na mstari wa 22, je, Yesu alistahili kuteseka? *Hapana, 'hakutenda dhambi yo yote'.*
- Tazama mstari wa 23. Badaka ya kutafuta kulipiza kisasi au kulaani watesi wake, Yesu alifanya nini?
  *Hakushindana nao, hakuwatishia. Badala yake, 'alijikabidhi kwake yeye anayehukumu kwa haki'.*
- Tazama mstari wa 24-25. Yesu Kristo amefanya nini kwa jili yetu? *Alizichukua dhambi zetu juu ya msalaba, alituponya jeraha zetu, alitukusanya tukiwa kondoo tuliotawanyika na kumrudia Mchungaji.*
- Unajisikiaje, unapokumbuka kwamba Yesu Kristo alifanya yote haya kwa ajili yako?
- Ni vigumu sana kuwapenda maadui zetu na kuwaombea wale wanaotuudhi. Hivyo kwa nini tujaribu kufanya hivyo? *Kristo alitusamehe sisi kwanza na kutuweka huru. Yeye mwenyewe aliacha kielelezo cha kuwasamehe maadui zetu. Anatuamuru kufanya hivyo. Kusamehe huvunja mduara wa kulipisa kisasi, na hutuondoa katika hali ya uchungu.*

**Kwa nini kusamehe?** *Zama kwa kina kuhusu mada hii kama muda utaruhusu.*
mkwa wawili wawili, wanafunzi lazima wasome **Mathayo 18:21-35**, jadilini kwa dakika chache na kisha mtoe mrejesho wa kile mlichojifunza katika kikundi. Kama inakubalika, waweze kusimulia au kuigiza habari hii.

**Swali la 9:** Soma sehemu ya kwanza ya habari ya Farid.

- Kama Farid angeendelea na mpango wake wa kulipiza kisasi, kungetokea nini?

*Angemruhusu shetani. Wafanyakazi wenzake wangemchukia, wangeongezeka kwenye 'mduara wa kulipiza kisasi'.*

**Swali la 10:** Soma sehemu ya pili ya habari ya Farid.

- Ni matokeo gani mazuri yalitokea kwa sababu Farid alisamehe badala ya kulipiza kisasi? *Mfanyakazi mwenzake aliguswa sana, na baadaye alifanyika mfuasi wa Yesu.*

**Soma kwa sauti kile kingine kilichotokea:** Baada ya kuandika barua ya kuomba msamaha, Farid alikwenda nyumbani kwao. Lakini bado alikuwa na wasiwasi kuhusu kupoteza mshahara wake wa mwezi mzima. Alisema, "sikuweza kupata usingizi usiku ule, nikijigeuza kitandani huku na huko mpaka nilipoamka na kuomba. Kwenye jiwe kulikuwa na barua kutoka kwa Mkristo mwingine ambaye nilikuwa sijakutana naye kwa miezi mingi kutokana na sababu za kiusalama. Barua ilikuwa na kiasi kilekile cha fedha kama mshahara wangu wa mwezi ulivyo. Nilishangaa sana: namna gani Bwana alivyo mwaminifu kwa kunijali mimi!" (www.pneumafoundation.org/pi_7_2003.jsp)

- Kama ungekuwa Farid unaipokea barua hii, ungejisikiaje? *Jadili mihemuko inayoweza kujitokeza.*

**Swali la 12:** Soma habari ya Miriam & na swali.

- Kwa nini unadhani Mungu alikidhi hitaji la kifedha la Farid kwa njia ya ajabu, na siyo Miriam?
- Ni nini kilichomfungua Miriam kutoendelea kuwachukia ndugu zake? *Alichagua kusamehe. Kisha furaha ikaujaza moyo wake!*

*Hatufahamu. Mungu anajua lililo jema kwa ajili ya kila mmja wetu na hutenda mema kwa ajili ya maisha yetu. Wakati mwingine hutuonesha muujiza ili kuimarisha imani yetu, kama alivyofanya kwa Farid. Wakati mwingine hutupitisha katika njia ngumu ili kuimarisha uvumilivu wetu, kama ilivyokuwa kwa Miriam.*

**Swali la 13:** Soma swali. Uliandika nini hapa?
*Wakati mwingine ni sawa kupinga, hasa kwa niaba ya Wakristo wengine. Wakati mwingine mtume Paulo alipinga pale alipotendewa vibaya (mfano Matendo ya Mitume 16:35-37). Lakini wakati wo wote uwe upinzani wa kisheria, siyo kulipiza kisasi.*

**Swali la 15:** Soma habari. Je, mwumini huyu aliona rahisi kuwasamehe wale waliompiga? *Hapana.*

- Alisema aliteseka sana kwa kutowasamehe watesi wake. Unadhani alimaanisha nini kwa kusema hivyo? *Yawezekana aliteseka sana kutokana na uchungu uliokuwa ndani yake.*
- Ni wakati gani umeshikwa na hasira na ukakataa kusamehe? Matokeo yake yalikuwa nini kwako?
- Kama ulimsamehe mtu huyo na kuachilia hasira, hii ilileta tofauti gani?

**Sasa soma sentensi baada ya kisanduku na maneno yaliyomo kwenye kitufe.**

- Unaweza kumfikiria mtu aliyekuumiza? Fikiria jina lake kwenye nafasi iliyoachwa wazi, na litaje kimyakimya. *Wape watu muda wa kufanya hivyo kimyakimya. Wanafunzi hawaruhusiwi kutaja kwa sauti jina au kuliandika, ni kujiepusha kuvujisha siri.*
- Je, ulifaulu kufanya hivyo? Ulihisi nini wakati wa kutamka maneno hayo?

## Furaha katika mateso yetu (Swali la 17-19)

**Soma 1 Petro 4:12-16.** *Kila mmoja afungue kifungu hiki kwenye Biblia yake.*

- Ni mstari gani uliokuvutia zaidi katika kifungu hiki, na kwa nini?
- Elezea tukio ambapo Mungu alikupa furaha katikati ya mateso.

## *Mwisho*

**Kutii mafundisho ya leo:**
Kwa wiki hii pata muda wa kumwuliza Mungu kama kuna watu unapaswa kuwasamehe. Ni vigumu na huwezi kufanya hivyo kwa nguvu zako mwenyewe. Hakuna atakayekulazimisha kusamehe, lakini ukichagua kusamehe, Mungu atakupa nguvu za kufanya hivyo. Kasha itaachilia furaha kuu ndani ya maisha yako!

**Ni nani unaweza kumwambia mada ya leo?**
Unaweza kumshirikisha mtu huyo habari ya mtumishi asiyeweza kusamehe (Mathayo 18:23-35).

**Pray together using the practical task:**
Lead learners through these steps in prayer:
**First** ask God to show us one person we need to forgive.
**Then** read steps 1 & 2 slowly.
**Omba sala** katika hatua 3 kwa pamoja, kila mmoja kimyakimya ataje jina la mtu anayetaka kumsamehe.
**Soma** kwa sauti hatua ya mwisho.
Tuombeane sisi kwa sisi ili tupate nguvu ya kusamehe kwa njia hii.

# Somo la 11: Waume na Wake

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. kuufahamu mpango wa Mungu kuhusu ndoa: mwanamume mmoja aliyeungana na mwanamke mmoja kwa maisha yao yote.
b. kutaka kuwafurahisha wenzi wao zao yao wenyewe.
c. Kuamini kwamba waume lazima wawape kipaumbele wake zao kuliko mama zao.
d. Kariri Mwanzo 2:24.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Ndoa katika Uislamu
- Umama katika Uislamu

**Andaa:** karatasi na kalamu, zingatia mambo ya kujadili kwa ajili ya swali la 3.

## *Kufungua*

**Shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** je, uliweza kumsamehe mtu aliyekuwa amekuudhi? Hiyo ilileta tofauti gani katika maisha yako? *Zungumza kwa faragha na wale wote ambao hawazungumzi au wanaona kusamehe ni vigumu.*

**Somo la 11 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** atawaacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja (Mwanzo 2:24). **Swali la 2:** moja, moja, yote **Swali la 3:**a) tii; b) anayezingatia **Swali la 4:** I

**Ombea somo la leo, tambulisha mada ya leo:** Mahusiano yetu na wenzi wetu ni mahusiano muhimu sana tuliyonayo ya kibinadamu, hata zaidi ya wazazi wetu. Mada yetu ya leo ni mpango wa Mungu kuhusu ndoa. ***Ni muhimu sana kulipokea somo la leo, mfano, kama wanafunzi wako hawajaoa au kuolewa.*** *Tunapendekeza majadiliano yafanyike kwa kundi lenye jinsia moja, kukiwa na kiongozi wa jinsia hiyo. Lenga maswali ambayo yanahusiana na wanafunzi wako. Mada hii ni muhimu sana, hivyo usiwe na haraka, na rudia tena kama kuna uhitaji huo.*

## *Majadiliano*

### Mpango wa Mungu kuhusu ndoa (Swali la 1-11)

**Swali la 2:** soma kila usemi na uulize:
- Je, wewe binafsi unakubaliana na usemi huu?
- Kwa nini au kwa nini siyo?

*Majibu haya yanatokana na mtazamo wa kibiblia, kuzingatia fundisho la mwamume na mwanamke wameumbwa kwa sura ya Mungu, lakini mitazamo ya Kikristo inaweza kutofautiana kutokana na vipengele vya majukumu ya kijinsia.*

**Swali la 3:** Rudia mstari wa kukariri, Mwanzo 2:24.
- Mungu ana mpango gani kuhusu ndoa? *Ona swalli.*
- Nini kinapaswa kutokea kati yao, kimwili, kiakili na kiroho? *Wanapaswa kuungana – kuwa mwili mmoja.*
- Katika utamaduni tunamoishi, ndoa huanza lini na kwa namna gani?
- Kwa Wakristo inapaswa kuwa tofauti kwa namna gani? *Pata muda wa kujadili mambo na changamoto pale unapoishi, kwa mfano, Huko magharibi: namna ya kupata mchumba, kuchumbiana, kuishi pamoja, tendo la ndoa kabla ya kufunga ndoa, harusi. Weka wazi ni tofauti zipi zinapaswa kuonekana kwa Wakristo.*

**Swali la 5:**
Tazama picha.
- Kila mmoja wenu aliandika nini katika swali la 5 a) , b)?



*Hiki ni kisa ambacho wanafunzi watakitambua. Kanuni ya kibiblia iko wazi kwamba mke lazima aje kwanza, lakini kuwajali na kuwaheshimu wazazi ni kanuni ya kibiblia ambayo haisisitizwi sana katika nchi za magharibi.* ***Soma swali la 4 kwa pamoja.***

*Jadilini mada inayofuata, kuachana, fundisha neema ya Mungu kwa makini na msamaha kwa waumini ambao wamepitia katika hali ya kuachana au kutalakiana na wenzi wao.*

**Swali la 7:** Soma Mathayo 19:3-6.



- Ilikuwa rahisi siku hizo kwa mwanamume kumwacha mke wake. Kristo ananukuu nini katika mstari wa 5?
- Ni kwa namna gani mume na mke wanaweza kuimarisha ndoa yao, siyo kimwili tu bali pia kwa mioyo na akili zao?
- Katika mstari wa 6, je, Kristo anasema kwamba ndoa ni mkataba wa kibinadamu, au ni kitu kikubwa zaidi?

*Kweli, baadhi ya Mafarisayo walifundisha kwamba mwanamume anaweza kumwacha mke wake kama ataunguza chakula!*
*Mwanzo 2:24.*
*Pata muda wa kuwa pamoja, zungumzeni kila mmoja na mwenzake na fanyeni mambo kwa pamoja, kama marafiki wa kweli.*
*Uislamu hufundisha wazo la ndoa kuwa ni mkataba lakini Biblia inasema ni vigumu kuuvunja.*
*Mungu 'alichokiunganisha' hivyo mwanadamu*

- Kuingana na maneno ya Kristo katika mstari wa 6, kwa nini kuachana ni vibaya?

*asikitenganishe (ona pia mstari wa 9). Hata hivyo, wakati mwingine ndoa hushindikana hata kwa wafuasi wa Kristo.*

**Swali la 9:** Soma swali. Uliweka vema kwenye jibu gani? Kwa nini unadhani hii hutokea?
*a), b) na d) ni kawaida kwa jamii za Kiislamu. Kuna visa vichache sana kuhusu c).*

**Swali la 10:** Soma kitufe chenye maneno na ile paragrafu ya mwisho. Uliandika nini hapa?
*Mume huyu anadhani mke wake ni kama mali, lakini Biblia inafundisha wanaume na wanawake wana thamani sawa.*

**Swali la 11:** Soma swali lote. Ni kwa namna gani inatusaidia kufahamu kwamba Mungu anahisi maumivu yetu? - *Yawezekana wanafunzi wako wako katika hali hii isiyo ya furaha. Inawasaidia kufahamu kwamba Yesu Kristo hapa duniani alihisi mfadhaiko mkubwa kwa ajili ya watu wanaoteseka na anahisi maumivu yetu kama hatuna furaha katika ndoa zetu.*

## Waume na Wake katika 1 Petro (Swali la 12-22)

**Swali la 13:** Soma swali lote.
- Kwa nini kuna wakati inakuwa ni vigumu kwa mke kumtii mume wake?
- Kwa nini kuna wakati mume inakuwa ni vigumu kumzingatia mke wake?

*Mfano: mume anaweza kuwa mbinafsi, bwana au asiye na hekima; au mke anaweza kutaka njia yake mwenyewe.*
*Mfano: waume walio wengi hutarajia wake zao wawatumikie.*

**Swai la 15 & 20:** Omba watu wawili wasome kwa sauti kile mke (swali la 15) na Tariq (swali la 20) wanasema.
- Wanajaribu kumfurahisha nani – wao wenyewe au wenzi wao?
- Mungu anataka kujali nini zaidi: ni kwa namna gani tunaweza kuwafurahisha wenzi wetu au yeye anawezaje kutufurahisha sisi? Toa mifano ya namna unavyojaribu kumfurahisha mwenzi wako, au ugumu unaoupata kuhusu hili.



**Swali la 21 & 22:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Je, mwanamume anaweza kutunza mamlaka yake nyumbani bila ya kuwapiga mke na watoto?

*Katika baadhi ya tamaduni, kupiga mke ni kawaida, bali Biblia inasema 'kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe'. Efe. 5:28.*
- 1 Petro 3:7 inasema nini kuhusu namna ya kumtendea mke? *'kaeni na wake zenu kwa akili' na 'na kumpa mke heshima'.*
- Toa mifano namna jambo hili linaweza kuonekana kwa vitendo.
- **Soma swali la 22**: Uliandika nini? *Majibu yanaweza kutofautiana, bali swali linawasaidi waume kufikiria namna ya kuishi kwa akili na wake zao kwa namna isiyo ya kibinafsi.*

## Kristo na mwenzi wako (Swali la 23-26)

**Swali la 24:** Soma habari ya kweli ndani ya kisanduku, na swali lililopo hapo chini. Nini maoni yako?

*Mwenzi anaweza kumgeukia Kristo. Hata kama siyo, mfuasi wa Kristo anapokuwa mvumilivu na mwenye upendo, husaidia kutunza amani ndani ya nyumba.*

**Swali la 26a:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Ni majibu gani uliweka vema, kwa nini?
- Ni kwa namna gani mnaweza 'kuungana pamoja kuwalea watoto wenu ili wawe wafuasi wa Yesu'?

*Mano: uwe mfano mzuri wa Kikristo; wape watoto wetu muda, usikivu, upendo, nidhamu njema, omba msamaha tunapokosa; kuwaombea; omba na soma Biblia kila siku; wahusishe unapokutana na waumini wengine.*

**Swali la 26b:** Soma kitufe cha mwalimu. **Tumia zoezi hili kulingana na kundi lako.**
Wape wanafunzi karatasi na kalamu. Kwa dakika 5, zingatia na andikeni ama:
- Mawazo 5 ya kivitendo ili kuimarisha mahusiano yako na mkeo au mumeo.
- **AU**, kama hujaoa au kuolewa, maeneo 5 ambayo unapenda ukue zaidi, ili baadaye uwe mume/mke mwema.

## *Mwisho*

**Kutii fundisho la leo:** Ni kitu gani muhimu ulichojifunza kuhusu ndoa? Ni kwa namna gani utatekeleza kwa vitendo?
- Utafanya lipi kati ya hizi wiki hii?

**Tia moyo**: Pendekeza kozi ya ndoa ya Kikristo kama ni inahitajika. Toa nafasi ya kuzungumza kwa faragha na watu walio na maswali kuhusu somo hili.

**Ombeni pamoja:**
Gawanyikeni katika makundi kulingana na jinsia au walioa na kuolewa ili kuomba msaada wa Mungu ili kutii yale waliyojifunza kuhusu ndoa.

# Somo la 12: Kutatua migogoro yetu

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. Chagua njia bora ya kutatua migogoro, siyo njia mbaya.
b. kufahamu na kufanya kwa vitendo hatua tatu za kutatua mgogoro kwa njia iliyo njema.
c. Kariri 1 Petro 3:11.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Migogoro na namna ya kuitatua
- Je, Mungu ana mihemuko?

**Andaa:** ona kama igizo litafaa kwa wanafunzi wako. Andaa wimbo & msalaba kwa kipindi cha maombi.

## *Kufungua*

**Shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** Ulifanya nini kwa wiki hii kilichosaidia kuimarisha ndoa yako au kumfurahisha mwenzi wako? Ilikuwaje? Au kama hujaoa au kuolewa, ulifanya jambo gani kwa vitendo?

**Somo la 12 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** Njia tatu zote ni mbaya katika kutatua migogoro.
**Swali la 2:** mihemuko, zungumza, toa, pokea msamaha.
**Swali la 3:** amani na aifuate sana (1 Petro 3:11)

**Tambulisha somo la leo:** Je, inawezekana kwetu waumini kuishi katika amani kamilifu na kamwe kusiwe na migogoro? *Kwa nadharia inawezekana, lakini kwa vitendo wafuasi wa Kristo, kama wale wasio-Wakristo, huwa wanaingia katika migogoro. Hata hivyo, kama waumini tunapaswa kuwa na njia nzuri ya kutatua migogoro kuliko wasio-Wakristo.*

## *Majadiliano*

### Migogoro kati ya wafuasi wa Kristo (Swali la 1-5)

**Swali la 5:**
- Kutokana na usemi wa a) hadi e), uliweka alama ya vema kwenye zipi?
- Katika usemi f), ni mfano gani ulioandika kutokana na uzoefu wako mwenyewe?

### Mungu anataka tutatue migogoro yetu (Swali la 6)

**Swali la 6:**
- Je, unafikiri matendo yetu yanaweza kumhuzunisha Mungu? *Uislamu hufundisha kwamba matendo yetu hayawezi kumwathiri Mungu, bali Biblia hufundisha kwamba ndiyo yanaweza. Mfano: katika Mwanzo 6:5-6, Mungu 'akaghairi' kwa sababu ya dhambi za watu na 'moyo wake ulijawa na maumivu'.*
- Unafikiri ni kwa nini migogoro yetu humhuzunisha Mungu? *Mfano: Kristo alilipa gharama kubwa mno ili kutuletea amani, anatamani tuishi kwa amani. Pia tunapokuwa na migogoro huo ni ushuhuda mbaya kwa wasioamini.*

**Soma 1 Petro 3:8-12:**
- Ni matendo gani mema na nia njema zinazotusaidia kuishi kwa amani na kila mmoja? (ms. 8)
- Ni matendo gani mabaya tunayopaswa kuyaacha? (ms.9)
- Badala yake tufanye nini?
- Tufanye nini zaidi, katika mstari wa 10? Kwa nini?
- Kifungu hiki kitaleta tofauti gani katika tabia yako wakati mwingine utakapoingia katika mgogoro na mtu mwingine?
- Ni sehemu gani ya mstari huu ni mstari wa kukariri? Wote waurudie kama walivyoukariri.

*ms. 8, ishi kwa utulivu, mpendani kila mmoja na mwenzake, uwe na huruma, mpole.*
*ms. 9, kulipa baya kwa baya au laumu kwa laumu. Badala yake tunapaswa kubariki.*
*ms. 10, Kuzuia ndimi zetu zisinene mabaya na midomo yetu isinene hila. Maana ulimi wa uovu na hila huchuchea sana migogoro.*

### Bjia mbaya za kushughulikia migogoro (Swali la 7-10)

**Swali la 7-10:** Jadili njia tatu mbaya za kushughulikia migogoro.
- Husababisha matokeo hasi gani kwa watu na mahusiano?
- Je, kuna mtu ye yote aliyepata uzoefu wa njia tatu hizi mbaya? Matokeo hasi ni yapi?

## Njia nzuri ya kutatua migogoro (Swali la 11-23)

**Ni njia tatu zipi zinazoweza kutumika kutatua migogoro? Tutajadili kila moja.**

**Hatua ya 1: Kabidhi mihemuko yako kwa Mungu.**

**Swali la 11-13:** Kwa nini ni vizuri kukabidhi mihemuko yetu kwa Mungu kabla ya kwenda kuzungumza na mtu mhusika?

*Kwa msaada wa Mungu, tunaweza kudhibiti hasira yetu. Kisha tunaweza kuzungumza kwa utulivu na mtu mhusika. Kama tutaingia katika hali ya hasira, inaweza kuharibu mambo.*

**Hatua ya 2: Zungumza na mtu mhusika.**

**Swali la 14:** Soma kitufe chenye maneno.

- Ni kitu kizuri kuhusu majadiliano yao?
- Kwa nini mambo yote haya huwasaidia kutatua migogoro yao?

*Wana utulivu, wanasikiliza kwa makini, siyo kuingiliana, wanaelezea hisia, wanasema ukweli kwa upendo.*

**Swali la 17:**

- Uliandika nini hapa? Kwa nini? *Tunapozungumzia tatizo na watu mbalimbali husaidia kuenea na kufika mbali, kama mbegu kwenye upepo, huongeza maumivi na kusababisha ugumu wa kufikia suluhu kwa haraka.*
- Je, ni vizuri kumshirikisha mtu wa tatu, kama mpatanishi? *Jadili. Kutatua moja kwa moja kati ya watu wawili ni vizuri zaidi. Lakini kama watashindwa kufikia muafaka wao wenyewe, ni vizuri kupata mpatanishi ambaye anaheshimika kwa wote wawili, hasa pale ambapo mmoja wao anapojaribu kulazimisha utii kutoka kwa mwenzake (ona Swali la 9).*

**Hatua ya 3: Toa na kupokea msamaha.**

**Swali la 20:** Soa kitufe chenye maneno.

- Katika mazungumzo haya, ni nani anayeomba radhi: Ali au Karim?

*Wote wawili! Kila mmoja wao anataja sehemu yake aliyokosea, na wanaomba radhi kwa hilo.*

**Sehemu ya vitendo – kutatua mgogoro kwa kutumia igizo (dakika 5 ongeza majadiliano)**

Ligawe kundi katika watu wawili wawili na wapatie sehemu ya kuigiza **1** au **2**. Mmoja anaweza kuwa A, na mwingine, B, na wote wawili waigize namna wanavyoweza kutatua mgogoro huu. Baada ya hapo wengine wanaweza kujitokeza pia kuigiza mbele ya darasa.

1. Mtu A alimkopesha fedha rafiki yake ambaye ni mtu B, na hajarejesha kwa wakati. Hivyo, mtu A anamlalamikia huyo mtu B kwa kumwambia mtu mwingine.
2. Mume na mke wanakaribisha ndugu zao kwa chakula maalumu. Mke (Mtu B) anachelewa kutenga chakula, mume wake (Mtu A) anakasirika mbele ya wageni. Mke anadhani amemfedhehesha, na mume anadhani amefedheheshwa na mke wake.

**Baada ya kuona igizo: Je, walitumia hatua zote tatu? Ilikuwaje? Ulijifunza nini?**

**Swali la 22-23:**

- Kwa nini tusamehe? *Mungu ametusamehe.*
- Tunapaswa kumsamehe mtu mara ngapi? Soma na jadilini kwa pamoja Mathayo 18:21-22.
- Tazama picha katika swali la 23. Elezea mihemuko yako ulipaweza kupatana na mtu fulani.
- Tunaweza kufanya nini pale mtu anaposhindwa kupatana nasi? *Soma maneno ya mwalimu.*

**Pata muda wa utulivu ambapo kila mtu analeta kwa Mungu mgogoro walio nao au wanaufahamu.**

## *Mwisho*

**Kutii mafundisho ya leo:**

- Umejifunza nini leo ambacho kitabadilisha namna unavyoshughulikia migogoro?
- **Someni kwa pamoja shughuli ya kivitendo.**
- Shughuli ya kivitendo inatuandaa tu kuzungumza na mtu huyo, lakini unapaswa kufanya. Pale Mungu atakaposema ni wakati sahihi, nenda na zungumza na mtu huyo.

**Oba kwa pamoja: Kumbuka kwamba tumesamehewa!**

**1.** Imba kwa pamoja au chezeni wimbo wo wote kuhusu msamaha kwa lugha ya Kiingereza au lugha ya wanafunzi wako, kwa mfano, 'Nimesamehewa'. Unaweza kuweka msalaba ili watu watafakari zaidi. Ruhusu muda wa utulivu ili kutafakari msamaha wa Kristo kwetu.

**2.** Waombe watu waombe kimyakimya wakimwomba Mungu awasaidie kupatana na mtu yeyote wanayehitaji kufanya hivyo naye.

**3.** Kwa wiki hii, omba baraka na ulinzi juu ya mchakato wa msamaha na upatanisho kwa kila mtu.

# Somo la 13: Kushuhudia

| Malengo kwa wanafunzi: | Dokezo za kitamaduni: |
|---|---|
| a. kutaka kuwaambia wengine kuhusu Kristo.<br>b. Uwe na busara ya kufahamu ni nani umwambie na ni wakati gani.<br>c. uweze kuelezea kile Yesu Kristo alichotutendea.<br>d. Kariri 1 Petro 3:18. | • Waislamu na ushuhuda (Shahada)<br>• Ujasiri au tahadhari?<br>• Mchoro wa 'Daraja'<br>**Andaa:** video fupi kwa ajili ya swali la 13 |

## *Kufungua*

**Rudia shughuli ya kivitendo:** je, uliweza kutatua mgogoro na mtu fulani, au bado unaombea fursa sahihi? Nini kilitokea?

**Msifu Mungu kwa kile alichotutendea, kisha ombwa kwa ajili ya somo hili.**

**Somo la 13 mapitio ya kujisomea nyumbani:**

**Swali la 1:** a) kuogofya; b) kuwa tayari; c) upole, hofu

**Swali la 2:** a) kuwa tayari, jibu; b) upole, hofu **Swali la 3:** ona swali la 10 (1 Petro 3:18)

**Tambulisha mada ya leo:** ni nani aliyekuambia habari za maisha mapya ndani ya Kristo? *Mwombe kila mtu ashirikishe*.

Tuna maisha mapya kwa sababu kuna mtu alituambia kuhusu hili. Kwa namna hiyo hiyo nasi tunapaswa kushirikisha maisha yetu mapya na kuwaambia wengine wapi kwa kuyapata. Kushuhudia (*shahada*) ni wajibu wa wafuasi wote wa Kristo.

## *Majadiliano*

### Kushuhudia kwa ajili ya Kristo (Swali la 1)

**Soma 1 Petro 3:14-18**


- Ni miongozo mitatu ipi muhimu tuliyojifunza kutoka katika 1 Petro 3:14-15?

*'msiogope kutisha kwao', 'mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye', 'kwa upole na hofu'.*

### Usiogope kutisha kwao (Swali la 2-7)

**Swali la 5:** soma swali.

- Ni mwanafamilia yupi wa Kiislamu anayefahamu kwamba wewe ni mfuasi wa Kristo?
- Je, mara zote unaomba kama mwanamume huyu kwenye picha au kama yule mwanamke?



**Swali la 6:** Soma swali. Uliandika jibu gani hapa?

- Je, bado hujakabiliana na 'kipindi cha kujaribiwa' pale ndugu zako wa Kiislamu walipofahamu kwamba wewe ni mfuasi wa Kristo? Kama ni hivyo, kilitokea nini, na matokeo yake yalikuwaje? *Ni majadiliano muhimu, usiwe na haraka.*
- Kama bado hujakabiliana na hali hii, unaweza kuchagua pale unapowaambia wengine au inaweza kutokea nje ya uwezo wako? *Tunapaswa kujiandaa maana inaweza kutokea wakati usipotarajia.*

### Uwe tayari kumjibu kila mtu (Swali la 8-13)

**Swali 8:** waulize wanafunzi washirikishe kile wanaweza kusema kwa ajili ya A, B na C. *Majibu yanayowezekana:*

***A**. kijana anaonesha mamlaka ya baba na tabia. Tunatumia 'mwana wa' kama mfano na siyo halisi. Mfano, kwa Kiarabu 'mwana wa barabara' humaanisha msafiri, na kwa Kifarsi 'mwana wa Kabul' humaanisha mtu kutoka Kabul.*

***B**. Tunawapenda wakurugenzi wetu na kabila na familia. Mimi namfuata Yesu aliyekuwa mtu wa Mashariki na siyo kutoka Magharibi. Kwa miaka elfu moja ya kwanza Wakristo walio wengi hawakuwa wa kutoka magharibi, na ndivyo ilivyo hata leo!*

***C**. Siyo kweli kwamba Wakristo walibadilisha Biblia. Katika makumbusho ya kiulimwengu leo kuna miswaada ya kale mingi tu ya Biblia. Kwa kuilinganisha tunapata ujasiri mkubwa kuhusu maadnishi ya asili ya Biblia.*

**Swali la 9:** Soma kitufe chenye maneno. Utampa jibu gani huyu mwanamke?

**Swali la 10:** Soma swali na ufanyie kazi mstari wa kukariri.

### Zoezi: Kuwaambia watu habari njema

**Swali la 13:** wagawe wote katika vikundi vya watu wawili wawili.

- Mtu wa kwanza atumie dakika tatu kuelezea Yesu Kristo alifanya nini kwa ajili ya wanadamu. Atumie jibu waliloandika katika swali la 13. Pia wanaweza kutumia Nyongeza ya 2 kama wanataka.
- Kisha wabadilishane, na mtu wa pili apate dakika tatu kwa ajili ya maelezo yao.
- Kutaneni kwa pamoja. Je, zoezi hili lilikusaidia 'kuwa tayari kumjibu kila mtu'?
- Je, uliona 1 Petro 3:18 ni msaada katika kuelezea kile Bwana Yesu ametutendea wanadamu?

**Kusimulia habari yetu kutoka kwa manabii:**

- Hatupaswi kuanza moja kwa moja na Yesu na Agano Jipya. Ni kwa namna gani unaweza kutumia manabii wa Agano la Kale ikiwa ni safari inayotuongoza kuelekea kwa Yesu Masihi?

*Marafiki zetu wa Kiislamu wana ufahamu sana na manabii kama vile Adamu, Nuhu (Nuh), Ibrahimu (Ibrahim), Yusufu (Yusuf), Musa na Daudi. Lakini Kuran haitoi maelezo ya kutosha kuhusu hao. Tunaweza kuwaambia marafiki zetu kuwa kuna maelezo mengi ya kuvutia katika Torati (Tawrat) kuhusu manabii hawa. Kisha kwa kutumia habari hizi tunaweza kuonesha namna zinavyotuelekeza kwa Kristo aliye dhabihu ya kweli na suluhu kwa laana ya Adamu.*

***Kama muda unaruhusu, tazama mwanzo wa Filamu ya Yesu (toleo lile linaloanza na uumbaji), au 'habari za manabii' kwenye youtube. Zote zina dakika 8 na hupatikana kwa lugha mbalimbali.***

## Kwa upole na hofu (Swali la 14-18)

**Swali la 16-17:** Soma maswali.

- Katika swali la 17, utaweza kufanya nini katika hali hizo ngumu? *Hali mbili za mwanzo zinaweza kubadilika mara, lakini ile ya tatu ni makini zaidi maana ina madhara ya kudumu.*
- Katika hali inayokulazimisha kuwakataa ndugu zako wa Kiislamu kwa ajili ya Kristo, unawezaje kufanya hivyo kwa 'upole na hofu'? *Zungumza kwa heshima, siyo kwa hasira. Isaidie famila kwa mambo mbalimbali na onesha upendo wako. Usifanye mambo mengi ya kuwafedhehesha. Chagua muda muafaka.*

## Mkate wa uzima (Swali la 19-20)

**Swali la 19:**

- Kwa nini jukumu letu ni kama lile la 'ombaomba mmoja anamwambia mwingine namna ya kupata mkate'?

*Mehdi Dibaj katika jaribu lake alitoa hoja iliyo sawa na methali ya Kiajemi. Alisema, "Waliupinga uinjilishaji wangu. Lakini 'kama ukimkuta kipofu karibu na kisima na ukakaa kimya umetenda dhambi'." Miezi sita baadaye aliuawa. Ujasiri wake wa kushuhudia uligharimu maisha yake. Mshuhudiaji (shahid) alifanyika kifo yaani mfia dini (shaheed).*

- Je, ilifaa? Unafikiri nini?

**Swali la 20:** Soma habari na swali.

- Ni kwa namna gani tunaweza kupata uwiano kati ya kuharakisha kuwaambia familia yetu kuhusu Yesu Kristo kabla hawajawa tayari na kusubiri sana?

***Ushauri kutoka kwa waumini wenye uzoefu hujumuisha yafuatayo:***
► Ruhusu maisha yako yaoneshe mabadiliko chanya kwa familia yako; ►Usikosoe kwa nguvu dini ya familia yenu; ►Usiwe na haraka ya kusema kwamba wewe ni Mkristo'; ► Polepole dokeza kwamba umepata msaada katika Biblia; ►Kama familia itakuuliza moja kwa moja kama wewe ni mfuasi wa Kristo, usikanushe; ►Mwombe sana Mungu ili aiandae mioyo yao; ► Mjulishe mwanafamilia aliye na huruma kwanza; ►Familia inaweza kusikia kuwa wewe ni mfuasi wa Kristo kabla hujawaambia, lakini Mungu ndiye anayetawala hali zote na anatenda yote kwa wema;

## *Mwisho*

| Kutii somo la leo | Omba kwa pamoja |
|---|---|
| **Kutii somo la leo:** Somo hili litaleta tofauti gani katika maisha yako?<br>• **Someni kwa pamoja shughuli ya kivitendo.** Utashirikisha nini kuhusu Yesu? | **Omba kwa pamoja:** Waombe wanafunzi washirikishane wawili wawili kuhusu imani yao, na kisha kuombeana kila mmoja na mwenzake kwa ajili ya hekima na nguvu ya kuwa mashahidi wema, hasa katika familia zetu. |

# Somo la 14: Ubatizo

| Malengo kwa ajili ya wanafunzi: | Dokezo za kitamaduni: |
|---|---|
| a. kuzifahamu kweli tatu kuhusu ubatizo.<br>b. ama kutazama nyuma kwa furaha kuhusu ubatizo wao au kutarajia na kupanga kuhusu ubatizo wao hapo baadaye.<br>c. Kariri Mathayo 28:19. | • WMK na ubatizo<br>• Utaratibu wa kutawadha katika Uislamu |

## *Kufungua*

**Shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** ulipata fursa zipi kwa wiki hii au kushirikisha imani yako kwa namna fulani kwa mtu fulani? *Kwa wale ambao bado, uliza 'je, mnaendelea kuombea hili?'*

**Somo la 14 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** mataifa yote, mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu (Mathayo 28:19).
**Swali la 2:** a) mtu; b) dhambi, kuoshwa; c) jumuia **Swali la 3:** muhimu sana

**Tambulisha mada ya leo:**
Je, wewe ni kama Hamid kwenye picha? Una maswali gani kuhusu ubatizo? Tutajaribu kujibu maswali yako leo.



**Oba kwa ajili ya somo la leo** *au mwombe mwanafunzi aombe.*

## *Majadiliano*

### Kwa nini nibatizwe? (Swali la 2-3)

**Swali la 2:** Soma swali.
- Ni sababu ipi nzuri inayotufanya tubatizwe? *Maana Bwana Yesu Kristo aliamuru.*
- Unakumbuka mazingira ambapo Yesu alitoa amri hii? *Baada ya ufufuo wake, kabla hajapaa mbinguni, aliwaamuru wafuasi wake kuendeleza kazi aliyoianzisha. Tangu hapo mpaka leo wafuasi wa Kristo wameendelea kufanya wanafunzi na kuwabatiza.*
- Nani anaweza kuusema mstari wa kukariri wa Mathayo 28:19? *Rudia hili na umpa nafasi kila mmoja kuusema mstari huo.*

### Ubatizo huonesha nini? *Mimi ni mtu mpya katika Kristo* (Swali la 4-8)

**Swali la 4:** soma paragrafu ya kwanza.
- Kwa maneno yako mwenyewe, eleza ubatizo huonesha nini kuhusu utu wetu wa kale na utu wetu mpya. *Utu wetu wa kale umekufa na tumefufuka katika utu mpya*

**Swali la 7:** Soma habari ya Firaz.
- Wale mliobatizwa, baada ya kutoka majini mlijihisi kama Firaz?
- Mihemuko yako ilikuwaje?

### Ubatizo huonesha nini? *Dhambi zangu zimeondolewa* (Swali la 9-11)

**Swali la 10:** Soma paragrafu ya kwanza.
- Je, maji ya ubatizo yana nguvu isiyo ya kawaida ya kuziosha dhambi zetu? *Hapana*
- Ni ni kinachosafisha dhambi zetu?*1 Yohana 1:7- damu ya Yesu husafisha dhambi zetu. Muaji huondoa uchafu tu ulio katika miili yetu, lakini ubatizo ni ishara muhimu sana ya Kristo kuosha dhambi zetu kutoka katika mioyo yetu.*

### Ubatizo huonesha nini? *Nimejiunga na jumuia ya Kristo* (Swali la 12-14)

**Swali la 12-13:** Soma swali lote kuhusu kujiunga na jumuia ya Kristo
- Unaweza kumwambia nini mtu anayedai, 'Ninabatizwa kwa ajili yangu mwenyewe, ni kati yangu na Mungu, siyo lazima nijiunge na kanisa?

*Kulingana na 1 Wakorintho 12:13, ubatizo humaanisha kuwa sehemu ya mwili wa Kristo – jumuia yake. Hili linaweza kuwa kanisa la mtaa au siyo, lakini tunapaswa kujiunga na mwili wa waumini kwa njia fualani. Sisi ni sehemu yao na wao ni sehemu yetu. Kwa pamoja sisi tu wateule wa Mungu.*

**Swawli la 14:** Bila kuangalia kwenye vitabu vyenu, rudia kweli tatu: ubatizo huonesha nini?

- Lipi kati ya hayo lililo la muhimu kwako?

## Je, ubatizo ni wa muhimu? (Swali la 15-17)

**Swali la 15-16:**

- Je, ni muhimu kwa kila mwumini kubatizwa? Kwa nini au kwa nini siyo? *Jadili.*

**Kutoa ushuhuda wako:**

Fikiria kwamba ni ubatizo wako na kwamba unatoa ushuhuda wako kwa kundi lote. Kwa muda wa dakika tano, utasema nini? Tumia maelezo ulioandaa kwa ajili ya swali la 16.

*Omba mtu mmoja au watu wengi watoe shuhuda zao kwa kundi lote au wanaweza kupeana zamu kwenye vikungi vyao au watu wawili wawili. Pia, na wewe uwe tayari kutoa ushuhuda wako! Zingatia kwamba BMBs* huombwa kufanya hivi, wakiwa waumini wapya. Wakati mwingine huombwa kufanya hivyo mara nyingi kadiri inavyowezekana na huwa hawapendi kusimamishwa mimbarini. Uwe makini na hilo pale unapoomba nani angependa kufanya kwa vitendo kutoa ushuhuda wake mbele ya kundi.*

** BMBs = Believers from Muslim Background*

## Nibatizwe lini? (Swali la 18-22)

**Swali la 21:** Uliandika nini kwenye swali hili? *Baadhi ya mapendekezo, hutegemea mazingira.*

- Usitangaze hadharani, badala yake karibisha kwa siri watu unaowaamini;
- Pata ubatizo mahali penye ukimya ambapo watu wa nje hawataona;
- Uwe na kamera moja tu, na mruhusu yule aliyebatizwa aamue nani atapata nakala ya picha hizo;
- Kwa kamera hiyo, usichukue picha wakati mtu huyo akiwa majini (picha zinaweza kuchukuliwa baadaye, kwenye kikundi akiwa pamoja na marafiki);
- Kama kuna chetu cha ubatizo, tunza mahali palipo salama sana.

**Swali la 22:** Soma paragrafu ya kwanza.

- Uliandika nini hapa?

*Jadilini pamoja. Hakuna jibu 'lililo sahihi' maana hutegemeana na mazingira au hali. Wale waliosubiri mpaka wabatizwe pamoja na wenzi wao mara zote wamefurahia sana. Lakini kama baada ya miaka mingi mwenzi hampokei Yesu Kristo, mwenzi anaweza kuhisi kuwa ni sawa kuendelea na uamuzi wao peke yao.*

**Zingatia**: Tazama kwenye vitabu vya wanafunzi, kwamba wameandika kitu kwa ajili ya swali la 21 na 22. Kuandika huwasaidia kufikiri kwa makini zaidi na kuweza kushiriki vizuri zaidi kwenye majadiliano.

- **Soma kitufe chenye maneno ya mwalimu.**
- Ndiyo, ingawa ubatizo una uhatarishi mwingi, hatupaswi kuogopa sana. Ni wakati wa kusherehekea!"

## *Mwisho*

**Kutii fundisho la leo:**

- Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?
- **Someni kwa pamoja shughuli ya kivitendo. Kama baadhi yao hawajui wazungumze na nai, waelekeze kwa mtu sahihi.**
- Lazima ufanye shughuli ya wiki hii kama bado hujabatizwa. Na kama ulishabatizwa tayari, unaweza kukutana na mshirika wa kundi lako ambaye bado anafikiria kuhusu hatua hii. Mpatie mtu huyo ushauri na omba pamoja naye

**Omba pamoja:**

Acha dakika chache za ukimywa kwa wanafunzi kuomba kimyakimya na kutafakari kuhusu linin a namna gani wanaweza kubatizwa.
Kisha mwombe kila mtu ashirikishe kitu kimoja ambacho anashukuru na eneo moja ambapo kuna hitaji. Msifu Mungu na ombea mahitaji haya.

# Somo la 15: Njia iliyonyooka

**Malengo kwa wanafunzi:**
a. kujidhatiti kuishi kwa ajili ya Mungu na siyo kwa ajili yake mwenyewe.
b. kukubali kwamba hatuwezi kutembea katika 'njia iliyonyooka' kwa juhudi zetu wenyewe.
c. kufahamu kwanini utumwa kwenda kwa Kristo huleta uhuru wa kweli.
d. Kariri 1 Wakorintho 6:19-20.

**Sokezo za kitamaduni:**
- Sharia & utunzaji wa sheria katika Uislamu
- Uislamu & njia iliyonyooka
- Dhambi 'kubwa' & 'ndogo'

## *Kufungua*

**Shughuli ya kivitendo ya wili iliyopita:** Je, ulipata ushauri kuhusu kupata ubatizo, au ulitoa ushauri katika hili? Kwa nini uliamua? *Kama mshirika yeyote anataka kubatizwa mapema, jadilini mipango hiyo baada ya kikao.*

**Somo la 15 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** a) sheria ya Musa; b) sheria ya Kristo **Swali la 2:** Mtakatifu
**Swali la 3:** a), b) na c) yote yanakatazwa katika sharia (sheria) ya Kristo; kwa ajili ya d) na e), omba walichoandika
**Swali la 4:** 1 Wakorintho 6:19-20. Ona swali la 21.

**Tambulisha mada ya leo:** Je, unadhani kanuni katika Ukristo ni rahisi kuliko za Kiislamu? *jadili. Ruhusu washirika waeleze maoni yao. Kwa muda wa wiki 3 zijazo tutajifunza kuhusu aina tatu za sharia.*

## *Majadiliano*

### Kwa nini watu hawawezi kufuata njia iliyonyooka? (Swali la 1-4)

**Tazama picha ya huyo mlevi.**



- Kwa nini mtu huyo hawezi kutembea katika njia ilinyooka? *Yuko chini ya utawala wa kileo.*
- Nini maana ya kiroho ya mfano huu? *Wanadamu wako chini ya utawala wa dhambi na wamekuwa walevi wake. Hawawezi kutembea wima hata kama wanataka.*
- Katika sala za kiibada (salah au namaz), watu huomba 'niongoze katika njia iliyonyooka'. Wanafikiri Mungu alituma maelfu ya malaika kwa ajili ya mwongozo. Lakini mwongozo pekee unatosha kuwafanya watembee katika Njia Iliyonyooka? Kwa nini siyo? *Maombi & manabii ni vema, lakini watu wanahitaji nguvu ili watembee wima.*

**Swali la 3:** Soma swali.
- Kitabu kinasema jibu la d) ni sahihi, lakini unakubali?
- Ni kwa namna gani unaweza kuelezea kwa rafiki yako Mwislamu kwamba sheria za ziada hazitoshi kuwaokoa watu kutoka katika ulevi wao wa dhambi?

*Mambo haya husaidia kidogo kwa ngazi ya kibinadamu, lakini hayawezi kushughulika na tatizo la msingi ambalo linahitaji nguvu ya Mungu.*

### Safi na Najisi (Swali la 5-6)

**Swali la 5:** Soma swali.
- Ni maneno gani uliyopigia mstari? *'mawazo mabaya, uasherati, wizi, uuaji, uzinzi, uchoyo, uongo, udanganyifu, wivu, kiburi, ujinga'.*
- Je, chakula halal (safi) kiliwafanya Mafarisayo wawe safi ndani yao? Kwa nini siyo? *Hapana, maana dhambi zao za ndani huwachafua kwa ndani.*
- Ni kilicho cha muhimu zaidi, chakula najisi au mawazo najisi? *Mawazo najisi huzingatiwa zaidi, maana huichafua mioyo yetu, kisha maneno machafu na matendo mabaya hujitokeza.*

**Swali la 6:** Uliandika nini?
- Je, ni rahisi kusafisha mikono yetu au mioyo yetu?

*Wanafunzi <u>wanapoandika</u> maoni yao, wafikiri zaidi kuhusu hili na wawe tayari kwa majadiliano.*

### Tiba ya Mungu kwa ajili ya moyo najisi (Swali la 7-10)

**Swali la 7:** Soma swali na rudia mstari wa kukariri na kila mtu akitaja jina lake.
- Nani anatusaidiza kwenye Njia iliyonyooka? Ni nani anayetuwezesha kufanya hivyo? *Roho wa Mungu*

### Kuishi kwa ajili ya Mungu (Swali la 11-16)

**Swali la 15:** Tazameni kwa pamoja hayo maoni.

- Jibu la a) ni sahihi, lakini vipi kuhusu b)? Je, dhambi ndogo zina madhara? Kwa nini au kwa nini siyo?
- Vipi kuhusu jibu la d), kusema uongo, au e), mawazo mabaya?
- Kama tuna nia kwa ajili ya dhambi lakini hatuitendei kazi, je, hiyo bado ni dhambi?

*Yawezekana hazina madhara katika Uislamu, lakini katika sharia za Kristo ni ndiyo zina madhara maana kiwango chake ni cha juu sana. Kama Shetani atatujaribu kwa mawazo mabaya na tukayapinga hiyo siyo dhambi. Lakini kama tutaendelea kuyatafakari au kupanga kuyatimiza, hiyo ni dhambi.*

**Swali la 16:** Soma swali.

- Ni majibu yapi katika orodhi hiyo unadhani ni muhimu? Kwa nini? *Jibu la b), c), e) na g) yanatoka katika 1 Petro, hivyo yako katika sheria ya Kristo. a), d) na f) hayatoki katika Injil, hivyo ni hiari kwa wafuasi wa Kristo. Pia jibu la b), c), e) na g) yanahusu nia zetu na tabia zetu kwa wengine. Katika Sharia za Kristo, mambo haya ni muhimu sana kuliko a), d) na f) ambayo yanahusu mwonekano wetu wa nje au matambiko.*

## Uhuru wa kweli (Swali la 17-22)

**Soma Warumi 6:11-18:** *Hiki ni kifungu kigumu, kisome mara mbili au katika tafsili mbili tofauti ili kuwasaidia wanafunzi kukielewa.*


- Nani anaweza kueleza mawazo makuu ya kifungu hiki?
- Katika ms.11, tunapaswa kufa katika lipi na kuwa hai katika lipi? *Kufa katika dhambi na kuwa hai katika Mungu.*
- Mstari wa 12, 13 & 14 inatueleza mara tatu kujiepusha na dhambi katika maisha yetu. Amri tatu hizo ni zipi? *'dhambi isitawale' (ms.12), 'msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi' (ms.13), 'dhambi haitawatawala ninyi' (ms.14).*
- Kulingana na ms. 14, kwa nini dhambi siyo bwana wetu tena? *Hatuko chini ya sheria bali chini ya neema.*
- Kama tuko 'chini ya neema', je, hii humaanisha kwamba tunaweza kufanya cho chote tunachotaka? Kwa nini au kwa nini siyo? Ona mstari wa 15-16. *Hapana! Maana ni lazima tujitoe wenyewe kwa Mungu kama bwana wetu mpya. Tuko huru kumtii Mungu, na siyo huru kutenda dhambi.*
- Mstari wa 17-18 unasema sasa sisi ni watumwa wa haki. Katika uzoefu wako, je, huu ni mzigo au furaha? *Ni furaha. Majadiliano lazima yahusishe furaha chanya ya kuishi kwa ajili ya Mungu, siyo changamoto tu ya kupambana na dhambi.*
- Sitisha na ufikiri: Je, unataka kuwa mtumwa wa dhambi au kuwa huru kumtii Mungu?

**Swali la 17:** Soma swali lote.

- Uliandika nini hapa? *1 Petro 4:2-3 inatuambia tusiendelee kuishi katika tamaa za wanadamu bali katika mapenzi ya Mungu.*

**Swali la 19:** Mtazame mtu katika picha hiyo.

- Je, mtu huyu yuko huru au la? Uliandika nini?



**Swali la 20:** Huyu ni mtu yule yule wa awali

- Kimetokea nini kwenye minyororo yake? *Imevunjika msalabani.*
- Tunapataje uhuru wa kweli, kwa kuishi kwa kuzifuata tamaa za wanadamu au kwa ajili ya Yesu Kristo?
  *Uhuru wa kweli huja kwa kufanyika watumwa wa Kristo. Inashangaza lakini ni kweli.*
- Hebu tushirikishane mifano kutokana na uzoefu wetu wenyewe wa namna Yesu alivyotuweka huru kutoka katika mazoea mabaya.
  *Kama mshauri, toa mfano halisi kutoka katika maisha yako mwenyewe na simulia furaha ya kuishi kwa ajili ya Mungu.*

**Swali la 21:** Soma & fanyia kwa vitendo mstari wa kukariri (ni sehemu ya 1 Wakorintho 6:19-20). Kila mmoja auseme mstari kwa mtu aliye karibu naye, kwa kutumia majina yao. Mfano, 'Umar, wewe hauko peke yako, ulinunuliwa kwa thamani. Kwa hiyo, mtukuze Mungu kwa mwili wako.'

## *Mwisho*

**Kutii somo la leo:** Umejifunza kitu gani muhimu kwa siku ya leo? Italeta tofauti gani katika maisha yako?
**Someni kwa pamoja sehemu ya shughuli ya kivitendo.** Inaweza kutusaidia kuwajibika kwa wengine kuhusu dhambi mahususi. Mkiwa wawili wawili, shirikishaneni namna mnavyohangaika na dhambi ya hasira. Kwa wiki hii tunza kumbukumbu kwa uaminifu ya namna ulivyoidhibiti hasira yako. Mnaweza kutumiana ujumbe kwa simu kuhusu hili.

**Ombeaneni wawili wawili kila mmoja na mwenzake:** Mshukuruni Mungu kwamba ametuweka huru kutoka katika utumwa wa dhambi. Omba msaada wake ili uwe mtumwa wa Kristo kwa wiki hii.

# Somo la 16: Sheria ya upendo

**Malengo kwa wanafunzi:**
a. kutafuta kumpenda Bwana kwa moyo wote, na jirani yetu kama nafsi zetu.
b. kuwa salama kwamba pendo la Mungu kwetu halitegemei upendo wetu kwake.
c. kufahamu kwamba kila kitu chetu ni kwa Mungu, kwa shukrani.
d. Kariri Marko 12:30-31.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Motisha wa Waislamu kwa ajili ya kutii
- Waislamu, WMK & ukarimu

**Andaa:** kama unataka, andaa mkate na juisi kwa ajili ya Meza ya Bwana.

## *Kufungua*

**Shughuli ya wiki iliyopita ya kivitendo:** Ni kwa namna gani ulidhibiti hasira yako kwa wiki hii? Gawanyikeni wawili wawili kama ilivyokuwa mwishoni mwa wiki iliyopita na mshirikishane kila mmoja kile ambacho kilifanyika vizuri, na nini ambacho hakikwenda vizuri. *Baada ya dakika 5 za kushirikishana, omba sala hii ukiwaomba wanafunzi warudie kila kifungu cha maneno unachotamaka:*

> Ee Baba Mungu... Asante kwa ahadi yako kwamba kama tukiziungama dhambi zetu... Wewe ni mwaminifu na wa haki... na utatusamehe dhambi zetu zote na kutusafisha udhalimu wetu wote...Tusamehe kwa maneno makali tuliyoyatamka wiki iliyopita… Tusafishe na tujaze na Roho wako… ili tukutumikie vizuri zaidi wiki hii. Katika jina la Bwana Yesu Kristo, Amina.

### Somo la 16 mapitio ya kujisomea nyumbani:

**Swali la 1:** ***Kwanza:*** Bwana, Mungu, moyo, nafsi, akili, nguvu ***Pili***: jirani, mwenyewe
**Swali la 2:** mpende **Swali la 3:**a) Siyo kweli; b) Kweli

**Tambulisha mada ya leo:** Sasa tunamfuata Yesu Kristo, tunapaswa kuishi kwa sheria au kanuni za nani? *Sheria za Kristo au sharia za Kristo.* Tunaziita sharia za Kristo kuwa ni sheria ya upendo. Leo, hebu tujifunze kuhusu upendo wa Mungu kwa ajili yetu, upendo wetu kwa Mungu na upendo wetu kwa ajili ya watu wengine.

## *Majadiliano*

### Mungu alitupenda sisi kwanza (Swali la 1-5)

Tazama picha ya watumishi wawili. Ni mtumishi gani aliye na furaha katika kumtumikia bwana wake? Hii ina maana gani kwetu? *Tunamtumikia Mungu kwa furaha kwa ajili yetu. Wengine humtumikia kwa hofu ya kupata adhabu.*

**Swali la 4:** Soma swali.
- Je, tuko salama na ulinzi katika pendo la Mungu?
- Hivyo, je atatupeleka jehanamu, hata kama ni kwa muda kitambo?
- Kwa nini basi tumtumikiea Mungu kwa moyo wote?

*Ndiyo, kama tuko ndani ya Kristo. Hapana, Kristo amelipa dhambi zetu zote. Waislamu walio wengi husema kwamba hawana hakika kama watakwenda moja kwa moja mbinguni au kupita jehanamu kwa muda.*

### Mungu alitoa upendo wake (Swali la 6-10)

**Swali la 7-8:** Wafuasi wa Kristo ulimwenguni kote huwa na sherehe mbili maalumu. Tulijifunza kuhusu ubatizo hapo awali. Moja huitwa Meza ya Bwana au Ushirika Mtakatifu.Tunashiriki ili kukumbuka na kusherehekea dhabihu ya Yesu Kristo iliyotolewa kwa ajili yetu msalabani. **Soma maswali yote 7-8.**

- Ni mara ngapi hushiriki Meza ya Bwana? Au bado hujapata fursa?
  *Baadhi ya makundi ya waumini hufanya hivyo mara kwa mara, wengine mara chache. Baadhi ya wanafunzi hawajapata nafasi ya kushiriki.*



- Sherehe hiyo huitwa kwa jina gani katika kundi lenu la waumini?
- Hisia zako huwa zikoje pale wakati wa kuumega mkate na kukinywea kikombe?
- Je, kundi lenu la waumini hutumia mvinyo au maji ya mzabibu? Kama ni mvinyo, je, hilo ni tatizo kwako?

*Katika nchi za Kiislamu, makanisa mengi hutumia juisi isiyo na kileo. Huko magharibi hutofautiana kati ya dhehebu na dhehebu lingine. Baadhi ya WMK hutumia kileo, wengine siyo, hivyo lipeleke suala hili kwa wanafunzi wako. Katika mazingira fulani fulani, pale ambapo kileo kinakubalika, kuna mazingira ambapo inaonekana kunywa kidogo ni tofauti na "kulewa".*

- Je, tunwaruhusu wasio waumini waumege mkate na kukinywea kikombe? *Hapana. Ni kwa ajili ya wafuasi wa Kristo mwenyewe.*

## Sheria ya upendo (Swali la 11-14)


**Soma 1 Yohana 4:7-13:**

- Ni mstari upi unaosema Mungu ni pendo? Hii inakufanya ujisikieje?
- Ni mistari ipi inayoonesha kwamba Mungu alitupenda sisi kwanza kabla hatujafanya cho chote cha kumrudishia?
- Ni kwa namna gani Mungu alionesha pendo lake?
- Kulingana na mstari wa 7 na 10, tuoneshe mwitikio gani kwa pendo la Mungu?
- Hakuna anayeweza kumwona Mungu mwenyewe, lakini nini wanaweza kukiona kama tutapendana kila mtu na mwenzake? Ona mstari wa 12.

*Mstari wa 8.*

*Mstari wa 9-10.*

*Mungu alimtuma Mwana wake (ms.9) kama dhabihu ya upatanisho (ms.10).*
*(Kinyume chake, Kurani hufundisha kwamba Mungu huwapenda wale wanaojisafisha.)*



*Kwa pendana kila mtu na mwenzake*

*Wanaona kwamba Mungu anaishi ndani yetu na pendo lake limekamilika ndani yetu.*

**Swali la 13: Rudia na fanyia mazoezi mstari wa kukariri:** Marko 12:30-31

- Muhtasari huu wa sheria ya Kristo ni mfupi sana na ni rahisi kukariri. Lakini, je, ni rahisi kutii?
- Ni nani anayetuwezesha kutii sheria hii ya upendo?*Roho wa Mungu katika maisha yetu.*

**Swali la 14:** Elezea kwa kifupi ni hoja zipi zenye buleti ambazo ulizizungushia mduara? Kwa nini?
*Mshauri lazima ashirikishe pia.*

## Kuwapenda majirani zetu kama nafsi zetu (Swali la 15-25)

**Swali la 17:** Tazama hizo picha nne. Jadili ni nani anayetii sharia za Kristo (sheria).

- Katika Picha A, kwa nini mume anataka kumfurahisha mkewe?
- Katika Picha B, ili kutii sheria ya Kristo, mume afanye nini?
- Katika Picha C, mi kwa njia zipi Mungu anaweza kujibu maombi ya mwanamke huyu?
- Katika Picha D, msichana hatii sharia ya Kristo (sheria). Matokeo yake yatakuwaje?

**Swali la 19:** Soma na jadili swali.

**Swali la 22:** Soma habari ya kweli katika kisanduku.

- Soma sehemu inayofuata baada ya kisanduku. Uliandika nini hapa?

**Swali la 24:** Tazama picha ya Farida na Asghar.

- Unafanana na ipi?

**Swali la 25:** Soma swali lote la 25 na kitufe chenye maneno.

- Unafikiri nini? Je, inawezekana kuwapenda adui zetu? *Ona Wafilipi 4:13!*
- Je, unaweza kutoa mifano halisi ya wafuasi wa Kristo waliowapenda adui zao?
- Kama watu wa nchi yako na jamii yako wangeanza kuwapenda adui zao, nini kingetokea?

*Habari moja ya kweli ni ya Farid katika Somo la 10. Nyingine imesimuliw katika kitabu cha Nik Ripken kiitwacho 'The Insanity of God' kuhusu mtu aliyetumia miaka mingi gerezani ambapo mlinzi wake alimtendea vibaya sana na kwa ukatili mkubwa. Miaka mingi baada ya kuachwa huru alikutana na mlinzi wake huyo, ambaye kwa wakati huo alikuwa mzee na ni mgonjwa. Mwumini huyu alimwombea mtu huyo na kumletea dawa.*

## *Mwisho*

**Kutii fundisho la leo:**

- 1 Petro 4:8 inasema "iweni na juhudi nyingi katika kupendana". Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?
- **Someni kwa pamoja shughuli ya kivitendo.**
- Endelea na kazi ya kujisomea nyumbani na shughuli ya kivitendo ya kila wiki!

**Ombeni kwa pamoja:**
Shirikini Meza ya Bwana kwa pamoja kama inawezekana. Kisha mpate muda wa kuomba, kumshukuru Yesu kwa ajili ya mwili wake na damu yake, na kuomba kwamba atusaidie kila mmoja wetu kuifuata sheria ya upendo.

# Somo la 17: Kufunga na Utoaji

| **Malengo kwa kila mwanafunzi:** | **Dokezo za kitamaduni:** |
|---|---|
| a. kuanza mazoea yenye nidhamu ya kufunga na kutoa chini ya uongozi wa Mungu.<br>b. Kuwa na furaha ya kufanya hivyo kwa ukarimu na kidhabihu, bila kulazimishwa au kutafuta sifa.<br>c. Kujifunza kanuni mbili za namna Mungu anavyotuongoza.<br>d. Rudia Marko 12:30-31. | • WMK na miongozo yenye maelezo mengi ya Sharia<br>• WMK na Ramadhan<br>• Waislamu na utoaji |

## *Kufungua*

**Shughuli ya kivitendo ya wiki iliyopita:** Je, ulipata nafasi ya kumsaidia mhitaji wa kike au kiume katika Kristo? Mtu huyo aliitikiaje? **Mtu mmoja aombe kwa ajili ya somo la leo.**

**Somo la 17 marudio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** Neno, Roho **Swali la 2:** maombi
**Swali la 3***:* a) yote; b) nyingi kadiri inavyowezekana **Swali la 4:** a) Mungu, watu; b) upendo

**Tambulisha mada ya leo:** Mpaka sasa tumejifunza nini kuhusu sharia za Kristo? *Ona utangulizi wa somo.* Kama wafuasi wa Kristo tunafunga na kutoa fedha tukiwa na motisha tofauti kabisa kuliko ule wa sharia ya kale.

## *Majadiliano*

### Ni kwa namna gani Mungu anatuongoza katika njia iliyonyooka? (# 1-5)



**Swali la 1:** Tazama picha mbili za kondoo.

- Ni ipi inayofanana na sharia zetu za kale na ni ipi inayofanana na sharia za Kristo? Tofauti ni ipi?

*Sharia za Kiislamu ni kama uzio, ambao umejengwa imara ili kuwatunza kondoo kukaa mahali pao sahihi. Kanuni zenye maelezo mengi huweka mipaka kati ya kipi kimekatazwa na kipi kinaruhusiwa. Kinyume chake katika Ukristo kuna kanuni chache na inaweza kuonekana kana kwamba hatufahami mipaka iko wapi. Lakini tunaye Kristo mwenyewe ambaye ni Mchungaji wetu. Ameahidi kuwaongoza kondoo zake mahali pazuri na kuwatunza salama.*

**Swali la 3-4:** Soma swali lote la 3 na paragrafu ya kwanza ya swali la 4.

- Ni kwa namna gani tunaweza kumsikia Kristo akizungumza nasi kwa Roho wake? *Roho huzungumza kupitia Biblia zetu kadiri tunavyosoma kila siku, kwa njia ya ukimya kwa dhamiri zetu, kwa kuleta wazo imara ndani ya akili zetu, au hisia katika roho zetu. Wakati mwingine husema nasi kwa sauti ya kusikika, kwa njia ya ndoto au sauti ya wazi. Pia husema nasi kupitia mausia ya waumini wengine.*
- Lakini, tunaweza kufanya makosa kwa kumsikiliza Roho Mtakatifu? *Ndiyo! Wakati mwingine tunafikiri ni sauti ya Mungu ilihali ni matamanio yetu tu mabaya. Lolote analosema Mungu kwetu halipingani na kile kilichoandikwa katika Neno lake – Biblia. Hivyo lazima tukague kile 'tunachosikia' kama hakipingani na Biblia!*

### Kufunga (Swali la 6-14)



**Swali la 6-7:** Soma paragrafu ya kwanza ya swali la 6 na maneno yaliyo kwenye kitufe.

- Je, una maswali yaleyale kama ya Parveen? Au maswali mengine kuhusu kufunga?
- Kutoka katika swali la 7, ni mambo gani mawili yanayoweza kumsaidia Parveen kupa ya maswali yake?



**Swali la 8: Kwa nini tufunge?** *Wagawe wanafunzi katika vikundi vitatu na kila kikundi ukigawie kifungu cha kutumia wakati wa kujibu swali. Au mpitie kila kifungu kwa pamoja.*

- Katika maswali yafuatayo, kwa nini watu walifunga?

**Danieli 9:3-5**– *toba ya dhambi, kutubu na haja.*
**Zaburi 35:13**– *kuombea mtu aliye katika uhitaji.*
**Matendo ya Mitume 13:2-3**– *kuabudu, maombi kwa ajili ya umisheni na kutafuta hekima kwa ajili ya maamuzi.*

**Swali la 12: Tufunge wakati gani?** Soma swali.

- Lini tufunge? Je, kufunga ni lazima au hiari kwetu? *Roho atatuongoza katika kufunga.*

**Swali la 13:** Soma swali lote la 13, ukijumuisha sehemu ya 'sitisha na ufikiri' iliyokolezwa wino.

- Nini majibu yako binafsi kuhusu swali hili?

**Swali la 14:** Soma swali lote la 14, kama hili ni suala linalokubalika katika muktadha wenu.

- Uliandika sababu zipi za kukubaliana na kutokukubaliana na Parveen kufunga pamoja na familia yake wakati wa Ramadhani?

***Sababu:*** *anaweza kuonesha uaminifu kwa familia yake hata kama yeye ni mfuasi wa Kristo. Anaweza kufunga na kuomba pamoja na familia yake ili kupata wokovu. Kama hafungi, inaweza kusababishwa matatizo yasiyo ya lazima na familia yake itawaza kwamba wafuasi wa Kristo hawana akili sawasawa.* ***Sababu dhidi ya:*** *Wanaweza kuwaza kwamba bado anafuata Uislamu au anafanya hivyo kwa sifa ya kidini. Anaweza kushawishika na njia zake za fikra za awali kwamba ni kwa sifa ya kidini tu.*

- Ni kwa kiasi gani uamuzi wa Parveen unategemeana na mazingira yake? *Mfano: inategemeana kama yuko pamoja na familia yake na wote ni Waislamu wenye itikadi kali. Kwa wale wanaoishi kwa kujitegemea wanao uhuru zaidi wa kuchagua.*
- Vipi kuhusu wewe, katika mazingira yako?

## Utoaji (Swali la 15-25)

**Swawli la 15:** Soma paragrafu ya kwanza na maneno yaliyomo kwenye kitufe chenye maneno.

- Je, una maswali sawasawa na Khalid? Au maswali tofauti kuhusu utoaji?



**Swali la 16-19:** Soma swali lote la 16 na nusu ya kwanza ya swali la 17.

- Ni kwa kiasi gani male zetu ni mali ya Mungu?
- Je, tuweke ukomo wa kiasi gani tunamrudishia Mungu?

**Soma 2 Wakorintho 9:6-15:**

Omba wanakikundi wasome mstari mmoja au mistari miwili kila mmoja, kwa kuzunguka l ili kwamba kila mmoja apate kitu cha kusoma.

*Baada ya kusoma, toa dakika moja ya ukimya kwa kila mtu kufikiri kuhusu maana yake.*

- Tafadhali kila mtu aeleze kwa maneno yake mwenyewe maana ya mstari au mistari uliyosoma.

**Swali la 21:** Soma swali. Nini jibu lako kwa swali hili, na kwa nini?

**Swali la 24:** Soma swali lote.

- Uliandika nini hapa? Ni kwa namna gani unaweza kuitunza fedha na usiitumie?
- Kama huna kipato, ni njia gani mbadala unazoweza kumtolea Mungu? *Mfano: muda wetu, huduma za kujitolea nk. Lakini watu wengi huwa angalau na kiasi fulani cha fedha na tunapaswa kujifunza kumtolea Mungu katika hizo. Hata watoto wanaweza kutoa kutokana na mapato yao madogo wanayopata.*

**Swali la 25:** Soma swali. Uliandika nini hapa? *Mawazo hujumuisha: kuwasaidia maskini, siyo tu ndugu zetu wa damu. Kununua vitabu vya injili au vitabu kuhusu Yesu na kuvigawa kwa watu wanaopenda ambao siyo Wakristo. Kuchangia katika kikundi chetu. Kuchangia waumini katika huduma za Kikristo wakati wote, ndani ya nchi yetu au nje ya nchi.*

## Sheria ya upendo (Swali la 26)

**Swali la 26:** Soma swali.

- Ni kwa namna gani kufunga inaweza kuwa njia ya kutii sheria ya upendo? *Tunajikana wenyewe kwa upendo kwa ajili ya Mungu, kumtanguliza yeye kwanza kabla ya njaa yetu. Pia, pale tunapofunga na kuombea watu wahitaji, hiyo huonesha upendo wetu kwake.*
- Kwa nini kutoa fedha ni moja ya njia ya kuitii sheria hii ya upendo? *Maana tunaonesha upendo wetu kwa Mungu kwa kumrudishia fedha, na upendo wetu kwa watu wengine kwa kutumia fedha ili kuwasaidia.*

| ***Mwisho*** | |
|---|---|
| **Kutii somo la leo:**<br>• Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?<br>• **Someni kwa pamoja shughuli ya kivitendo.** Usifikirie tu kutenga fedha kwa ajili ya kumpa Mungu, anza mwezi huu!<br>*Kama unataka, panga siku ya maombi na kufunga kama kikundi. Wote mnaweza kufunga kwa siku moja na kukutana pamoja kwa ajili ya maombi, kwa mfano kwa ajili ya hitaji maalumu.* | **Omba**: kwa dakika chache za ukimya, mwombe Mungu atuonesha kila mmoja wetu namna na lini tunaweza kufunga, na ni kiasi gani anataka tumtolee. Kisha ombeni katika vikundi tukimwomba atusaidie tuwe wakarimu & kuwa na nidhamu katika mambo haya. |

# Somo la 18: Majaliwa na Uchawi

**Malengo kwa wanafunzi:**
a. Kuwa na uhakika wa kweli kuu tatu za kibiblia kuhusu majaliwa na uchawi.
b. Kufahamu kwamba Mungu yuko karibu na anatujali.
c. Kushughulika na ushawishi wowote wa madhehebu yasiyo ya kweli kutokana na maisha yao ya kale. d. Kariri 1 Petro 5:7.

**DOkezo za kitamaduni:**
- Waislamu na uchawi
- Waislamu na nguvu za kiroho
- Kutoa faraja

**Andaa:** Kadiri unavyojiandaa na kuongoza somo hili kama kiongozi dai ushindi wa Kristo katika ibada, na katika kutubu dhambi. Wasihi wengine pia waombee somo hili. Majadiliano yanaweza kufunua ushawishi wa madhehebu yasiyo ya Kikristo, kutegemeana na mazingira yao, hivyo ni muhimu kuwa macho kiroho. **Lazima uanze na kuhitimisha somo kwa ibada na maombi, mkitangaza ushindi wa Mungu kwa pamoja.**

## *Kufungua*

**Shughuli ya kivitendo kwa wili iliyopita:** Je, uliamua na kutendea kazi, utatenga fedha kiasi gani kila mwezi kwa ajili ya kumrudishia Mungu? Au umewaza njia zingine za kuweza kutoa kwa ukariamu?

**Somo la 18 marudio ya kujisomea nyumbani:** **Swali la 1**: a) majaliwa; b) chukia; c) nguvu **Swali la 2:** fadhaa zako zote kwake, maana anajishughulisha sana na maisha yako (1 Petro 5:7)

**Tambulisha mada ya leo:** Ni nani aliye na nguvu zaidi ulimwenguni? Mungu ana uweza wote, na Mwana wake Yesu Kristo alimshinda Shetani na nguvu zote za giza. Leo tutajifunza kwa nini, kama wateule wa Mungu, hatupaswi kuishi kwa hofu ya kitu cho chote – yaweza kuwa majaliwa, majini, au jicho ovu.

## *Majadiliano*

### Utangulizi & Swali la 1

**Ombeni kwa pamoja kabla ya Swali la 1.** Katika mada hii ya majaliwa na uchawi, yule mwovu ametuambia uongo mwingi sana. Watu wengi wameuamini uongo huo kwa karne nyingi, hivyo wanaendelea kuwa chini ya nguvu za Shetani. Yawezekana hayo mawazo mabaya ambayo hukaa akilini mwetu pia. Hebu leo tuyavunje kwa kutumia kweli ya Mungu!

**Swali la 1:** Soma swali. *Ruhusu wanafunzi washirikishe mazingira yao na ufahamu wao.*
- Maoni yako **hasa** ni yapi: 'ndiyo', 'hapana' au 'sina hakika'? Ni kwa namna gani ulijenga oni hilo?

### Mungu huongoza maisha yetu, siyo majaliwa (Swali la 2-9)

**Swali la 2:** Soma swali na utazame mchoro *(mawazo ya uongo ya watu).*
- Je, umewahi kuamini kwamb Mungu huko mbali sana hawezi kujali? Hili limebadilikaje kwako?

**Swali la 3:** Tazama mchoro huu *(pamoja na maneno yaliyojazwa katika nafasi zilizoachwa wazi).*
- Je, unawajua watu wanaofikira hayo majaliwa, na jicho ovu kuwa vinaathiri maisha yao ya kila siku?
- Kulingana na Biblia, je, mambo haya yapo? *Ndiyo (ingawa Wakristo hutofautiana katika ufafanuzi).*

**Swali la 6:** Tazama picha na usome swali.
- Uliandika nini kwa sehemu ya a)? What about part b)? Why these answers?
- Wakati mwingine utakapoteseka wewe mwenyewe, je, usemi wa 1 utakufariji au usemi wa 2?

**Swali la 7:** Soma mchoro: 'Mungu yukoje'.
- Nini kilicho cha tofauti katika mchoro huu ukilinganisha na ule ulio katika swali la 3? *Mungu, badala ya kuwa mbali, hushuka chini kwa njia ya Yesu Kristo. Hakika anatujali. Siyo kwamba yuko mbali asiweze kutujali.*

**Swali la 8:** Soma swali na fanya mazoezi ya kukariri mstari. Jaribu kufanya hivyo katika kikundi au mkiwa wawili:
- Mtu wa kwanza anauliza swali kwa mtu wa pili, "Una mashaka gani siku hizi?"
- Mtu wa pili anatoa majibu yao binafsi. Kisha mtu wa kwanza anasema: "huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu (1 Petro 5:7)". Mtu wa pili anafanye vilevile kwa mtu anayefuata, na kuendelea mpaka kila mmoja katika kikundi amehusika, ukiwemo na wewe kama kiongozi mwishoni kabisa.

## Mungu huxhuki uchawi na ibada ya sanamu (Swali la 10-17)

**Swali la 10:** Soma swali.

- Uliandika nini hapa?

*Waislamu wa nchi za Magharibi, kwa namna fulani bado huwa wameshikwa na imani zao za msingi. Waulize kuhusu tamaduni za familia zao.*

**Swali la 11-15:**

- Ni matendo gani yanayotajwa katika maswali haya? *Baadhi yake ni maneno magumu, hivyo uwe tayari kueleza maana zake. Usifungue Biblia sasa maana somo la kujisomea Biblia ni baadaye.*
- Nia ya Mungu kwayo yote ni ipi? *Anayachukia, na anayakataza.*
- Kwa nini mateando haya ni aina ya ibada ya sanamu (swali la 15)? *Matendo haya ni kama ibada ya sanamu kama watu wanayatumaini na kuyatii kuliko Mungu, maana yanaweka mambo yaliyoumbwa mahali pa Muumbaji.*


**Swali la 16:** Soma kitufe chenye maneno. Ni ushauri gani utakaompatia mwanamke huyu?
***Baadhi ya mapendekezo:*** *Zaidi ya yote, anapaswa kufahamu kwamba Mungu anamjali sana. Anahisi huzuni zake. Yule 'mtu mtakatifu' hayuko karibu na Mungu kuliko mwanamke huyu, ukweli ni kwamba yuko ndani ya Kristo na yeye yuko karibu naye zaidi kuliko yule mwanamume. Hapaswi kufuata mabwana wawili, yaani, Kristo ni bwana wake au yule mtu mtakatifu. Awaombe waumini wengine waombe kwa ajili yake ili Mungu ampe mtoto. Lakini kusudi lake ni zuri sana, ama ana mtoto au la.*

## Yesu anatawala juu ya nguvu zote za kiroho (Swali la 18-21)

**Swali la 18-19: Soma na ujadili vifungu viwili vya Biblia.**

- **Marko 1:21-27.** Katika mstari wa 22, ni nini kilichowashangaza watu kuhusu Yesu? *Alifundisha kwa mamlaka.*
- Ni kwa namna gani Yesu alithibitisha mamlaka yake kwa vitendo? *Aliamwamuru pepo mchafu na akatii.*
- Katika mstari wa 24, yule pepo alitambua mambo gani mawili muhimu kuhusu Yesu? *1. Yesu alikuja kuangamiza pepo wabaya. 2. Yeye ni Mtakatifu wa Mungu.*
- Ni kwa namna gani watu waliitikia katika mstari wa 27? *walishangaa kuliko hapo awali.*

- Ona mchoro katika swali la 19 na **soma 1 Petro 3:21b-22** (kuanzia nusu ya mstari wa 21) Ni kweli zipi zinazooneshwa na mshale unaoonesha kuelekea juu? *'ufufuo wa Yesu Kristo', 'amekwenda zake mbinguni', 'mkono wa kuume wa Mungu'.*



- Uliansika nini kwenye mduara? *malaika, enzi, nguvu.*
- Katika mchoro huo, ni nani aliye juu ya majini na nguvu za kiroho?
- Katika mchoro huo, sisi tuko wapi? *Tumeketi pamoja na Kristo & kutawala, Waefeso 2:6.*
- Kama mtu akikulaani, ni nani aliye na nguvu kuliko laana hiyo?

**Swali la 21:** Je, kuna mmoja wetu aliye na uzoefu wa Kristo akiwashinda pepo wabaya?

- ***Soma sehemu iliyo ndani ya mabano.*** Baadhi yenu mnaweza kuwa na mashaka kuhusu pepo wabaya, tafadhali tuzungumze nami baadaye au mwumini ye yote aliye na uzoefu.

## Je, tunaweza kuwatumikia mabwana wawili? (Swali la 22-24)

**Swali la 23:** Soma habari hiyo. Uliandika jibu gani?

- Kubuka usemi huu, 'Kama Yesu siyo Bwana wa yote, basi siyo Bwana kabisa!'
- Leo tumezungumzia kweli tatu muhimu za kuvunja uongo wa yule mwovu. Ni upi huo?

*1. Mungu huongoza maisha yetu, siyo majaliwa. 2. Mungu huchukia uchawi na ibada ya sanamu. 3. Yesu anatawala juu ya nguvi zote za kiroho.*

- Unajisikiaje baada ya kuhitimisha mjadala wa leo?

| ***Mwisho*** | |
|---|---|
| **Kutii fundisho la leo:**<br>• Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?<br>**Someni pamoja shughuli ya kivitendo:** Pitia kwa makini maswali yote. Mwombe Mungu akukumbushe hali yo yote ile iliyopita pale ambapo mambo hayo yalishawishi maisha yako. Kama kulikuwa na ushawishi wa aina kama hiyo, mwombe mwumini mwingine akusaidie kuomba dhidi ya hilo. | **Omba & abudu pamoja:**<br>Simama na utangaze hadharani kweli hizi tatu dhidi ya yule mwovu: Mungu huongoza maisha yetu, siyo majaliwa. Mungu huchukia uchawi na ibada ya sanamu. Yesu Kristo hutawala juu ya nguvu zote za kiroho. |

# Somo la 19: Kutumikiana kila mmoja na mwenzake

| Malengo kwa kila mwanafunzi: | Dokezo za kitamaduni: |
|---|---|
| a. kujidhatiti kutumia karama zao kwa unyenyekevu, ili kutumikiana kila mmoja na mwenzake.<br>b. Kuwasaidia viongozi wa kanisa na kufahamu wajibu wao.<br>c. Kariri 1 Petro 4:10. | • Kutawadha miguu kwa Kiislamu<br>• Mambo ya kiuongozi kwa vikundi vya BMBs<br>**Andaa:** Taulo, sabuni, beseni, maji moto |

## *Kufungua*

**Shughuli ya kivitendo kwa wiki iliyopita:** Je, ulikagua kuona kama kulikuwa na ushawishi wa kichawi katika maisha yako ya awali? Je, uliomba pamoja na mtu fulani? Kama bado una mashaka kuhusu hili, basi nione binafsi.

**Somo la 19 mapitio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1**: a) tofauti; b) kila; c) kwa ajili ya huduma
**Swali la 2:** "kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu.*"* (1 Petro 4:10).

**Tambulisha mada ya leo:** MUngu ametupatia karama nyingi na vipawa vingi. Leo tutajifunza namna ya kuzitumia karama hizi ili kumtumikia Mungu na kuhudumiana kila mmoja na mwenzake. Hata viongozi ni lazima wawatumikie watu wao!

## *Majadiliano*

### Kuhudumiana kila mmoja na mwenzake (Utangulizi & Swali la 1-3)

**Tafakuri juu ya picha ya ufunguzi:** Yesu alitawadha miguu ya marafiki zake wa karibu usiku ule




kabla hayaangikwa msalabani. **Soma YOhana 13:3-5,12-17**. *Kisha polepole, kwa vituo:*
"*Tazama mikono katika picha hii. Fikiria kwamba ni mikono ya Kristo."*
*"Tazama miguu na fikiria kuwa ni miguu yako. Kristo anatawadha miguu yako!"*
*"Unajisikiaje kuhusu hili? Zungumza na Bwana wako kuhusu hili sasa ndani ya moyo wako."*
**Mihemuko gani iliibuka pale tulipofikiria kuhusu Bwana Yesu Kristo anatawadha mituu yetu?**

**Swali la 2:** Soma swali.
- Katika tamaduni tunazotoka, je, viongozi huwatumikia wafuasi wao?
- Lakini kiongozi wetu mkuu Yesu Kristo aliinama na kutawadha miguu yetu. Kwa hiyo, tufanye nini kama mwitikio wetu?
- Je, viongozi watapoteza heshima yao kwa watu kwa kuwatumikia kama Kristo alivyofanya?

*Ona kisanduku katika # 1. Anasema, "nimewaachia kielelezo". Tunamshukuru kwa kututumikia sisi, na sisi pia lazima tuiname chini ili tuwatumikie wengine. Mwisho, viongozi kama hao watapata heshima.*

### Karama ni kwa ajili ya huduma (Swali la 4-8)

**Soma 1 Petro 4:10-11 na rudia mstari wa kukariri 1 Petro 4:10).**



- Katika ms. 10, ni kwa namna gani tunaweza kutumia karama alizotupatia Mungu? *Kuwatumikia wengine*
- Kwa nini unadhani tunapaswa kuwa kama 'mawakili waaminifu'? *Tunapaswa kuwa kama msimamizi mwaminifu ambaye hamiliki mali za bwana wake, bali huzitumia vizuri kwa niaba ya mwenye mali.*
- Vifungu mbalimbali vya Biblia hutaja karama nyingi. Ni karama mbili zipi zinazotajwa katika mstari wa 11?
- Ni kwa namna gani watu hao wawili katika ms. 11 wanaweza kuzitumia karama zao?
- Tunapaswa kuzitumia karama zetu kwa utukufu wa Mungu. Hebu tuiseme kwa sauti sehemu ya mwisho ya mstari wa 11.

### Watu mbalimbali wana karama mbalimbali people (Swali la 9-10)

**Swali la 9:** Soma habari iliyomo kwenye kisanduku na paragrafu inayofuata.
- Uliandika nini hapa? *Kwa mfano: sisi sote tuna maeneo tunayofanya vizuri lakini pia yapo maeneo tunayofanya vibaya. Sisi sote, kwa njia moja ama nyingine ni 'vipofu' au 'vilema'. Hakuna mmoja wetu aliye mkamilifu kabisa kwa yeye mwenyewe. Lakini udhaifu wangu ni nguvu yako. Hivyo tunahitajiana katika kikundi chetu cha waumini.*

## Kila mmoja wetu ana karama (Swali la 10-14)

**Swali la 11:** Tazama picha.




- Fayzia amepewa karama gani na Mungu?
- Ni kwa namna gani Laila alimsaidia Fayzia kuitambua karama yake?

**Swali la 13:**

- Tunawezaje kuzitambua karama zetu? *Ona ile mishale mitatu.*
- Mwanakikundi mmoja, tafadhali taja njia moja ya kutumika. Mtu anayefuata arudie kutaja hiyo na aongeze nyingine. Hebu tuendelee kuongeza kadiri tunavyoweza. *Kwa mfano: kuongoza vikao, kufundisha Biblia, kupiga chombo cha muziki, kutunza kikundi, maombi, kutia moyo watu wengine, kuwafikia wasioamini, msaada kwa vitendo, msaada wa kifedha, kupika, n.k.*
- Ni kwa namna gani aina hizi mbalimbali za huduma zinaweza kusaidia kukijenga kikundi cha waumini?

## Lazima tuzitumie karama zetu kwa unyenyekevu (Swali la 15-18)

**Swali la 15:** Soma swali.

- Uliandika sababu zipi kwa Samir akiwa kiongozi wa kikundi? Ni sababu zipi dhidi yake?
- Ni kwa namna gani kikundi kinaweza kumsaidia Samir kukua katika suala la uongozi bila kuwa na kiburi?

*Muumini aliyekomaa kiroho anaweza kusema na Samir kuhusu nia yake ya kiburi. Pia, Samir anaweza kupewa wajibu kidogo chini ya kiongozi mwenye mamlaka. Kama atafanya vizuri, akiwa na nia njema, anaweza kupewa wajibu zaidi. Pia, kama atakuwa kiongozi asiachwe peke yake, bali awe katika timu ya watu wawili au zaidi ya viongozi wanaofanya kazi kwa pamoja.*

**Swali la 17:** Soma swali.

- NI nani aliye wa muhimu katika macho ya Mungu, mtu anayehubiri au mtu anayehudumia wakati wa chakula?

*Wote wawili ni wa muhimu. Lazima tuwashukuru wale wanaohubiri na wale wanaohudumia wakati wa chakula.*

## Kutumika kama viongozi (Swali la 19-25)

**Swali la 21:** Tazama orodha ya tabia zilizoko mwishoni mwa swali hili.

- Ni sifa zipi katika hizi ambazo Yesu ambaye Mchungaji Mkuu alizionesha? *a), b) & e).*
- Ni kwa namna gani kiongozi anayemfanana Kristo anaweza kuonesha tabia hizi kwa vitendo?

**Soma 1 Petro 5:1-6:**

- Katika mstari wa 2-3, tafuta njia tatu ambazo kiongozi anayemfanana Kristo anaweza kuwa ni wa tofauti na wale viongozi wa kidunia. *Kama kuna mashaka, ona swali la 22*
- Mstari wa 4 unatoa ahadi gani kwa viongozi kama hao?
- Ni kwa njia gani waumini wanaweza kuwasaidia viongozi wao katika majukumu yao magumu?. *watii (ms.5a), waombee, waheshimu, watie moyo, uwe na shukrani kwa ajili yao, usiwalalamikie wala kuwasengenya.*
- Katika mstari wa 5b na 6, ni nia gani tunayopaswa kuwa nayo wakati wa kuzitumia karama zetu?

**Swali la 25:** Soma paragrafu ya pili.

- Uliandika nini hapa?

**Kila mmoja kwa pamoja, soma kitufe cha mwalimu chenye maneno mwishoni mwa # 25.**

*Mfano: kiongozi anayehudumu bado ni kiongozi. Wana mamlaka ya kuongoza na watu lazima wawaheshimu. Heshim yao haitokani na hofu bali upendo. Kiongozi huwatumikia kwa kujitoa dhabihu mwenyewe kwa ajili ya manufaa yao.*

| ***Mwisho*** | |
|---|---|
| **Kutii fundisho la leo:**<br>• Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?<br>• **Soma kwa pamoja shughuli ya kivitendo. -** Je, una namna yo yote ambayo unaweza kutumia karama yako kuwatumikia wengine? | **Fanya kwa vitendo kuwatumikia wengine:** Mpeane zamu za kutawadhana miguu (wanaume peke yao na wanawake peke yao). Wewe kama kiongozi lazima uanze!<br>**Omba pamoja:** Fikiri tena kuhusu Kristo akitawadha miguu yetu. Mwombeni atuoneshe namna tunavyopaswa kuwatumikia watu, na atusaidie kuwatumikia wengine kama alivyotutumikia sisi. |

# Somo la 20: Hija yetu kwenda mbinguni

**Malengo kwa kila mwanafunzi:**
a. kuwa na uhakika kwamba watawafika paradiso wakiwa salama na kuitarajia kwa furaha.
b. Kujifunza kutambua na kupinga mashambulizi ya yule mwovu.
c. Kariri 1 Petro 5:10-11.

**Dokezo za kitamaduni:**
- Waislamu, kuhiji & Paradiso
- Yerusalemu & Usayuni

**Andaa:** Andika au chapa nukuu hii (ona swali la 22) pamoja 'nasi' na 'sisi'. Panga kusherehekea hitimisho la kozi hii, mfano, kwa kikao mkishirikishana shuhuda na kupata chakula cha pamoja.

## *Kufungua*

**Anza kwa maombi kasha rudia shughuli ya kivitendo:** Je, umekwisha kumwuliza rafiki yako kuhusu karama uliyo nayo? Walisema nini? Je, umepata muda wa kuwatumikia wengine kwa wiki hii? *Kila mmoja azungumze.*

**Swali la 20 marudio ya kujisomea nyumbani:**
**Swali la 1:** a) Yerusalemu; b) mbingu (au paradiso) **Swali la 2:** a) nasi; b) Kristo
**Swali la 3:** ni nani aliyekuita katika utukufu wa milele katika Kristo, baada ya kuteseka kitambo, yeye mwenyewe atakurejesha na kukuimarisha, imara na bila kutikisika; nguvu ya milele (5:10-11)
**Swali la 4:** Majibu binafsi. *Mungu anataka tuwe na uhakika kabisa. Hatutapita katika mateso kwanza, bali tutakwenda kuwa na Mungu huko paradiso pale tutakapokufa! Kama kuna mtu ambaye bado ana mashaka, waoneshe katika kitabu cha Luka 23:39-43 kwamba Yesu alimwahidi mharifu 'Leo hivi utakuwa pamoja nami peponi'!*

**Tambulisha mada ya leo:** Tuko katika safari ndefu ya kwenda mbunguni, au paradiso. Tuna hatima ya utukufu, lakini humo safarini lazima tupigane na adui yetu, yule mwovu. Leo tutajifunza kuhusu safari yetu hii ya kiroho.

## *Majadiliano*

### Safari yetu ya kiroho (Swali la 1-5)

**Swali la 2-3:** Soma swali lote la 2 na paragrafu ya kwanza ya swali la 3.
- Ni aina gani ya kuhiji au safari tunayoiendea kama wafuasi a Kristo? *Ni safari ya kiroho ambayo inadumu maisha yetu yote. Tunasafiri kuelekea nyumbani kwetu mbinguni.*
- Sikuhizi wafuasi wa Kristo wanapoomba, kwa nini hawageukii Yerusalemu? *Kwa sababu maombi yetu na maisha yetu havipaswi kuelekea mji wo wote wa kidunia, bali kwa Mungu mwenyewe.*

**Swali la 4:** Soma swali, ikiwemo sehemu ya 'Sitisha na Fikiri'.
- Je, ulifikiri kuhusu hili na uliamua nini?

### Mpingeni Shetani (Swali la 6-16)

**Swali la 1 Petro 5:6-11**



- Ni kwa namna gani mstari wa 6 unaweza kutusaidia pale tunapokuwa na kiburi? *Hutusaidia kuwa wapole.*
- Ni kwa namna gani mstari wa 7 unatusaidia tunapofadhaika? *Hutupatia ahadi imara, kwamba Mungu anatujali!*
- Kuingana na mstari wa 8, ni nani aliye kama simba 8? *Yule mwovu.*
- Kulingana na mstari wa 9, je, tunaweza kumpinga? *Ndiyo, kama 'tutasimama imara'.*
- Soma mstari wa 10-11 kwa pamoja na kwa sauti moja mpaka kila mmoja aweze kuikariri.

**Swali la 7:** Soma swali lote na shirikisha kile ulichoandika katika sehemu tatu:
- Ni kipi kinachoweza kuwadhoofisha wafuasi wa Kristo? *K.v. kama wataacha kuomba na kusoma Neno la Mungu. Au kama watajificha kwa muda mrefu sana kuwa wao ni wafuasi wa Kristo (ingawa kujificha kwa muda ni SAWA).*
- Ni mambo gani yanaweza kuwafanya wafuasi wa Kristo waikeshe? *K.v. Pale wanaposhindwa kutambua kwamba yule mwovu anawajaribu. Hivyo wanaweza kuanguka dhambini, kama vile kiburi, hasira au dhambi ya ngono.*
- Ni mambo gani yanaweza kuwaondoa wafuasi wa Kristo katika kundi? *k.v. kama wakiacha kukusanyika pamoja na waumini wengine kwa ajili ya jumuiya, kwa mfano kama wameolewa au kuoa mtu asiye Mkristo.*

**Swali la 11:** Soma paragrafu ya kwanza.

- Wakati mwingine magumu yetu huonekana kuwa ni makubwa mno mpaka tunafikiri kwamba hatuwezi kuvumia tena! Lakini **soma 1 Wakorintho 10:13**. Hii inatupa tumaini gani?
- Je, unaweza kuelezea tukio ambalo ulidhani kwamba huwezi kuvumilia zaidi ya hapo? Ni kwa namna gani Mungu alikupatia nguvu ya kukabiliana nalo? *Mpe fursa kila mmoja aweze kusema bila shinikizo lo lote.*

**Swali la 12:** Tazama picha ya swali la 12.

- Ni waumini wawili wapi wanaoshambuliwa kutokana na magumu ya nje? *Gul (b) na Iftikhar (d)*.
- Ni yupi kati yao wawili anashambuliwa kupitia majaribu ya ndani? *Akhtar (a) na Shireen (c).*
- Elezea wakati ambapo Shetani alikushambulia kwa magumu ya nje au majaribu ya ndani. Nini kilitokea? Ulijifunza nini kutokana na hilo? *Hili ni muhimu, ruhusu muda wa kila mmoja kusema.*

**Swali la 15-16:** Tazama picha ya swali la 15. Soma swali lote la 16.

- Wakati wowote tukikutana na msumari barabarani, ni uamuzi gani tulio nao?
- Yule mwovu hutujaribu ili tuifuate njia yake. Ni nani anayepaswa kufanya uamuzi wa kupinga jaribu hilo – sisi au Kristo? *Lazima sisi tufanye uamuzi. Kama tutafuata njia ya yule mwovu ni kosa letu, siyo la Kristo.*
- Kwa Akhtar na Shireen katika swali la 12, ni nani anayepaswa kuchagua kugeuka kutoka katika jaribu? *Lazima wachague wao wenyewe*. Ni nani atakayewasaidia kufanya uamuzi sahihi? *Kristo*
- Pale yule mwovu anapotujaribu, tunaweza kumpinga kama tutafanya uamuzi huo. **Soma 1 Yohana 4:4,** Kristo yumo ndani yetu na ndiye aliye mkuu kuliko Shetani!

## Hatima yetu mbinguni (Swali la 17-22)

**Swali la 19:** Soma swali.

- Ni kwa namna gani tunaweza kuwa na uhakika kwamba Mungu atatupokea paradiso?

*Yesu Kristo mwenyewe atatuvusha daraja hadi kuingia paradiso. Tumemtegemea yeye, na kamwe hatatuacha tuanguke!*


**Swali la 21:** Soma habari ya kweli kuhusu Umar *(ndani ya kisanduku).*

- Unategemea kiasi gani kuingia mbinguni: kidogo au kwa wingi?
  *Jadilini pamoja. Ni sawa kuwa na furaha na kutimiza kumtumikia Mungu hapa duniani, bali hatupaswi kuyaondoa macho yetu kwenye hatima yetu ya kweli, mbinguni! Naomba tutamani zaidi na zaidi kama Umar!*

**Swali la 22:** Soma swali lote.

- Ni maneno gani katika kifungu hiki unayoyapenda zaidi?
- Ni ahadi gani za ajabu zilizopo kwenye kifungu hiki! Hebu tukisome tena, tukiweka badala ya 'wao' iwe 'sisi'.

*Mwombe kila mwanafunzi aseme, na wewe pia washirikishe.*
***Ili kuwasaidia wanafunzi wako, andika au onesha kifungu mapema kukiwa na mabadiliko yaliyofanyika tayari;*** *k.v."Tutakuwa watu wake, na Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nasi na kuwa Mungu wetu. Atafuta kila chozi katika macho yetu" n.k.*



**Swali la 22:** Tazama picha katika ukrasa wa mwisho na soma maneno.

- Unapata mihemuko gani?
- Hebu waza kuwa Mungu anafuta machozi yetu yote huko paradiso!

## *Mwisho*

**Kutii fundisho la leo:**

- Somo la leo litaleta tofauti gani katika maisha yako?
- **Someni kwa pamoja shughuli ya kivitendo.** Kila siku kwa wiki hii, chukua kifungu kimoja cha maneno. Tafakari kwa kina. Kizungushe akilini mwako kama mtoto azungushavo pipi mdomoni mwake, akifurahia utamu wake kwa muda mrefu.
- **Sherehekea:** Ni kwa namna gani kikundi kitasherehekea kwa kuhitimu kozi hii? K.v. chakula cha pamoja wiki ijayo, kwa kutoa shuhuda za nini mlichojifunza katika kozi hii? Jadilini na mweke mpango.
- **Jadilini** ni kwa namna gani ufuasaji utaendelea, kama kikundi au katika mahusiano binafsi chini ya uelekezaji.

**Omba kwa pamoja:**

Kila mmoja afungue 1 Petro 5:8-11. Hivyo, kila mmoja aombe sala fupi kwa kuzingatia sehemu mbalimbali za kifungu hiki.
Ombea maalumu 'familia yetu ya waumini ulimwenguni kote walio na aina ileile ya mateso' (ms.9)

# Nyongeza: Chati ya Kukariri Mistari ya Biblia

| | | | |
|---|---|---|---|
| Somo la 1 | ***Mathayo 11:28***<br>“Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.” | Somo la 11 | ***Mwanzo 2:24***<br>“ Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.” |
| Somo la 2 | ***2 Kor 5:17***<br>“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama! Yamekuwa mapya!” | Somo la 12 | ***1 Petro 3:11***<br>“Na aache mabaya, atende mema; Atafute amani, aifuate sana.<br>.” |
| Somo la 3 | ***1 Yohana 3: 1***<br>“Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye!” | Somo la 13 | ***1 Petro 3:18***<br>“Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; akauawa kimwili, lakini akahuishwa kiroho.” |
| Somo la 4 | ***1 Petro 1:15***<br>“bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote.” | Somo la 14 | ***Mathayo 28:19***<br>“Basi, nendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.” |
| Somo la 5 | ***SALA YA BWANA***<br>“Baba yetu uliye mbinguni…”<br>nakuendelea | Somo la 15 | ***1 Kor 6:19-20***<br>“Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.” |
| Somo la 6 | ***SALA YA BWANA***<br>“Baba yetu uliye mbinguni…”<br>nakkuendelea | Somo la 16 | ***Marko 12:30-31***<br>“nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. 31 Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi.” |
| Somo la 7 | ***1 Petro 2:9***<br>“Bali ninyi ni uzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.” | Somo la 17 | ***Marko 12:30-31***<br>“nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. 31 Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi.” |
| Somo la 8 | ***1 Petro 2:17***<br>“Waheshimuni watu wote. Wapendeni ndugu. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme.” | Somo la 18 | ***1 Petro 5:7***<br>“huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu..” |
| Somo la 9 | ***1 Petro 2:21***<br>“ Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake.” | Somo la 19 | ***1 Petro 4:10***<br>“kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu.” |
| Somo la 10 | ***Mathayo 5:44***<br>“ lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi.” | Somo la 20 | ***1 Peter 5:10-11***<br>“Na Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika Kristo, mkiisha kuteswa kwa muda kidogo, yeye mwenyewe atawaimarisha, atawathibitisha, atawatia nguvu na kuwapa msingi imara. 11Uweza una yeye hata milele na milele. Amina” |